




SURA YA KWANZA

KARATASI ZA SIRI

Ilivyo ni kwamba mimi siku za Jumapili hulala mpaka saa tatu au saa nne. Na kama huamini hiyo si shida yangu. Ilikuwa Jumapili nyingine. Usiku wa jana, yaani Jumamosi, nilikwenda kwenye dansi na rafiki yangu mmoja msichana. Tulirejea nyumbani mnamo saa tisa na nusu za asubuhi. Kutokana na uchovu mwingi ulionielemea nikafahamu wazi kwamba Jumapili hii nitaamka kama saa tano hivi. Lakini utastaajabu nikikwambia kuwa Jumapili hiyo ilinibidi niamke saa kumi na moja alfajiri!

Kengele ya simu ililia mnamo saa kumi na moja, na miye nilikuwa nimelala saa moja tu hivi. Nilipuuza kuichukua kwani nakueleza nilivyochukia, Mungu ndiye anayejua. Iliendelea kulia na kulia, mwishowe nikaona nisipoijibu pia nisingeweza kulala kwa sababu ingaliendelea kuniudhi. Huyu binti aliyekuwa amelala karibu na hii simu naye aliamka, akaniomba afadhali niijibu. Basi kwa shingo upande, nilimwambia huyu binti anisogezee. Yeyote yule aliyekuwa amepiga hii simu nilikuwa mpaka sasa nimechukia kiasi cha kwamba angalikuwa karibu ningalimwuma.

“Hallo, huyu ni Chifu.” Nilisikia sauti ikisema.

Usingizi ulipotea papo hapo, nikajua kuna jambo, maana, S, anapojifahamisha kwa jina la Chifu jua kuna kazi, na kazi kubwa. “Halo, huyu ni Willy. Chifu mbona unapiga simu wakati kama huu? Nadhani ingefaa uwe kitandani, la sivyo utazidi kuzeeka upesi, kwa mtu wa makamo kama yako, “ nilimjibu.

“Sikiliza Gamba, hapa ninapopigia simu ni ofisini, na wala si nyumbani-kitandani kama ambavyo ungalifikiria. Na miye nakuhitaji hapa ofisini mnamo nusu saa bila kuchelewa. Kuna jambo la muhimu na la haraka, hili si ombi ila ni amri, asante sana,” alimalizia Chifu.

Nakueleza, hakika kweli, kuna wakati mwingine ninapochukia hii kazi yangu, lakini hata hivyo kwa mtu kama mimi nipendaye visa, nikiwa nasikia kuna jambo kubwa kubwa basi moyo nami huwa unanidundadunda ukiniambia nenda, huenda mara hii kuna visa zaidi.

Della ambaye ndiye msichana niliyekuwa naye hakupenda kuniona naondoka saa kama zile. Akaniambia,

“Willy hii ndiyo sababu nakuchukia. Sasa karibu tena uende kwenye masafari yako ya ovyoovy, hasa unapoitwa na hilo lijanaume linaloitwa liChifu. Kweli kama mara hii ukikubali kwenda miye naweza kufa.”

Nilimjibu Della nikisema, “Wajua kabisa ya kwamba hii ndiyo kazi yangu, ndiyo inayonipa unga, mboga na starehe za kila aina. Nisipofanya hizi safari, itakuwa kama wewe usipoenda ofisini.”

Kwa sababu Della ni msichana mwenye hekima alinyamaza na kuelewa nimesema nini. Kumwacha msichana huyu, na asubuhi kama hii amelala kitandani, na miye nikakimbia ofisini, ati kusudi nikapige ripoti kwa Chifu, moyo wangu ulidunda mara nyingi zaidi. Kama ninge hesabu wenda mapigo yangu yafika tisini kwa dakika moja. “Nitarudi mapema baada ya kumaliza shughuli na Chifu,” nilimwambia Della.

Nilifungua mlango, nikaangaza nje maana kulikuwa bado giza giza. Macho yalipozoea nikafunga mlango kwa nyuma, nikaenda kwenye gari langu. Nikaingia ndani na kuliwasha gari hilo. Kutoka kwangu ambako ni Upanga, mpaka ofisini kwetu ni mwendo wa dakika kumi. Kwa sababu wakati kama huu hakuna magari mengi nilitegemea kuchukua dakika tano hivi. Ingawaje ni kawaida ya Dar es salaam kuwa na joto jingi, asubuhi hii kulikuwa na baridi sana. Nilitia gari moto, nikashika barabara ya United Nations moja kwa moja mpaka Jangwani kwenye taa za 'traffic.' Nikaona hakuna gari ingawaje zilikuwa haziniruhusu kupita. Lakini nilienda tu. Nikaingia barabara ya Morogoro hadi Independence Avenue.

Nilipoingia Independence Avenue, niliona gari moja inakuja kwa nyuma. Na ilionekana kama kwamba ilikuwa imesimama katika barabara ya Morogoro wakati nikipita, kwa hiyo nikapunguza mwendo, na hiyo pia ikapunguza. Miye nilikuwa sipendi mtu yeyote ajue kuwa nilikuwa nikienda ofisini, saa kama zile. Na kwa nini hilo gari likawa linanifuata? Hiyo ndiyo pia nilikuwa sitaki. Nakwambia, kwa sababu nilishafutwa na magari mengi, mara moja tu naweza kutambua kuwa lile gari linanifuata hata anayenifuata awe mjanja namna gani. Wakati huu nilikuwa nimebakiwa na dakika kumi tu kuripoti kwa Chifu.

Nilikata shauri kurudi mara moja nikaone nani aliyekuwa ananifuata. Basi nilipiga kona na kuanza kurud. Hilo gari lilipoona nimerudi, likatia moto kuja kwa kasi sana. Likanipita na kwenda mwendo wa kama maili mia moja kwa saa. Dereva wa

hiyo gari alikuwa amejifunga shuka. Alikuwa amevaa miwani mweusi ya jua. Nikabahatisha kuwa, huyo alikuwa mtu ninayemfahamu, hivyo alivaa ili kusudi nisiweze kumtambua. Gari lake lilikuwa aina ya Datsun 160 SSS lakini alikuwa ametoa sahani ya namba.

Nilikata kona tena nikaendelea na safari yangu mpaka ofisini. Niliendelea mbele kidogo ya ofisi kusudi nione kama hilo gari lilikuwa karibu hapo. Ilionekana huyo jamaa alikata shauri kwenda zake. Nilianza kupanda juu ya jumba ambalo ndimo zilimo ofisi zetu hapo Independence Avenue karibu na jengo la Bima ya Taifa. Ilikuwa tayari saa kumi na moja na nusu. Niligonga kwenye mlango wa ofisi ya karani wa Chifu. Nilisikia sauti ya Maselina ikinikaribisha.

Nilifungua mlango na kuingia ndani. Nilimuhurumia sana Maselina maana naye alionekana mwenye usingizi mwingi. Nilipomuuliza alifika saa ngapi ofisini alinielesha kuwa Chifu alikuwa amempitia nyumbani kwake huko Magomeni Mikumi, yapata saa kumi hivi, wakati yeye alipokuwa amefika kutoka 'Afrikana Hoteli' ambako alikuwa ameenda kustarehe na rafiki zake. Akazidi kunieleza kuwa lazima kulikuwa na jambo kubwa sana kwani Chifu alionekana hana furaha kabisa.

Kweli Maselina alifaa sana kuwa karani wa Chifu, maana alikuwa msichana mwenye bidii sana ya kazi. Hata mimi nilimpenda kwa ajili ya bidii zake na pili alikuwa na umbo la kupendeza. Alizidi kunieleza kuwa Chifu alikuwamo ndani akiningojea. Maselina alimpigia simu Chifu na Chifu akamwambia aniambie niingie. Basi niligonga kwenye mlango ulioandikwa “MKURUGENZI WA UPELELEZI.” Nilisikia sauti ya Chifu ikisema;

“Ingia ndani Gamba.”

Nilipoingia ndani nilimkuta Chifu anavuta mtemba. “Kaa chini,” aliniambia. Sura yake ilionyesha kama kwamba kulikuwa na jambo ambalo hakulipenda. Alikaa kama dakika kumi hivi akiniangalia tu bila kunieleza neno. Hata miye mwenyewe nilijisikia sina furaha hata chembe. Kisha Chifu alitoa mtemba wake kwenye mdomo, akakung'utia majivu ya tumbaku katika sahani la majivu. Akaanza kutia tumbaku mpya. Halafu akainua macho yake na kuanza kusema,

“Sikiliza kwa makini sana tafadhali maana sitaki kuwepo makosa yeyote ambayo yanaweza kuleta hatari. Habari niliyonayo ni muhimu sana, hivyo kwamba, kosa la mtu mmoja tu, linaweza kuleta maangamizi ya Afrika nzima.”

“Mnamo usiku wa manane, nimepokea simu nyumbani kwangu ikitoka kwa mkubwa wa Polisi. Mkubwa wa Polisi alinielesha ya kwamba, ofisi moja ya

wapigania uhuru imebomolewa. Na kwamba karatasi fulani za siri zimechukuliwa.” Alipofika hapo Chifu alionekana hana furaha katika kutaja neno hili 'zimechukuliwa.' Aliendelea kusema;

“Na polisi wanafikiri kwamba jambo hili limefanyika kati ya saa nne usiku na saa tano. Askari Polisi aliyekuwa akilinda amekutwa amekufa kwa kupigwa risasi tatu kifuani. Polisi walifika hapo ofisini yapata saa tano kamili, baada ya kupigiwa simu na mtu mmoja aliyeiona hiyo maiti ambayo ilitupwa barabarani. Mtu huyo alikuwa akitoka dansini akielekea nyumbani kupitia mtaa wa Nkurumah.

“Polisi walifika na Dakitari. Daktari alieleza kwamba huyo askari alikuwa amekufa yapata saa moja iliyopita, ambayo ilionekana ilikuwa saa nne. Mkubwa wa wapigania uhuru alifika baada ya kupigiwa simu na akachunguza vitu vilivyopotea. Ilionekana kwamba kila kitu kilikuwemo ila kabati moja la chuma ambamo mlikuwa na karatasi za siri, kufuli la kabati hilo lilifunguliwa kwa kutumia bastola .45. Karatasi hizo zilizochukuliwa ni za maana sana kwamba lazima 'kwa njia nzuri ama mbaya' zipatikane. Maana zisipopatikana, zinaweza kuleta maangamizi kwa wapigania uhuru na kwa nchi huru zote za Afrika.”

Alipofika hapa mimi nilisema, “ingefaa unieleze jinsi ninavyohusika katika mambo haya, maana mpaka sasa bado inaonekana hakuna jambo au kiini cha kuweza kuzipata iwapo hawamjui mtu yeyote aliyehusika na mambo haya.”

Chifu hakusita kupanua midomo kunieleza, “baada ya kuelezwa yote haya, imeonekana kwamba. Na pia wakuu wa serikali wanafikiri kuwa wizi wa karatasi hizi, Ureno na Afrika ya Kusini ndiyo wako nyuma ya mambo yote haya, pia Indonessia. Lakini watu waliofanya au waliozichukua hizo karatasi ni watu au majambazi wa papa hapa Afrika ya Mashariki. Maana kutokana na wizi wenyewe ulivyotokea, imeonyesha kwamba ni watu wenyeji wa Afrika ya Mashariki tu wanaweza kuendesha wizi huu.

“Mimi sasa ninavyofikiria ni kwamba hizo karatasi zina mambo yote jinsi wapigania uhuru wanavyoweza kufaulu katika mambo yao. Kwa hiyo wakafanya jitihada wazipate, lakini hawakuweza, maana wapelelezi hao wote wamekamatwa kama unavyojua. Hivyo wakaona jambo wanaloweza kufanya ni kuwafuata majambazi katika Afrika Mashariki ambao haja yao kubwa ni pesa. Sasa basi, hao watu wakafuata hao majambazi na kuwambia kuwa watalipwa pesa kiasi kikubwa. Na hapo ninavyofikiriwa. Majambazi wakakubali kufanya hivyo.

“Zaidi ya hayo,” aliendelea Chifu, “hao majambazi hawajali kama wapigania uhuru wanashindwa ama wanashinda. Na wala hawaoni hatari za mbele kwa nchi zote za Bara la Afrika. Kweli, hao majambazi ninavyofikiria kuwa ndiyo wamefaulu.

“Sasa hapo ndipo sisi tunaingia katika habari hii. Na sasa sikiliza kwa makini. Wakuu wa Serikali wamekaa na kufikiri usiku huu huu na kuona watupe sisi kazi hii, na ni lazima tufaulu ama sivyo bara zima la Afrika litaumia si Tanzania wala Zambia wala Ethiopia wala Kenya zitakazoumia pekee. Wala si Msumbiji na Rhodesia na Angola peke yake. Kwa hiyo nimekuita wewe na utaondoka leo hii kwenda kwenye tume hii. Ninavyofikiria ni kwamba karatasi hizo hazijatoka katika Afrika Mashariki, maana Polisi katika nchi zote wameishafahamishwa na kuna ulinzi mkuu katika mipaka, viwanja vya ndege na mahali penginepo.

“Hao majambazi wanajua kwamba Serikali itachukua hatua kuzitafuta hizo karatasi kwa njia nzuri ama mbaya watajaribu kuwapa wanaohusika upesi iwezekanavyo. Lakini nadhani hawatazitoa mpaka wamepokea fedha yao. Lakini lazima ujue kuwa makundi ya majambazi yana akili sana wanangojea sisi tuanze kushughulika kusudi wajue kama kweli tunaweza kuwafikiria wao. Watakapoona kuwa tunawashutumu, mara moja na wao, wataanza kupambana nasi, maana hawatakubali kupoteza hiyo fedha. Hapo ndipo maisha yatakuwa magumu maana itakuwa ua au uawa. Na huenda wakasaidiwa na majasusi toka Ureno, Afrika Kusini na Rhodesia.

“Na pia nilifikilia kuwa, hao majambazi watapanga mahali pa kuonana na hao watu ili wabadilishane hivi vitu. Na lazima wapelelezi wa nchi hizi ndiyo watatumwa na Serikali zao kuja kuonana na hao majambazi. Hatari nyingine ni kuwa hao majambazi lazima wawe na majina ya wapelelezi wetu maarufu, na wewe ukiwa nambari moja kwenye orodha hiyo. Sasa ninafikiria kuwa ofisi kuu ya majambazi hao iko Nairobi. Kwa hiyo utaondoka hapa kwenda Nairobi, leo hii saa tatu unusu na ndege ya shirika la ndege la Afrika Mashariki.

“Vyeti vyote vya kusafiria viko tayari. Huenda itakubidi usafili mpaka Afrika Kusini au Ureno au Rhodesia ikiwa lazima. Mambo ya safari katika nchi hizo pia yako tayari. Ukiona ni lazima kusafiri katika nchi hizo usisite. Jina lako tangu sasa ni “Joe Masanja,” na kazi yako ni uandishi wa habari juu ya maonyesho ya mavazi. Maana tangu kesho maonyesho ya mavazi yataanza kote ulimwenguni. Upashanaji wote wa habari kati yetu katika kazi hii, utajulikana kama “Kufa na Kupona.” Na pia nakupa hiki cheti ambacho kimetolewa na Serikali, kikikuruhusu kuua kama ni

lazima. Nakutakia mafanikio mema. Mungu akusaidie ila nakuonya usihusiane sana na mwanamke, na katika hii safari usimwamini mwanamke yeyote.”

Chifu alimalizia kunieleza, lakini bado niliona mambo yote hayo ni kama muujiza. Kwani hakukuwa hata na chambo cha kuanzia. Ilikuwa kwamba nitaenda Nairobi bila hata kuwa na fununu ya mtu ambaye anaweza kuhusika habari yote niliona kama ya mwendawazimu. Kweli ilikuwa uendawazimu mtupu. Kisha nikamuomba Chifu kama angaliweza kuniruhusu kuuliza swali, naye akakubali.

“Kuna mtu yeyote ambaye anaweza kunisaidia huko Nairobi?” nilimuuliza

“Nitapata jina la huyo mtu mnamo saa mbili na nusu asubuhi hii, na kama pia kutakuwa na maelezo yoyote zaidi nitakupa wakati huu.”

Nilitoka ofisini kwa mkurugenzi wa upelelezi, na kufungua mlango. Nilimkuta Maselina amelala kwenye meza: Nikamgusa hakaamka. Akaniuliza ilikuwa ni saa ngapi. Nikamweleza ilikuwa saa kumi na mbili unusu. Akaniomba nimweleze kwa kirefu palikuwa na nini. Lakini sikuwa na muda, kwani ilikuwa inanibidi nijitayarishe upesi iwezekanavyo, nipate ondoka saa tatu.

Nilimweleza kwa kifupi tu mambo yalivyokuwa. Maselina akaniambia

“Willy, kweli safari hii mambo ni mengine, na kesi hii inaonekana imejisokota vibaya sana. Lakini naamini unaweza ukaisokotoa na kurudi salama Mungu awe nawe.”

Nakwambia kama mtoto huyu angalikuwa anakuaga wewe, walahi usingefanya safari, maana utadhani badala ya kukuombea usalama, anakuombea maafa! Maana hiyo sauti yake ilikuwa mno mbichi mbichi. Nilimwaga Maselina.

Nilitoka nje nikakuta kulikuwa kumeishapambazuka. Nikaingia katika gari langu, huyoo Upanga. Mitaani bado hakukuwa na watu maana kumbuka kuwa hii ni Jumapili. Nilipofika nyumbani kwangu nilimkuta Della bado amelala. Lakini baadae alipioniona tu, jambo la kwanza kuniuliza ni kama nitaondoka. “Naondoka mnamo saa mbili zijazo.”

Della alianza kulia, na huyo mtoto anapolia, ndipo anakuwa mzuri kiasi cha ajabu. Utadhani mwelekevu ambaye Shaaban Robert anamzungumza katika kitabu chake cha 'Adili na Nduguze. Kama hujakisoma miye Willy nakuomba ukakisome ndipo utajua Della ni msichana mzuri wa kiasi gani.

Nilimbembeleza Della na kumwambia, “Usijali sana. Safari si mbaya sana, na nitarudi muda si mrefu.” Lakini moyoni nilijua hii safari ilikuwa “HATARI TUPU!”

Della aliamka akaanza kutengeneza kahawa, wakati mimi nikifungasha vitu vyangu vya lazima. Muda mchache kijana mmoja alibisha hodi mlangoni. Nilipomuona nikafahamu kuwa alikuwa mfanyakazi ofisini kwetu. Daudi alikuwa ametumwa na Chifu kuniletea kamera moja ya gharama sana, ambayo ningetumia kama mwandishi wa habari na mchukua picha za maonyesho ya mavazi. Pia alibeba bastola mbili zote “automatic .45.” Visu sita na vitu vingine ambavyo ningeweza kuvitumia safarini.

Pia alinieleza kuwa Chifu alikuwa amekata shauri niende pamoja na ofisa mwingine wa upelelezi, kwa jina la Sammy Rashidi. Huyu kijana nawambieni nyie kuwa ni mwamba, maana katika kazi yetu hii kila siku ni nambari mbili akinifuata mimi. Na mara nyingi ameponyesha maisha yangu. Alishawahi kushinda mashindano ya kutupa visu katika mashindano ya Jumuiya ya Madola. Ukiwa na bastola na Sammy akiwa na visu, jua umekwisha kazi!

Kusikia Sammy anakwenda na mimi, Moyo wangu ulipata furaha kidogo. Daudi alinieleza kuwa Sammy atakwenda akitumia jina la Athumani Hassani. Kazi yake itakuwa msaidizi wangu katika mambo ya kuchukua picha, na yeye ndiye atakayekuwa mchukuaaji picha, na kwamba tutaonana naye kiwanja cha ndege cha hapa Dar es Salaam saa tatu.

Sasa ilikuwa saa moja na nusu, Della alikuwa tayari ameweka kahawa, mayai na mkate. Miye nilikuwa nimemaliza kufungasha vitu vyangu. Nilikuwa nangojea tu habari zaidi kutoka kwa Chifu. Tulikaa mezani na Della na kuanza kunywa kahawa. Nilizidi kumbembeleza Della, “Usijali sana juu ya safari yangu. Na kama mola akipenda tutaonana tena.”

Ilipofika saa mbili kamili, simu ilisikika. Nikaenda kuijibu, na kama ilivyotegemea, ilikuwa inatoka kwa Chifu. Chifu alisema, “Gamba sikiliza. Nairobi mtaonana na Ofisa mwingine wa Upelelezi aitwaye John Mlungu. Huyu ni kijana tunayemuamini sana. Nadhani mlishawahi kuonana. Yeye aliishafika Nairobi toka Kampala asubuhi hii. Atakungojea saa nne asubuhi katika Hoteli ya Fransae huko Nairobi. Inaonekana yeye anafununu kidogo kuhusu hii habari mpaka wakati huu. Maana anajua mambo mengi sana ya hapo Nairobi baada ya kufanya kazi hapo kwa siku nyingi akipambana na majambazi wa hapo kwa muda mrefu. Sasa tayarisha kila kitu uondoke. Nakuombea safari njema.”

Baada ya kupata habari zote hizi kwa Chifu nilionelea sasa niondoke kwenda zangu kwenye kiwanja cha ndege. Ilibidi Della anisindikize mpaka kwenye kiwanja ili apate kurudi na gari. Sikuwa na mzigo mkubwa sana, kwani huwa nina mfuko mmoja wa ngozi ambao nikiufunga unaonekana mdogo sana lakini ndani yake unaweza kubeba hata ngamia! Della alitia gari moto tukaondoka. Niliangalia nyuma kuiangalia nyumba yangu na sehemu ya Upanga kwa makini sana. Sijui ilikuwa mara ya mwisho kuiona ama nitaiona tena, huo ulikuwa ndiyo wasiwasi wangu.

Nilionelea nipite kwanza mtaa wa Nkurumah nikaone hilo jengo lililobomolewa, kwa sababu nilikuwa bado na dakika ishirini za kupoteza kabla sijafika kwenye kiwanja cha ndege. Na mwendo wa kutoka mjini mpaka kiwanja cha ndege. Ikiwa Della anaendesha ni dakik tano, kwani huyu msichana anafahamu kuvuta gari.

Nilipofika kwenye hilo jengo, nilimwacha Della ndani ya gari nikamwambia, “usitoke garini humu ila uwe ukiangalia ikiwa kuna mtu yeyote anayeonekana na wasiwasi wa kuiona hii gari hapa.”

Wakati huu watu wengi walikuwa wamekusanyika kwenye hilo jengo, kwa hiyo ilikuwa rahisi sana kuchunguza mambo fulani fulani bila mtu kuwa na wazo lolote juu yako. Polisi walikuwa wanasukumasukuma watu wasikaribie sana, hata mimi nilianza kusukumwa lakini polisi Inspekta mmoja alivyoniona alinichukua na kunionyesha kila kitu. Jambo moja nililifikiria ni kwamba hao watu waliobomoa hili jengo walikuwa wakifahamu kabisa kuwa hizo karatasi za siri zilikuwa kwenye hili kabati la chuma, maana la sivyo, wangelikuwa wamejaribu kupinduapindua na kutafuta tafuta kila mahali. Lakini vitu vyote hata wino katika vidau, haukuwa umemwagika japo tone moja hii inaonyesha kuwa walikuja moja kwa moja bila kugusa kitu kingine chochote, na kupiga kufuli la kabati kwa risasi na kuchukua karatasi na kwenda zao. Pia inaonekana haikuwachukua muda mrefu.

Hili jambo ambalo nimekueleza hapo juu, linanipa wazo. Na kama wewe pia ni mtu mwenye kufikiria kama miye Willy nadhani tayari umepata wazo ni kwamba hizi karatasi zilikuwa zikifahamika kwa watu wachache sana. Na kama hata zilijulikana kwa wapigania uhuru kuwa zipo, wachache walijua zipo wapi. Kwa hiyo ingawaje hao majambazi walijua zipo, wasingeweza kujua mahali gani zilipo, mpaka wameambiwa na mtu anayejua zaidi juu ya karatasi hizo. La sivyo wangelitafuta kila mahali kabla ya kuzipata. Hivyo tungalikuta vitu vimevurugwa vibaya sana. Kama una kichwa cha kufikiria nadhani umejua nina maana gani.

Baada ya kupata fununu fununu, na kufikiria mambo mawili matatu, niliondoka hapo mahali na kurudi kwenye gari ambamo Della alikuwa akiningojea. Della aliniambia, “Sikumuona mtu yeyote ambaye alionekana kuwa na wasiwasi juu ya gari hii. Ila tu niliona gari moja aina ya Dutsun 1600 SSS, dereva wake alikuwa amevaa shuka na miwani myeusi. Dereva huyo alinitupia macho kidogo tu.”

Nadhani hiyo habari ya Della inakupa wazo jingine kwani hilo gari ndilo lililokuwa likinifuata wakati nikienda ofisini kwa Chifu. Della alivuta gari moja kwa moja mpaka kiwanja cha ndege ambako tulimkuta Sammy akiningojea kwa hamu. Nilimuaaga Della kwa kumbusu kisha akarudi zake hali machozi yakimtoka.

SURA YA PILI

WASIWASI

Sammy alikuwa ameelezwa kwa kifupi na Chifu juu ya habari yote, hivyo aliomba nimweleze kwa urefu mambo yalivyo. Wakati wote huo hata Sammy, hakuwa akiona dalili yoyote ya kupata mwangaza wa jambo hili. Wote tulionekana vibuda.

Hapo uwanja wa ndege palikuwa na ukaguzi mkali sana. Lakini kwetu siye Chifu alikuwa amefanya mipango yote, kwa hiyo tulipita moja kwa moja mpaka kwenye ndege. Wakati huo nilikuwa bado najaribu kufikiri jambo hili na lile, kama naweza kutoa jambo kamili lakini wapi. Yule mtu mwenye shuka na miwani myeusi alikuwa akija kwenye mawazo yangu kila wakati. Mambo niliyofikiria kwenye lile jengo lililobomolewa pia yalikuwa yakinjia mara kwa mara. Nikamweleza Sammy kila fununu, au jambo lolote nililofikiria linaweza kutusaidia. Sammy naye akanipa mawazo yake.

Ilipofika saa tatu u nusu ndege iliondoka. Tuliiangalia Dar es Salaam kama kwamba hatutaiona tena. Hakuna aliyeamini ataiona tena. Wasafiri wenzetu walionekana kuwa wachovu wote kama sisi tulivyokuwa, kwani kama unavyojua ni Jumapili asubuhi. Mie nadhani ndiye niliyekuwa mchovu kushinda wote. Kwa hiyo nilimwambia Sammy awe macho wakati mimi nikijipumzisha kidogo maana katika kazi yetu hii huwezi kujua ni nani adui na nani rafiki. Wote ni maadui zetu mpaka tutakapohakikisha wenyewe mia kwa mia, ni nani rafiki yako. Na pia nilimweleza kama kukitokea kitu chochote ambacho atakishuku aniambie. Kwani nilijua mchana huo Nairobi kungekuwa na shughuli kubwa sana.

Sammy aliponiamsha niliona kuwa tulikuwa tayari tumefika kwenye kiwanja cha ndenge cha Embakasi. Tulitelemka kwenye ndege. Kisha tulitafuta gari la kukodi twende zetu mjini. Sammy alinunua gazeti la “Sunday Nation” aone kama kuna kitu chochote juu ya tukio hili lakini hakukuwa na lolote, ila mambo mengi juu ya maonyesho ya mavazi na mashindano ya muziki mjini Nairobi. Tulikuwa tumemweleza Chifu asiruhusu hili jambo kuchapishwa mpaka Jumatatu wakati tutakapokuwa tayari tumeanza kazi yetu huko Nairobi.

Tulitazama huko na huko ili tupate gari gani tukodi. Tangu tutoke kwenye ndenge ulikuwa umepita muda wa robo saa na ushee hivi. Nia ya kungojangoja hapo

kiwanjani ni kutaka kuona kama kuna watu wowote ambao walikuwa wanategemea kurejea kwetu, kwani siye kushuku kila mtu ndiyo kawaida yetu.

Tulipoona hakuna lolote, tulikodi gari moja la”Archers Tours.” Tukamweleza dereva atupeleke mpaka Embassy Hoteli, ambako nduko tulitegemea kulala. Lakini Sammy hakuonelea vizuri wote kukaa katika Hoteli moja kwa hiyo yeye alitaka tumtelemshe Hoteli Pigalle. Tulipanga tuonane mara moja Hoteli Fransae, kusudi tupate kuonana na John Mullunga, kama ilivyopangwa.

Mimi nilishuka Embassy Hoteli, nikaenda katika ofisi yao, ambako nilijiandikisha kama Joe Masanja. Halafu huyo binti ambaye ndiye karani hapo Hotelini akanipa cheti changu, funguo na nambari za chumba. Nikaingia chumbani. Kilikuwa chumba kizuri maana kilikuwa kwenye pembe ya nyumba. Kilikuwa na madirisha mawili. Dirisha moja kwenye upande wa mtaa wa Koinange na moja lilikuwa limezibwazibwa na nyumba zingine. Baada ya kuweka vitu vyangu nilitelemka mara moja kwenda zangu Hotelini Fransae. Nilipopita pale ofisini, nikamweleza mshughulikaji wa simu kuwa kukija simu yangu achukue hiyo habari. Halafu nikampa shilingi ishirini. Akanitazama kwa macho ya kusema asante mara mia. Kwani tarehe ishirini kwenye jiji kama Nairobi, ni mwambo mbaya sana.

Kisha nikaharakisha kwenda zangu Fransae. Nilipofika mlangoni, nilimuona Sammy naye anamaliza kuingia. Nilimuona John amekaa kwenye pembe ya mlango upande wa kushoto kama ukiwa unaingia tu hotelini. Sammy alikuwa hamjui John, kwa hiyo yeye alikuwa bado anaendelea kwenye kaunta ya hoteli. Nilipoingia nilimpigia mluzi akageuka tukamfuata John pale pembeni. Tumewahi kufanya kazi na John huko Kampala, wakati tulipotumwa kuwatafuta waibaji almasi. Na ninakwambia wewe msomaji John kusema kweli si mchezo. Katika kila kesi wanayomweka John hawa watu wa Uganda jua kuna makubwa. John alikuwa amekaa na kijana mwingine mwenye sura ya kupendeza sana. Nafikiri John alimfanya rafiki yake kusudi huyo kijana awe anamtengenezea mpango kwa ndasa, kwani alidhani kuna msichana yeyote ambaye asingesimama kama huyo rafiki wa John akimpigia mluzi.

Tulipofika hapo John alitukaribisha tukae. Kisha akatufahamisha kwa rafiki yake ambaye anaitwa Robin Mwangi, Kikazi akiwa ofisa wa usalama nchini Kenya. Nayo Serikali ya Kenya ilikuwa imemleta Robin kwenye kazi hii. Mimi nilijifahamisha kama Joe Masanja, na Sammy kama Athumani Hassani. Na mikamfahamisha John kwa Sammy kama Fred Kamau. John tayari alikuwa amepata habari zote za kuja kwetu, na jinsi ambavyo Chifu alivyomweleza kama

angeweza kumtambua Sammy, kwa kule kuwa na kamera shingoni. Wote tayari tulikuwa tumeshaelezana majina ambayo tutatumia. John alituagizia vinywaji. Aliagizia “Marteli Cognac” toti nane, pamoja na soda kwenye barafu.

Wakati tukinywa, John alitueleza, “Hapa tulipo si mahali pazuri sana kwa kuelezana habari, kwa maana watu wengi huwa wanakuja kuzimua hapa hotelini saa kama hizi, siku za Jumapili. Hata hivyo nitawatolea muhtasari wa habari niliyokwishapata,” Alinyamaza, kisha akaanza kusema, “Joe kusema kweli tukio hili linatisha kuzidi matukio yote, kwani inaonekana wote tuko gizani kabisa. Miye nilidhani nitapata jambo lolote la maana lakini wapi. Robin nilimweleza mnamo saa moja aweke vijana wake mahali fulani kusudi huenda wakaweza kutupatia maelezo yoyote ama kama wanaweza kupata fununu yoyote. Lakini ajabu ni kwamba vijana wanne wameisha uawa katika muda huu wa saa mbili. Hii inaonyesha tutakuwa na muda mgumu sana, tena sana.

“Mmoja alikuwa amepigwa risasi huko Embakasi. Mwingine ametiwa kisu huko “Uhuru Park”. Wengine wawili walikutwa wameuawa huko Lavington Green kwa risasi. Sasa hata hatuwezi kuunganisha vifo hivi, ila tu kwamba watu hawa wako kila mahali. Na linaonekana kuwa kundi kubwa sana. Lakini jambo kubwa ni kwamba lazima tufanye kichwa cha tukio hilo.

“Mkurugenzi wa Idara ya Upelelezi wa kwenu amenieleza kwa simu anavofikiria. Nami ninakubaliana naye, kwani huyu mzee akibashiri kitu, naamini ni hivyo. Kwa hiyo sisi itatubidi tuendele kama alivyofikiri, la sivyo tumekwisha”.

Bado mimi nilikuwa sijaweza kuunganisha jambo lolote. Ilikuwa bado ajabu. Ajabu kubwa. Hapo nilimwuliza John, “Unafikiri, sasa tutaanzia wapi?”

“Mimi nafikiri tutaonana usiku huko Starlight Klabu maana, yule kijana aliyekutwa Uhuru Park, alikuwa sehemu hizo. Na miye nilipochunguza sana ilionekana kama kwamba huyu mtu aliuawa katika nyumba fulani halafu akatupwa Uhuru Park. Kama unavyojua leo ni Jumapili watu wengi walikuwa bado wamelala.

Baada ya kukaguakagua afisa mmoja wa polisi alisema aliona tone la damu kwenye mlango wa Klabu hiyo. Nikaonelea vizuri nimwambie Mkurugenzi wa Usalama wa hapa amueleze Mkuu wa Polisi. Niliwataka wasiulize jambo lolote, au wasiulize maswali yoyote juu ya vifo hivyo mpaka baadaye. Kwa hiyo sasa tutatawanyika halafu tutaonana usiku huko Klabu. Wakati huu Robin na mimi

tutaendelea kukusanya habari chache chache toka kwa maafisa wake. Nendeni mkapumzike.

Tuliagana na Robin akanieleza, “Kama ukitaka msaada wowote wa watu waweza kupiga ripoti ofisini kwetu, Chifu huko Dar es Salaam tayari amefanya kila mpango na wakubwa wa usalama katika nchi zote tatu za Afrika ya Mashariki.”

Tulikubaliana kuwa wote tutaonana Starlight Klabu mnamo saa tatu usiku. Sammy alienda hotelini kwake, nami nikarudi hotelini kwangu kupumzika kidogo.

Nilipoingia hotelini kwangu nikaenda mpaka kwa mshughulikaji na simu kumwuliza kama amepata simu yoyote. Naye akasema kwamba alikuwa bado hajapata. Nilienda moja kwa moja kitandani kwangu nikalale.

Nilipoamka ilikuwa saa kumi na mbili za jioni. Nilioga na kunyoa ndevu. Halafu nikajitayarisha kwa kila njia ili niweze kuonekana kama mwandishi kweli kweli. Halafu nikaagiza chakula. Sikula chakula kizito sababu hali yangu haikuwa nzuri sana. Baada ya kula nilimpigia simu Sammy anipitie mnamo saa mbili na nusu.

Ilipofika saa mbili na nusu Sammy alinikuta baa ya Fransae. Tukafunga safari kwenda Starlight. Mimi nilitaka tuchukue taxi, lakini Sammy alikataa, kwa kusema, “Twende kwa mguu, maana tunaweza tukapata jambo la kufurahisha. Pia ni lazima uchukue bastola yako, maana kunaweza kuwa na mambo ya hatari.”

Nilirudi chumbani kwangu, nikaweka bastola yangu ndani ya mkoba wake wa begani. Nikaweka koti langu juu nikafunga tai sababu mwezi wa saba, ni baridi sana Nairobi. Ninge kuwa sehemu za Dar es salaam, wakati huo ninge kuwa ninavaa furana. Kweli nilipojiona kwenye kioo nilionekana mwungwana. Na ninakwambia ninapokuwa nimevaa koti, huwezi kujua kuwa hata siku moja nimewahi kugusa bunduki. Nilirudi huko, baa kumpitia Sammy ili twende zetu.

Tulienda na mtaa wa Koinange, halafu tulipofika New Avenue Hoteli, tukashika Kenyatta Avenue. Tuliendelea na Kenyatta Avenue mpaka tuliposhika Uhuru Highway, tulikoingia katika kijinjia kinachopitia Uhuru Park. Tuliangaza huku na huko katika Uhuru Park lakini ilionekana hapakuwa na watu. Nadhani watu walikuwa wameishasikia kifo cha huyo kijana. Pia tulitegemea kuwa kama watu hao wamekuwa wakifuata myenendo yetu, huenda wakawa wanatufuata. Hivyo Sammy akawa tayari tayari na visu vyake ikiwa kutatokea matata. Lakini hatukupata jambo lolote.

Tulipoachana na Uhuru Park, tulishika Kirk Road. Tukaenda zetu moja kwa moja mpaka Starlight. Nje ya Klabu hiyo tulikuta watu wengi wakikata tikiti. Wanawake walikuwa wengi sana hapo nje, na walionekana wakitafuta wanaume wa kuwaingiza ndani. Lakini sisi tulikata shauri tusiwajali maana wangeweza kuingilia kazi yetu. Nilienda nikakata tikiti halafu tukaingia ndani.

Hii Starlight Klabu inapendeza mno maana hali ya hewa ya humo ndani ni tulivu kabisa. Kila mtu alionekana ni Mwingwana. Watu wengi walikuwa wameishaingia. Wengi wao walikuwa wawili wawili, yaani” Kitu Mtu.” Nadhani unanielewa ninaposema hivyo. Tulienda tukakaa kwenye pembe moja ya kulia karibu na mlango mkubwa wa kuingilia. John alikuwa bado hajafika. Tulishangaa sana, lakini tulijua tu ya kwamba atafika muda si mrefu. Punde si punde Robin alifika. Na mara alipotuona akatufuata.

Robin aliuliza, “Fred yuko wapi?”

“Hata siye bado hatujamuona. Tulidhani mngelika wote hapa, “alijibu.

“Hata, aliniambia kuwa yeye atakuwa hapa mnamo saa mbili u nusu, kama ni hivyo basi huenda yuko kwenye ile baa ya nje, au amepata habari fulani ambayo anaishughulikia.”

Kisha Robin aliondoka akaenda kwenye baa ya nje kuchunguza kama Fred yuko huko. Aliporudi alitueleza kwamba Fred hakuweko. Sammy aliagiza vinywaji. Muziki nao ulianza kupigwa na vijana wa Fiesta Matata ambao hupiga muziki taratibu kabisa. Wakati huo wote tulikuwa tukimngojea Fred lakini hakuonekana. Tulianza kupatwa na wasiwasi mwingi sana. “Kwani Fred anaishi wapi?” Sammy alimwuliza Robin.

“Anaishi Princess Hoteli.”

“Afadhali nikampigie simu huenda anaumwa,” nilisema

“Sammy uwe unaangalia kama yuko mtu mwenye shauku na mimi nipigapo simu.”

Nilipopiga simu hotelini kwa Fred ilionekana hayuko kwani kengele iliendelea kulia kwa muda mrefu sana. Nilikata simu na kurudi pale kwa akina Sammy. Niliporudi Sammy alinieleza, “Ulipokuwa ukienda msichana mmoja ambaye alikuwa amevaa mini alikuwa akikuangalia kwa jicho la pembeni pembeni. Msichana huyo alikuwa akicheza dansi na kijana fulani. Halafu alipokuona ukienda kwenye simu alisogea mpaka kwenye kiti cha karibu na simu, kisha

akajifanya kuwa anasoma gazeti. Na baadaye msichana huyo akapotea mumu humu mwenye watu.”

Hilo jambo niliona huenda ni hatua moja wapo. Lakini hatua hii ilikuwa bado haina uhusiano wowote na tukio letu. huenda ni kwa sababu ameona ajabu kwa nini tulipiga simu, na kwamba tulikuwa tumekaa tu bila wanawake na hali tunaonekana vijana nadhifu mno.

“Habari zenu,” sauti nyororo ilitoka kwa nyuma yetu. Kila mtu kati yetu alipatwa na kigugumizi cha kujibu, kwani wote tulipotupa macho nyuma yetu, tulimwona msichana mzuri mmno!

Nakwambia maishani mwangu nimeona wasichana, lakini ilivyo ni kuwa huyu msichana alishinda. Nilisikia nywele zikinisimama nilipomwangalia tena. Nilijikaza kisabuni nikamjibu, “Siye wazima tu, vipi wewe?”

“Miye salama tu. Nilidhani kuwa huenda nyiye ni wageni hapa. Na kwamba huenda mlipofika hapa mlifanya mpango na wasichana fulani fulani mwonane nao, lakini hawajaonekana, si hivyo?”

“Kidogo huenda uko sawa, lakini si sana,” nilimjibu.

“Mbona unaonekana mwenye wasiwasi basi? Nilidhani kwamba ulienda kupiga simu kwa madhumuni ya hao wasichana.” Akanyamaza hali akinitazama machoni.

Kweli mimi nakwambia sitaki wasichana wanaonitazama machoni. Kwa hivyo msichana huyu mara moja alinitisha. Macho yake yalionekana kusinziaritia, lakini yanaweza kukusoma moyoni mwako.

“Nilikuwa napiga simu kwa rafiki yangu mmoja ambaye ni mwandishi juu ya mambo ya muziki. Yeye tulimwacha Acadia Klabu. Nilitaka kumweleza aje huku kwani, muziki wa hapa unaonyesha umeshinda. Lakini inaonekana kuwa muziki wa huko umewaingia sana hata hawasikii mlio wa simu,” niliongopa.

Alitabasamu. Tabasamu hilo lilifanya nywele zangu zisimame tena.

“Kweli nimeupenda muziki wa hapa,” alisema msichana huyo. “Hata mimi huwa napenda bendi hii hii, na mahali papa hapa.”

“Jina lako nani, “aliulizwa na Sammy.

“Mimi naitwa Lulu. Lulu Jack, kazi yangu ni kuonyesha mavazi. Nimetoka Kampala kuja kwenye maonyesho ya mavazi hapa Nairobi ambayo yatachukua kama wiki mbili hivi.” Alinyamaza kwa muda wa kupisha mate yapite kooni. Kisha akauliza,” Na nyiye ni akina nani?”

“Miye ni Athumani Hassani, na huyu,” alisema Sammy akionyesha kidole kwangu,” ni Joe Masanja. Na huyo ni Robin Mwangi. Kazi yetu sisi ni uandishi wa habari juu ya maonyesho ya mavazi. Hata sisi tumeletwa na yaya haya maonyesho ya mavazi. Hivyo inaonyesha tutaonana mara nyingi toka sasa. Naamini nitakuwa mtu mwenye furaha sana nitakapokuwa nakuchukua picha. Maana mimi ndiye mchukuaji picha katika kundi letu hili.”

“Nitafurahi sana kuzidi kuonana na nyinyi kwani mnaonekana kuwa watu waungwana sana. je, mnatoka wapi?” Aliuliza.

“Siye tunatoka mjini Mwanza, Tanzania,” alijibu Sammy. Kisha Lulu alituaga akaondoka kwenda kucheza dansi. Mimi huwa siwaamini wasichana wazuri kama hawa. Nakumbuka siku moja mama yangu, Mama-Willy, alinieleza kuwa kati ya wanawake wote, ukiona mwanamke mzuri sana jua mwanamke kama huyo ni hatari sana. Na nilipoanza kazi kila siku ninapotumwa kwenye shughuli fulani jambo la kwanza la Chifu ni kunisihi nisifuate wanawake wazuri sana. Maana wanawake kama hao ni sumu kali sana. Lakini mimi Willy, ingawaje nakubaliana na Mama Willy pamoja na Chifu, nimekuja kutambua kutokana na kazi zangu kuwa, kutokana na mwanamke mzuri sana unaweza kupata habari za ajabu sana. Nilikata shauri kuwa sitamwachia Lulu vivi hivi lazima nitafute mengi ya maisha yake.

Huyo mtoto Lulu ni Lulu kweli kweli. Kwani toka kwenye dole gumba mpaka utosini hana dosari yoyote. Ukimwona hutaamini kuwa alizaliwa na mwanadamu ila labda mtoto wa jini, kama unaamini kuwa kuna majini, ama amefyatuliwa kutoka katika mashine baada ya kuchongwa na mchongaji nambari moja hapa ulimwenguni. Nakwambia kama Lulu ataacha wazi sehemu ya kifua chake halafu umtazame, utababaika. Hutaweza kumwangukia mwanamke mwingine yeyote. Utawahesabu wanawake wengine kama wanaume tu. Kama Mungu amewahi kupendelea, basi huyu Lulu amempendelea hasa.

“Sammy,” niliita, “angalia kila mtu anayehusiana na Lulu katika hii klabu. Nawe Robin pata watu wa kumfuatia Lulu ili tupate kujua anakaa wapi.” Nilinyamaza kidogo kisha nikaendelea, “Mimi itanibidi niende kule hotelini kwa Fred nikajue kuna nini, maana mpaka sasa yapata saa nne na nusu na bado hajaonekana.

Ninawaacheni wote hapa ili kuangalia mambo ya hapa klabu. Lakini Sammy unipigie simu kama ukiona nimechukua muda mrefu, zaidi ya dakika arobaini na tano. Na upige kule kule chumbani kwa John. Kwaherini.” Nikaondoka.

Nilikodisha gari nje na kwenda moja kwa moja mpaka Ambassador Hoteli. Sikutaka anitelemshe hapo Princess Hoteli. Niliposhuka hapo, ilinibidi nichukue Government Road nionekane kama kwamba nataka kuchukua 'bus' kwenye kituo cha 'mabus' cha Ambassador. Nilikwenda nikazungukia mtaa wa Duke, halafu nikaingia katika mtaa wa Tom Mboya.

Nilipoingia Princess nikakuta watu wengi sana katika baa. Nikajifanya kama miye pia mpangaji wa hapo lakini nilitazama huku na huko hapo hotelini ili nione kama kuna mtu ananichunguza. Lakini watu wote walionekana wakishughulika na unywaji wa pombe na kadhalika. Nilipanda ngazi mpaka ghorofa ya kwanza, Robin alikuwa amenipa nambari za chumba ambamo John alikuwa akilala. Nilikwenda mpaka kwenye hicho chumba. Kabla sijagonga nilikagua vyumba viwili vilivyokuwa upande wa kuume na kushoto wa hicho chumba. Lakini sikuona wa kusikia chochote. Ilionekana hivyo vyumba havikuwa na watu, au wote walikuwa wamekwenda kutembea.

Niligonga kwenye mlango wa John lakini sikusikia lolote. Nikafikiria kutoka, lakini nikaona afadhali niingie ndani pengine nitaweza kupata habari zozote. Ama huenda akawa ameacha habari fulani fulani. Nilichukua funguo zangu malaya ili nifungue mlango kwani ulikuwa umefungwa.

Nakwambia sijawahi kushituka kama nilivyoshitushwa na hali niliyoikuta humo chumbani nilipowasha taa. Hofu iliniingia, nikaanza kugwaya. John alikuwa amelala kifudifudi. Amekufa! Fahamu zilinitoka kwa muda wa dakika tano hivi. Baada ya kuzinduka nikaenda karibu na maiti ya John ili niichunguze vizuri. Niliona kuwa alikuwa amepigwa risasi sita, zote kifuani.

Ilionekana kuwa huyo aliyempiga hizo risasi, bastola yake ilikuwa .45. Kwani miye nimewahi kuona matundu ya risasi hizi. Haya mauaji yalikuwa ya kutisha sana. Yalikuwa mauaji ya kikatili sana, maana aliyemwua alimwachia risasi nyingi kana kwamba alimwua ng'ombe. Na ilionekana kwamba waliingia kwa ghafla, kiasi ambacho hata John hakuweza kujitetea.

Kifo hicho cha John kiliniuma sana hata nikaapa kuwa huyo aliyemwua, lazima nimkamate na kumwua mimi mwenyewe, kama nitakuwa mzima wakati wote wa madhila kama hayo. Woga ulianza kuniingia kwa mara ya kwanza. Tangu nianze

kazi hii sijapatwa na woga kama huo. Kitu kilichofanya nitishike sana ni jinsi wauaji hao walivyomfahamu John. Na kama ni hivyo, basi hata sisi tutakuwa tumeisha fahamika. Na kama wameweza kumwua John ambaye ni mpelelezi mashuhuri katika Afrika ya Mashariki, lazima watu hawa wawe miamba kweli. Na lazima wawe ni wenye akili nyingi sana juu ya kuwinda watu.

Kweli tulikuwa tunanuka vifo siye sote. Hazijapita hata saa ishirini na nne, watu watano tayari wameishakufa! Hata kama ungekuwa na moyo mgumu kama wa Farao, hata wewe ungeweza kutishika.

Nilikata shauri, kuufunga mlango na kuiacha hiyo maiti halafu niende kuwapigia simu polisi. Lakini kabla sijatoka niliona heri nipekuepekue mifuko ya John ili huenda nikapata kitu chochote kilichofanya hata wamfuate. Na kama unafikiri sana unaweza kuona kuwa lazima John, wakati sisi tunashangaashangaa yeye alikuwa amegundua jambo fulani ambalo ndilo lililosababisha kifo chake. Kisha nilienda mpaka kitandani ambako kulikuwa na mkoba. Nilipoinama tu, nikasiki sauti ikiniambia, ”Tafadhali kaa ulivyo wala usisogee hata inchi moja. La sivyo utapata idadi ya risasi zile zile zilizomwingia huyo mshenzi karibu nawe hapo.”

Nikaduwaa....!

SURA YA TATU

NILIJIONA siwezi kufanya lolote. Na kama kweli ningefanya upuzi hapo, nilijua hata mimi ningeyala marisasi. Kwa hiyo nilionelea ninyamaze tu mpaka hapo nitakapopatiwa yangu. Jinsi huyu mtu alivyoingia hata sifahamu maana aliingia kama mchawi bila hata kishindo. Zaidi nilikuwa nataka nimwone ni nani, lakini niliona kwamba ningegeuka uso tu, ningekwisha kazi. Nilijua hata mimi huo ndio mwisho wangu. Mara nyingi huwa katika hatari kama hizi, lakini kwa mwujiza wa Mungu hutokea nikaponyoka. Mara hii mambo yalionekana kuwa tofauti kwani watu hao hawakuweza kufanya kosa hata moja.

“Wewe ni nani, na unafanya nini hapa?” Niliulizwa.

“Mimi naitwa Joe Masanja, na nimekuja hapa kumtazama huyu Fred Kamau ambaye ni mwandishi mwenzangu. Sote tunaandika habari juu ya maonyesho ya mavazi ambayo yameanza hapa. Na nimestaajabu sana kumkuta ameuawa.” Nilinyamaza kisha nikasema kwa upole mwingi, “Lakini mbona unanijia kijeshi namna hii, kama kwamba miye nimefanya jambo lolote? Ninashangaa kujiona nimeshikiliwa bunduki mgongoni. Ninaweza kuzimia hivi. Na wewe ni nani? Niliuliza.

“Nyamaza,” alijibu “sina muda wa kujibu maswali yako, nimo kazini. Ila nataka kujua uliingiaje humu! Mlango ulikuwa umefungwa. Na kwa nini baada ya kuingia humu ukaonekana kuchunguzachunguza vyumba vilivyo karibu na hiki, kama kwamba ulikuwa ukijua kwamba ulikuwa unafuatwa?”

“Nilifungua mlango kwa kutumia ufunguo niliopewa na huyu rafiki yangu Fred, maana alikuwa na funguo mbili. Nilikuwa nimesahau nambari ya chumba ndiyo sababu ilinibidi nithibitishe ni kipi kati ya hivi vitatu,” nilimjibu. Wakati huo zilikuwa zimepita dakika arobaini na saba, na simu ilikuwa bado haijalialia. Hivyo nilizidi kukabiliwa na wasiwasi.

“Wewe ni mwongo - mwongo nambari moja. Hii inaonyesha unafahamu mambo mengi kuliko hivyo unavyotaka kusema. Huyu si Fred ila ni afisa wa upelelezi aitwaye John Mullunga,” alijibu kwa sauti ya hasira. “Na siye tulikuwa tunajua kwamba atakuja mtu wa aina yake kuangalia. Na wewe lazima ni mmoja wao, ila tu unajidai ni mwandishi. Hivyo lazima na wewe ufe kusudi tuweze kuendelea na mipango yetu.”

“Hayo ni maneno yako wala si yangu. Na hata kama ukiniua, siku moja nawe utakamatwa. Miye sikuwa nikijua kuwa huyo ndiye John Mullunga. Na wewe tu ndiye umeniambia maneno haya. Na kama huyu kweli ndiye John Mullunga ambaye nimesikia habari zake, na nyiye mmemwua, basi serikali ikifahamu, itawawinda mpaka watawatia vitanzi.” Nilimueleza.

Wakati wote huu nilikuwa nasema kusudi dakika zizidi kwenda ili pengine baadaye nipate mkombozi. Alianza tena kunitisha, “Maiti huwa hazielezi habari. Sitakusikiliza kwa maana wewe ni maiti tayari.” Alianza kucheka kisha akaniambia,”Toa sala zako za mwisho. Na kama wewe pia ni afisa wa upelelezi, serikali itatukoma, maana hizi serikali bado hazitutambui. Na 'bosi' wangu nadhani atafurahi sana kusikia John amekufa na kijishenzi kingine.”

Wakati huu wote nilikuwa nafikiri namna ya kuweza kujiponyesha. Lakini niliona hakuna. Bastola yangu nilikuwa nayo kwapani lakini nilijua nikijitingisha kidogo tu nitaingia kuzimu! Kwa hasira na uchungu nikasema, “Niue basi sasa unafanya nini? Unapoteza muda wako.”

“Fumba macho, usali kwa dini yako, ama vyovyote.”

“Naomba nipige magoti basi.” nilisema.

Alicheka akasema, “Lo! Nadhani polisi watakaokuja humu watapata tishio, kwani watakukuta wewe umekula risasi sita hali umepiga magoti kitandani unasali. Halafu wataona rafiki yako amelala kifudifudi hapo chini, akiwa kama anaomba msamaha. Naye pia amekula risasi zipatazo sita.” Sauti ya huyu mtu ilinionesha kuwa ni mwuaji, na ni mtu ambaye anafurahia kuua. Pia alionyesha kuwa mtu katili na jambazi.

Nilikuwa wakati wote huu nikifikiria njia ya kujiokoa. Na kule kuomba nipige magoti, ni jaribu la kwanza kama huyo mtu akikubali tu nimtengeneze mara moja. Nikajifanya kuwa nilikuwa natetemeka ovyo. Bastola yake ilikuwa nusu inchi kutoka kwenye mgongo wangu. Nikabaki katika kufikiria jinsi ya kuirusha. Nilijua kuwa mtu huyo alikuwa mwuaji na hatanihurumia.

Mama-Willy alinishauri siku moja kwa kusema. “Mwanangu kama umo hatarini, usife kama kondoo, kufa kama mwanaume ambaye wakati wa kuzaliwa mama yake alishikwa na uchungu wa ajabu.”

Tangu siku hiyo sikukubali kufa kikondoo. Basi niliposogea kwenye kitanda, hili jambazi lilipitisha mkono kwenye koti langu. Likatafutatafuta na kukuta bastola

yangu ambayo aliichukua. Halafu likacheka. “Yee, eti wewe ni mwandishi. Mwandishi gani anatembea na bastola, automatic '45' katika Afrika ya Mashariki? Mawili, wewe ni jambazi ama afisa wa upelelezi.”

Wakati huo akizungumza nilijua nimeishapatikana. Nukta yoyote ningeweza kula risasi. Na kicheko alichocheka kilikuwa cha hasira. Nilisikia akiitupa bastola yangu upande mwingine wa chumba. “Upesi piga magoti. Huwezi kunidanganya mimi ati ni mwandishi. Ingekuwa Marekani ningelikubali, lakini Afrika ya Mashariki usinitanie.”

Wakati ninapiga magoti na huku najifanya kama kwamba natetemeka, nilitupa shoto langu kama umeme. Kufumba na kufumbua, bastola ya hilo jambazi iliruka na kwenda kwenye pembe moja ya chumba. Hapo hapo nikamgeukia. Akanitupia ngumi moja, nikaikwepa. Nikatupa shoto langu tena likampata kwenye taya mpaka chini. Ilivyo ni kwamba shoto langu likikupata, ukiwa dhaifu hutaamka tena hadi siku Yesu atakapokuja kwa mara ya pili!

Niliruka mpaka alipo, lakini akanipiga kwa mguu tumboni. Nikaenda kuangukia kitanda! Wakati huo alikuwa ameisha simama. Akanijia wakati nikijaribu kusimama. Akanitia ngumi shingoni na kujikuta niko chini! Halafu akanitia teke la usoni na kuikimbilia hiyo bastola. Kabla hajafika niliruka kama swala na kumchukua 'judo' mpaka kitandani. Katika maisha yangu ya miaka sita katika kazi hii sijaonana na mtu kama huyu. Kweli siku hii, lo, maisha yaliniwia magumu.

Kabla hajasimama nikamtia ngumi nyingine kwa mkono wangu wa kulia. Na hapo nikaona amedhoofika. nikaondoka kukimbilia bastola. Kabla sijafika nilipata teke la mgongoni na kunifanya nipepesuke. Kabla hajashika hiyo bastola nilimpa tena shoto langu mpaka akaanguka chini. Nilimfuata hapo chini na kumtia teke la tumboni, na jingine ubavuni. Maana majitu kama haya, ukijigamba kuyapiga kichwani tu utacheka. Yanavyo vichwa vigumu kama paka.

Alipodhoofika kabisa niliendea bastola. Kurudi nikakuta amezimia. Ilikuwa yapata saa tano na robo za usiku sasa. Niliendea chupa ya “whisky” iliyokuwa humu chumbani na kuanza kummwagia na kumnywesha kidogo kidogo. Kisha akaanza kuzindukana. Hapo nikashikilia bastola yangu kwenye taya lake.

“Niambie wewe ni nani, la sivyo utameza risasi zote hizi zilizomo katika hii bastola,” nilimwambia.

“Yeeh, sitaweza kusema hata ufanye nini na afadhali uniue tu,” alijibu.

“Sasa kama hutaki kusema jina lako huyu uliyemuita 'bosi' wako ni nani?”

Hakujibu alinyamaza tu. Nikaona nisipokuwa katili hapo sitaweza kupata fununu yoyote. Niliwasha kiberiti changu. “Usiponielea jina lako nitakuchoma masikio yako ingawa unaonekana kuwa hujali.”

Basi nilisogeza moto kwenye sikio lake nikaanza kumchoma. Kwanza alijifanya hajali ingawaje alionyesha kuhisi uchungu wa ajabu. Hii ilinionyesha kuwa yeyote yule ambaye anaitwa 'bosi' wa watu hawa lazima anajua kuchagua watu wake. Kwani kweli ni wanaume. Ni watu wachache sana wanaoweza kuvumilia moto. Lakini maumivu yalipozidi alianza kuguna halafu akaanza kulia.

Mwishowe alisema, “Acha, niachie, nihurumie. Ngoja nitakwambia, hebu niache.”

Nilitoa moto penye sikio lake kumpa nafasi aseme.

“Mimi naitwa....”

Kabla hajasema jina lake alipigwa risasi toka dirishani. Akafa! Niligeuka kutazama aliyemwua, lakini sikuona mtu. Na wala sauti ya bastola au bunduki iliyomwua sikuisikia. Hii ilionyesha kuwa bastola zao zote zina viwambo vya kunyamazisha sauti, ambavyo huitwa “sailensa.”

Kupigwa risasi kwa mtu huyo kulinipa wasiwasi zaidi. Moyo ulipiga mara nyingi mno. Chuki ilinijia maana hawa watu wanaonekana kuwa wameipanga mipango yao kiasi cha kwamba wanahakikisha hawafanyi makosa, hata chembe ya kosa. Nilikata shauri nitoke hapo mahali. Niliangalia zile maiti kwa mara ya mwisho. Nikaamua kwenda kuuchunguza ule mfuko wa John kabla sijaondoka. Lakini kabla sijafika kwenye huo mfuko, nilisikia sauti ikisema, “Simama hapo hapo ulipo, na usijitingishe.”

Moyo uliniuma na hofu ilinizidi kwani niliona mara hii hawatafanya makosa kama mara ile.

“Angusha chini bastola yako,” mtu huyo nisiyemtambua alisema kwa sauti ya hasira.

“Geuka unitazame.”

Niligeuka upande wake na huku nimeinua mikono juu. Huyo mtu alionekana katili zaidi ya yule mwingine. Alikuwa kijana mwenye sura mbaya mbaya. Mweusi na mwenye umri upatao miaka ishirini na minane. Kwa umri tulikuwa tukilingana.

Mimi pia nilikuwa nina umri wa miaka ishirini na minane. Na kuadhimisha sikukuu yangu ya kuzaliwa ilikuwa wiki moja toka siku hiyo. Nilimwacha Della akialika watu kwenye hiyo sikukuu yangu. Lakini huenda badala ya kuadhimisha sikukuu yangu ya kuzaliwa, watakuwa wakiadhimisha matanga yangu, siku hiyo. Maana sasa kila dakika ilinuka kifo kitupu.

“Mara hii hatutafanya makosa. Huyu mshenzi waahedi hapo chini, alifanya makosa na ndiyo sababu na yeye amepata zawadi yake. Wewe ni nani? Maana unaonekana kuwa tisho kwetu zaidi ya wengine wote. Hakuna aliyewahi kupambana na Kasha akabaki mzima. Hebu nipe maelezo kwa kifupi. Maana utake usitake utakufa tu. Huwa sifanyi makosa mimi.”

Nilipomtazama alionekana kuwa mtu ambaye hawezi kufanya makosa. Niliomba Mungu kimoyomoyo na kuanza kutubu makosa yangu.

“Mimi naitwa Joe Masanja. Na ni mwandishi wa habari juu ya 'Maonyesho ya Mavazi,' Nimetoka Mwanza. Tanzania,” nilisema.

“Pumbavu wee, unadhani unaweza kunidanganya mimi, mwandishi hawezi kuwa jasiri kama wewe hata kuweza kumshinda nguvu Kasha,” alisema, kisha akanipiga kofi moja mpaka nikaona jua, ingawaje ilikuwa usiku. Fahamu zikaniruka kwa muda. Ziliporudi nilikuta bado ameshikilia bastola yake na kuniuliza tena mimi nilikuwa nani. Nilimjibu vile vile, “Oke, oke, mimi sitajali kama kesho nitakuona ukila chakula cha mchwa,” alisema kwa kiburi sana.

Nilifumba macho maana niliona ndio mwisho wa maisha yangu. Hapo sikuwa na ujanja wowote. Kwani huyu kijana anavyoshikilia bastola, afadhali naye yule, mchezaji wa sinema wa kule Mexico, “Cowboy Cuchilo.”

Wakati nilipoona anakaza mkono wake kuachia risasi, kufumba na kufumbua nilishtukia anaanguka chini. Alikuwa amepigwa risasi! Taratibu akakata roho! Niliruka mara moja kuchukua bastola yangu tayari kwa matata mengine yoyote. Mlango ulipofunguliwa nilikuta ni Sammy.

Kwa mara nyingine tena Sammy alikuwa ameponyesha maisha yangu, la sivyo dakika hii ninge kuwa mfu.

“Willy - naona walikuwa wamekusakama sana. Sasa, tukimbie tutoke hapa ili ukanieleze jinsi mambo yalivyokuwa, alininong'oneza Sammy.

Kulikuwa na maiti tatu hapo chumbani sasa. Kabla sijatoka hapo chumbani nilienda kwenye mkoba na kuanza kukagua kagua. Nikaona hamna la kutusaidia. Tulipitia dirishani na kutelemkia kwenye ukuta na kutokea kwenye kijinjia.

Tulikimbia toka hapo mpaka River Road.

“Nilipiga simu baada ya dakika arobaini na tano kama ulivyosema,” alisema Sammy,” Simu ilionekana kuwa ilikuwa imekatwa, kwa hiyo tukaanza kuingiwa na wasiwasi. Ikabidi tungojee kwa muda wa dakika ishirini tena. Nilipotoka tu baada ya dakika kama tano hivi Lulu naye hakuonekana tena. Pia vijana fulani watatu waliokuwa wakienda lakini tukaona mambo yasingekuwa mazuri sana kwako. Maana usingalijua tumekwenda wapi. Baada ya kungoja kwa dakika ishirini tena, mimi na Robin tulianza kuwa na wasiwasi. Kwa hiyo mimi nikakata shauri nikufuate na kumwacha Robin humo Klabuni kuzidi kuchunguza.

Nilichukua taxi hapo nje mpaka nyuma ya Hilton Hoteli na kuanza kutembea kwa mguu mpaka hapa hotelini. Ndani ya bar watu walionekana kushughulika na ulevi. Kwa hiyo mimi nilienda kwenye kaunta na kuagiza 'bia' moja. Nilianza kumwanguka kila mtu kwa usiri sana. Mwishowe ndipo nikamwona mtu akipenya kwa haraka kati ya mlango mmoja unaotokea nje kwenda mwenye vyumba vya kulala. Huo mlango umeandikwa “HAKUNA KUPITA HAPA.”

Nilipoona hivyo nilitoka kwenye 'kaunta' kwa siri na kuingia katika vyumba vya huko juu. Halafu nikangoja. Kwanza mtu huyo aliingia katika chumba cha mkono wa kulia. Baada ya kukaa kidogo alitoka na kuingia humu. Wakati wote huu miye nilikuwa nashindwa kutoka, kwani kulikuwa na wafanyakazi wa humu hotelini wakifanya kazi.

Alipotoka ndipo nikakimbia na kuingia katika chumba cha upande wa kulia. Baada ya kuchungua sana niliona hakikuwemo chochote humo. Ila ukutani katika pembe moja kuna matundu matatu. Haya matundu yanatosha kuingiza mdomo wa bastola. Na ninadhani ndimo huyu mtu wa pili alimomwulia mtu wa kwanza. Na kwa kutumia tundu hilo hilo ndimo mimi nimemwua huyo jamaa. Na nimetumia 'sailensa' hata mimi,” alimaliza Sammy.

Na mimi nikamweleza mambo yote yalivyotokea.

Sasa tulijaribu kuunganisha mambo yote yalivyotokea.

Inaonekana hawa watu walijua John amekuja kufanya nini kwa hiyo walitumia kila njia wamwue. Pili wanajua kuwa kuna watu ambao watafanya kazi hii na John,

hivyo walikuwa wanavizia mtu yeyote ambaye angekuja katika chumba cha John. Nilipokuwa nimepiga simu mara ya kwanza inawezekana hawa watu walikuwa chumba cha pili. Nilipokata simu, nadhani walionelea wakate waya wa simu, ndiyo sababu wewe uliponipigia haikuweza kulia kengele.

Nilipofika mimi walijua lazima ndiye mwenzake John, hivyo lililokuwepo ni kuniua hata mimi. Nilipoweza kumshinda Kasha. huyu mtu wa pili alikuwa chini ya hoteli akimngojea Kasha. Kasha alipokawia akaona aje aangelie. Alipofika humu hakuja moja kwa moja, akaona aingie mwenye chumba hicho cha pili sababu alijua kuwa wameshatayarisha hayo matundu. Alipochungulia aliona nimeshamshinda nguvu Kasha. Na Kasha alikuwa karibu atoe siri, kwa hiyo ikambidi amwue Kasha kabla hajasema.

“Angeniua na mimi papo hapo lakini alitaka kuwa na hakika mimi ni nani, kwa vile alivyodhani anaweza kunilazimisha kusema. Nilipokataa kumwambia uhakika aliona aniulie mbali, lakini wewe ukamuua kabla. Huyu mtu wa pili alionekana kuwa wa maana zaidi katika huu uhaini kuliko Kasha. Sasa lililopo ni kutaka kujua hawa ni akina nani.” Nilinyamaza kumeza mate.

“Maswali ya kujiuliza sasa ni mawili au matatu. Je walimfahamuje John, mapema hivi? Je huyu mwenye hoteli ana uhusiano nao? Sammy alitaka kuzungumza.

“Willy mimi naona kuwa wewe uende tena huko Princess maana sasa ni saa sita kasoro robo. Miye nitarudi Starlight nikamwone Robin. Huenda akawa na jambo. Halafu wewe nenda kazungumze na wafanyakazi wa hapo upate kujua lini chumba hicho kimeacha kutumika. Nadhani vijana wa Robin wamemvia Lulu kwa hiyo huenda Robin anaweza kuwa na jambo juu ya Lulu na watu wake. Hizo maiti hazitatambuliwa huenda mpaka kesho asubuhi. Hii itatupa muda wa kutosha kufanya kazi zetu.

Ukitoka Princess njoo moja kwa moja mpaka Starlight Klabu kabla ya saa saba. Ukichelewa tutajua huenda umesakamwa na siye tutakimbia kuja hapo.”

Mawazo ya Sammy niliyaona kuwa ya busara sana. Kwa hiyo tulifanya kama alivyosema. Nilikodisha gari toka River Road kupitia Compos Robeiro mpaka Princess. Sammy naye akakodisha gari kwenda zake Starlight.

Nilipofika Princess nilikuta watu wote bado wanashughulika na kunywa, na kila mtu alijali mambo yake. Wengi walikuwa wakimalizia vinywaji vyao kwani saa za kutoka zilikaribia. Katika pembe moja nilimwona msichana mmoja ambaye

hakuonekana mwenye furaha hapo halipoketi. Nilipokuwa nikimfuata hakuonekana kupenda nimfuatie hivyo.

“Habari zako binti,” nilimsalimu. Badala ya kunijibu alinitizama tu. Nilikaza roho kiume, nikaenda kukaa kwenye meza moja naye. Uso wake ulionyesha uhasama wa chuki, ingawa sura yake ilikuwa na haiba kiasi cha kutosha .

“Mbona nyiye wanaume hamwezi kujali mambo yenu wenyewe? Huko kuniona hapa unadhani mimi natafuta wanaume?” Alisema kwa dharau.

Si hivyo bibie. Miye mwenzio si mwenyeji sana hapa. Nimekujia ili unisaidie mambo mawili hivi. Na hakika nilistaajabu kuona kisura kama wewe kukaa peke yako hapa pembeni tena ukionekana mwenye kuwa na huzuni. Je, kuna jambo lmekuudhi? Ama ikiwa ni shemeji aliyekuudhi, nitumie nikamsihi,” Nilinyamaza nikitabasamu.

“Sema basi unataka nikusaidie nini? Miye hapa napumzika na kawaida yangu huwa sipendelei sana kukaakaa na wanaume wanaokunywa pombe. Ndiyo sababu nimekaa hapa peke yangu. Wewe ni nani?” Aliuliza.

Mimi ni Joe Masanja, mwandishi wa habari juu ya maonyesho ya mavazi. Ninatoka Mwanza. Tanzania. Hii ni mara ya yangu ya kwanza kufika Nairobi. Nina haja ya kujua baa hapa Nairobi zinafungwa saa ngapi siku za jumapili?”

“Nenda uulize huko baa,” alijibu kwa hasira.

“Ah binti! Mbona wasichana wa Nairobi wakali hivi? Msichana kama wewe hufai kuwa mkali kwa kijana kama mimi. Uzuri wako unakutaka uwe mkarimu na msikivu ili uweze kuziliwaza nyoyo za watu dhalili kama miye.” Nikamjengea tabasamu pana la haiba.

Maneno hayo yalimlainisha kiasi. Ukitaka msichana afurahi, mwambie kuwa midomo yake ni mizuri na mitamu.

“Wanafunga saa saba, lakini unaweza unafungiwa ndani ukaendelea kunywa mpaka huenda hata saa tisa,” alijibu.

“Jee unaitwa nani, na unakaa wapi?”

“Mimi naitwa Lina Samson. Kwetu Nakuru, lakini kwa sasa niko hapa kwa mapumziko kidogo ya mwezi mmoja. Ninaitambua vyema Nairobi sababu nilizaliwa nikakua na kusoma papa hapa mpaka baba alipohamia Nakuru, ambako ndiko masikani hasa,” alijibu hali akimwemwesa.

“Sijui kama nitakuona tena Lina. Ningependa kukuona mara nyingi kama hutajali,”

“Ninaishi Guaden Hoteli chumba nambari kumi. Unaweza kupiga simu hapo hotelini, na watakuunganisha na chumba changu. Alamsiki,” alimalizia hali akisimaa kujiandaa kuondoka hapo. Akaondoka.

Nilizunguka zunguka kidogo humo ndani kusudi niweze kuona kama naweza kumpata mfanyakazi anayeweza kuaminika kidogo. Nilimuona kijana mdogo hivi, apata umri wa miaka ishirini. Nilitoa noti ya shilingi mia na kumpa. Utafikiria kuwa huenda natumia pesa vibaya, lakini ukitaka cha uvunguni sharti uiname. Kijana kama huyo wakati wa mwambo kama huo ukimpa shilingi mia atakueleza hata yale aliyoyazungumza na mpenzi wake faraghani. Kijana huyo aligutuka sana hata akaniuliza, “He, unataka nini, pombe gani?”.

“Hiyo fedha nimekupa, chukua ni yako. Sasa tafadhali naomba unielezee habari fulani fulani, Mbona chumba nambari hamsini hakina kitanda wala mtu?”

“Hicho chumba hakina mtu kwa sababu kinavuja kwa juu siku za mvua. Na siku hizi kuna manyunyu mengi”.

“Kimeanza lini kuvuja?”

“Leo kiasi cha saa nne hivi kama unakumbuka kulikuwa na manyunyu,”

“Nambari hamsini na moja kulikuwa na mtu?”

“Ndiyo, mtu mmoja toka Uganda aitwae Fred, ndiye alikuwa amepanga humo kuanzia saa moja asubuhi.”

“Kuna mtu yeyote aliyewahi kuingia chumba nambari hamsini kutoka nje wakati wa mchana?”.

“Ndiyo, mtu mmoja aitwae Benny, alikuja na watu wengine watatu hivi. Waliingia kukitazama kama wanaweza kukiziba, lakini baada ya kukikagua sana walisema hawawezi, wakaenda zao. Sifahamu wanakaa wapi”, alimaliza.

“Basi usimwambie mtu yeyote nilivyokuuliza.”

Nilipotazama saa yangu, ilikuwa saa tisa na nusu. Nilitoka hapo baa na kukodisha gari hadi Starlight. Niliwakuta Robin na Sammy wakitungojea.

Robin hakuonekana mwenye furaha. Nadhani Sammy alikuwa amemweleza mambo yalivyokuwa. Halafu niliamua kupiga simu polisi ili waweze kushughulika na hizi maiti.

“Hapo ni Polisi?”.

“Ndiyo Bwana, unataka nini?”.

“Naweza kuzungumza na Polisi Inspekta Tsumah?. Tafadhali”.

“Ngoja kidogo” alijibu.

“Halo, huyu ni Polisi Inspekta Tsumah. Nani mwenzangu, na nikusaidie nini?”

“Mimi ni rafiki yako, ambaye ninazo habari za kukugutusha kidogo. Ni kwamba ziko maiti tatu katika Princess Hoteli chumba nambari 51. Nenda ukajionee mwenyewe. Miye sina uhusiano nazo. Kwaheri.” nilikata simu kabla hajaweza kusema neno lolote.

Nilipiga simu kwa Chifu saa hiyo hiyo, nikimweleza kuwa awashauri maafisa wa polisi wasishugulike sana na mauaji yoyote yatakayotokea hapa Nairobi mpaka tutakapokuwa tumemaliza kazi yetu. Pia nilimweleza kuuawa kwa John.

Robini alitoa taarifa aliyokuwa amepewa na vijana wake juu ya Lulu. Alisema, “Baada ya wewe kutoka, Lulu naye alitoka. Mmoja wa vijana wangu alimfuata, na ilionekana Lulu alikwenda moja kwa moja hadi International Cassino. Alivyofika huko alisimama nje kwanza. Kisha alitoka kijana mmoja katika International Cassino na kuja kuonana naye. Alinyamaza alipokuwa akimeza mate.

“Walikaa hapo nje kwa muda. Kisha huyo kijana alimpa busu Lulu. Ilionekana kuwa Lulu alikuwa akimtegemea huyo kijana huko Starlight, lakini kijana huyo hakuonekana. Ilionyesha kuwa Lulu alijua kwamba huyo kijana mara nyingi alikuwa akienda Cassino. Alipofika hapo nje kumbe huyo kijana naye alikuwa akitoka. Kijana wangu alifikilia kuwa lazima wawe marafiki. Kijana huyo alionekana nadhifu sana, lakini macho yake yalionyesha uovu mwingi. Kijana wangu hakuweza kusikia waliyokuwa wakisema, ila alibuni kuwa walikuwa wakizungumzia juu ya kitu fulani kuhusiana na Starlight Klabu.

“Kijana wangu alingoja hapo mpaka walipokuwa wakiondoka. Walipoondoka, Kama alivyoripoti kijana wangu, waliingia katika gari moja Zephyr 6 nambari KKK 117. Walivyoanza safari ya kurudi mjini na Uhuru High Way naye aliwafuata. Walienda na kusimama nje ya Hoteli Intercontinental. Na Lulu alitoka nje. Alipokuwa akiingia hotelini, kijana wangu alimsikia Lulu akimuaga huyo kijana kwa sauti, “Kwaheri Benny.”

Kusikia jina la Benny, nywele zangu zilisimama kidogo, kwani yule kijana wa Princess alikuwa pia ameniambia kama unakumbuka. Benny alikuwa amekuja kuchunguza kile chumba nambari 50. Katikati yangu na wewe nadhani Benny ana jambo hapo.

Nami nilimweleza mambo ambayo niliyapata kutoka kwa yule kijana wa hotelini. Nao walianza kumshuku Benny na Lulu pia. Maana kama nilivyosema awali. Kwamba wasichana walio vipande wote ni sumu mbaya sana.

Wote tulifikiria kwa tulikuwa tukianza kuona mwanga kidogo. Lakini ehee, makubwa yalikuwa bado yanakuja, kwani kama huyo Benny na Lulu ndiyo wanacheza haya mambo lazima kuna kitu!

Tuliondoka hapo nje ya Klabu na kila mtu akakodisha gari kwenda kulala. Tulikuwa tumepanga, kupigiana simu kesho yake asubuhi mnamo saa mbili. Robin alikuwa akilala New Avane Hoteli.

Gari niliyokodisha ilinipeleka hadi hoteli Fransae. Kisha niliingia vichochoroni mpaka Embassy Hoteli. Kama mtu alikuwa akinifuata, angeweza kufikiri kwamba nilikuwa nikilala hoteli Fransae. Niliingia chumbani kwangu ili nilale. Mawazo yangu yote yalikuwa juu ya mauaji ya John. Niliwaza kumuua huyo aliyemuua John iwapo muuaji huyo hatatangulia kiniua. Kitandani hapo chumbani, niliweka bastola yangu chini ya mto, kwani sikuweza kujua lini watu hao wangenifuata, maana wanaonekana kuwa wajuvi sana.

SURA YA NNE

ASUBUHI niliamshwa na mfagiaji, ambaye alikuwa anafagia nje ya mlango wangu. Kwa bahati mbaya akagonga mlango huo. Nilipotazama saa ilionyesha kuwa ilikuwa yapata saa mbili kasorobo. Nilikwenda kuoga, na kujiweka tayari kwa kazi ya mchana huo. Saa mbili kamili nilikuwa nimekwisha piga simu kwa Sammy na Robin.

Kabla sijapiga simu, Sammy alianza yeye kunipigia akisema, “hallo Willy, vipi? Umelala salama leo? Miye mwenzio nilikuwa na ndoto za ajabu na za kutisha. Nadhani kifo cha John bado kinanitisha. Sasa unasemaje, tuanzeje?”

“Sammy, nadhani haya tusiyazungumze kwenye simu, ila mpigie Robin simu umweleze mje hapa hoteli kwangu. Umeshapata kifungua kinywa ama vipi?”

“Bado sijapata, ila nategemea kupata sasa hivi.”

“Vema, tutaonana saa tatu.”

“Nililetewa kahawa na kuanza kunywa. Baridi ilikuwa kali sana... Ukungu ulikuwa umejaa kote. Siku ilianza kunitisha sana, hata kabla sijaanza kufanya lolote. Nilionekana mtu mwenye wasiwasi mwingi sana. Ungaliniangalia asubuhi hiyo hata wewe ungalinihurumia, ingawaje mimi si mtu wa kuhurumiwa. Ilipofika saa tatu. Sammy na Robin walifika. Mimi naona twende 'City Hall' maana maonyesho yanaanza leo saa tano. Na kama hamjui, leo ni sikukuu ya kufungua maonyesho. Kwa hiyo watu kote nchini wanapumzika hawaendi kazini. Na kwa sababu Lulu anasema ni mwonyeshaji mavazi, basi lazima atakuwepo. Na kama kweli Benny ni rafiki yake, hata yeye atakuwepo hapo 'City Hall' na kutokana na msongamano huenda tukafahamu lolote,” alisema Robin.

'Gazeti la Daily National' lilikuja, na baada ya kuliangalia ilionekana mengi hayakuandikwa juu ya hivyo vifo. Maana waliandika tu ya kuwa “Watu watatu walikutwa wamekufa katika chumba kimoja Princess Hoteli. Polisi bado wanafanya uchunguzi,” basi. Tulifikiria mkurugenzi wa usalama Kenya alifanya kama tulivyokuwa tumeomba.

Saa nne na nusu tuliondoka kuelekea City Hall. Sammy alibeba kamera na kuonekana kuwa mpiga picha hasa. Miye nilionekana kama mwandishi wa habari. Tulikuwa tumechukua vitambulisho vyetu. Tulipofika City Hall, baada ya

kuonyesha vitambulisho vyetu, tulikuta siye tumepewa viti huko mbele karibu na jukwaa kusudi tuweze kuangalia na kuchukua picha vizuri. Mimi na Sammy tulikaa karibu karibu na Robin alikaa mbali kidogo nasi.

Robin alikuwa ameishafanya mpango na vijana wake kuwa karibu karibu katika huo ukumbi, kusudi ikiwa wataweza kuona lolote waweze kusaidia.

Kitu kilichokuwa kinaniuma ni kutaka kujua zilipokuwa hizo karatasi za siri. Pia wakati gani wamepanga kuzibadilisha. Na tatu wapi ambako haya mabadilishano yangefanyika. Mpaka hapo tulikuwa tumekwisha hakikisha kuwa Chifu alivyobuni itakuwa sawa. Maana mpaka hapo ilionekana ni watu wa Afrika Mashariki waliotuandama. Kule kujua kwao kwamba siye tumefika Nairobi na kuanza kuwasaka, kungefanya waharakishe kuzibadilisha hizo karatasi, kitu ambacho hatutaki kitokee. unaweza kuona mwenyewe jinsi muda ulivyokuwa mbaya. Akili zetu zilivurugika kama nini sijui.

“Hujambo mwananchi?” Nilisikia sauti kwa nyuma yangu ilinishtua sana kwa maana nilikuwa katika mawazo mengi. Nilipogeuka nikakuta ni mtu ninayemfahamu ambaye alikuwa muda mrefu sana Dar es Salaam. Huyu alikuwa Peter ambaye naye alikuwa mpigania uhuru na sasa akiwa ameletwa Nairobi kufanya kazi.

“Hallo Peter, habari? Mimi ni Joe Masanja nimekuja hapa kama mwandishi wa habari juu ya maonyesho ya mavazi. Na huyu ni Athumani Hassan, Mpiga picha”.

Peter alijua nilikuwa na maana gani sababu ananijua, na anajua kazi yangu ni nini.

“Mmefika lini hapa. Lazima liwepo jambo alininong'oneza.

Kisha aliandika habari kwenye karatasi na kunipa. Humo aliandika maneno haya,” Jee mmekuja kuchunguza kuhusu tukio la jana? Nimeambiwa na ofisi ya Dar es Salaam nisaidie. Kama ndivyo niko tayari kuwasaidia.”

“Tulifika jana. Na hasa,” nilijibu.

Peter alielewa, kisha alihama akaja kukaa na sisi. Alikaa upande wangu wa kulia na Sammy upande wa kushoto.

Baadaye nilimuona Lulu anaingia akiwa na Benny. Nilimuuliza Peter, “ati unawajua hawa?”

“Siwajui, ila tu nimewahi kumuona yule Benny katika mabaa fulani fulani tangu nifike hapa Nairobi. Kama ukipenda kujua jambo lolote juu yake hiyo ni kazi rahisi. Ninaweza kukupatia habari kabla ya usiku wa manane leo.”

“Nitafurahi sana ukifanya hivyo na watu wako.”

Peter alioneka mwenye kuhudhunishwa sana na jambo hili akiwa kama mpigania uhuru. Baadaye Lina naye aliingia. Alikuwa peke yake kama kawaida. “Ulitaka kumuona yule? Nilimuuliza Peter.

Ndiyo. Yeye ni Lina Samson.”

Lina alikuwa msichana tofauti sana na wasichana wengine. Sura yake ilikuwa ya kupendeza vya kutosha, kama nilivyosema awali. Lakini licha ya Lina kuwa mzuri wa sifa hivyo, hakufua dafu kwa Lulu, kwani Lulu alikuwa 'Lulu' kweli. Pia Peter alisema utamkuta Lina siku zote peke yake mwenye mabaa akinywa soda akichanganya na 'Babycham'. Hivi ndivyo hata mimi nilimkuta usiku uliopita. Lina alituona akaja moja kwa moja kutusalimia. Kisha akanipigia kope akaenda kukaa mbali nasi kidogo.

Wakati Benny alipoingia na Lulu kila mtu aligeuka kuwaangalia. Lulu alitembea kwa maringo sana na Benny alionekana akifurahia kuona kila mtu akimwangalia wakati wakifuatana na mrembo huyo wa kushtua. Hata mimi nilimuonea wivu. Maana nilitamani niwe mimi badala yake nitembee na mrembo huyo. Lina alimwangalia sana Lulu. Nikaona huenda alikuwa pia akimuonea haya Lulu.

Nilitambua kuwa Lina anamfahamu Benny, kwani Benny alipokuwa anapita na Lulu, alipomuona Lina amekaa karibu na mahali walipokuwa wakipita, alitazama chini. Kwa hiyo niliona itakuwa vizuri kama nitaifanya urafiki na Lina maana naweza kupata msingi mdogo wa kutusaidia. Pia niliona Lina angeweza kusikilizana na mimi, kwani kama nilivyosema alinipigia kope kuonyesha dalili ya urafiki.

Maonyesho yalipoanza wanawake walianza kutoka mmoja mmoja wakionyesha mitindo ya kila aina. Kulikuwa na wanawake kutoka karibu kote Ulimwenguni wakitoa mitindo mbali mbali. Niliandika kikaratasi na kumpa Sammy akiangushe katika mapaja ya Lina, wakati akijifanya kama kwamba anatafuta mahali pazuri kwa kupiga picha. Niliandika, “Tafadhali tuonane nje, kwenye mlango mkubwa, kama dakika kumi kabla ya watu wote kutoka. angalia watu wasifahamu unaningoja mimi.

Sammy alikiangusha kama nilivyomueleza. Baada ya kusoma bila mtu kujua aliniangalia na kutikisa kichwa, akionyesha kuwa amekubali. naye alianza kuandika kwenye hicho kikaratasi. Akakitupa mbele ya Sammy. Alipokuwa anarudi. Sammy alijifanya ameangusha kasha la 'Film', akainama na kukiokota hicho kikaratasi pamoja na kasha la 'film' yake. Niliposoma nikakuta maneno haya.

“Ndani ya gari langu jeusi namba No. KKT 581 - Mazda Delux - kulia mwa mlango mkubwa” basi niliona mambo yote yamekuwa kama nilivyopanga. Lakini ukavu wa macho ya Lina ulinitisha kiasi cha kwamba woga uliniingia kidogo. Lakini kwa sababu sikuwa mwoga kama wewe, sikujali lolote litalotokea baadae.

Lulu alijitokeza. Alipotokea kwenye jukwaa kila mtu alipiga kelele, kwa vifijo na ushangiliaji wa ajabu. Lulu aling'aa kama nyota. Alionyesha mtindo wake unaoitwa 'Popcom'. Wachukuaji wa picha walichua picha kwa fujo sana.

Alipokuwa anarudi kwenye chumba wanachotokea. Robin alipita karibu yangu na kudondosha kikarasi. Nikakisoma kilikuwa kimeandikwa “Mjiangalie sana, maana yametokea mauaji mawili tayari humu ndani”, wakati Lulu alipotoka na watu walipokuwa wakipiga kelele na kushangilia vibaya sana, vijana wetu tuliokuwa tumewaweka kuviziavizia, wawili wao wameuawa. Inaonekana waliona jambo fulani ambalo limewaponza. Mueleze na Athumani, laa zivyo na siye tutakufa”.

Loh wasiwasi ulinizidi sana. Sammy alipokuja karibu yangu nilimueleza mambo yalivyokuwa. Zilikuwa zimebaki kama dakika kumi na tano hivi maonyesho ya asubuhi yaishe. Hivyo tukafungashafungasha vijitabu vyetu tuondoke. Tulimuaga Peter baada ya kumweleza ninapokaa. Tulitazama huku na huku kwa mashaka makubwa sana. Nadhani hata wewe unaweza kufikiria mawazo tuliyokuwa nayo.

Tulipofika mlangoni, nilibahatisha kumuona Benny amesimama na kijana fulani akimueleza mambo fulani fulani na huku akitutizama kwa usiri mno. Nilijua alikuwa akimuambia huyo kijana atufuate. Hivyo nilimueleza Sammy abaki nyuma kidogo ili niweze kuwapoteza wasije wakajua ninaondoka na Lina.

Peter alikuwa kwenye dirisha moja la 'Hall’ na akaniona nilipokuwa nikiingia katika gari la Lina. Akanipungia mkono. Nadhani aliweza kupata nafasi ya kukisoma kikaratasi cha Lina. Sikujali Peter kufahamu hayo, kwani na yeye ni mtu wetu.

“Mtu yoyote amekuona?”

“Hapana, uenda wamekuona wewe” alijibu.

“Sidhani kama wameniona”

Lina alitia moto tukaondoka. “Tupitie njia ipi?” aliuliza.

“Twende moja kwa moja, mpaka Embassy Hoteli.”

Lina alivuta gari mpaka tukaingia Kenyatta Avenue. Nilipotazama nyuma, niliona gari moja kama kwamba linatufuata. Kutaka kuhakikisha nilimueleza Lina badala ya kuingia Koinange akate kona na kuingia uhuru High Way. Halafu aingie Haile Selassie Road. Gavament Road ndipo turudi Kenyatta Avenue. Kisha tuendelee na safari yetu. Kusema hili gari lilikuwa linatufuata maana kuzunguka kote huku nalo lilikuwa bado linazunguka kutufuata tu. Tulipofika kwenye kona ya Kenyatta Avenue nilimwambia Lina asimame, aliposimama hilo gari nalo likasimama karibu sana nasi. Nilitoka nje nikamfuata dereva wa gari hilo.

“Sikiliza bwana mdogo, Miye sitaki kufuatwafuatwa. Sikuzoea mambo hayo. Na kama hutaki meno yako zidi kunifuata. Kamwambie huyo mume wako aliyekutuma kuwa kama anataka kunitafuta aje yeye mwenyewe ajionee. Kama unataka usalama tia gari lako moto uende zako.”

Kijana huyo hakuwa na la kufanya ila kufanya kama nilivyomwambia. akaenda zake. Nilirudi katika gari la Lina akaendesha mpaka Embassy Hoteli.

“Sikiliza Lina, nenda ukasimamishe gari hili mbali na Embassy Hoteli kusudi hawa wahaini wasijue tuko hapa wakatufuata”

Baada ya kuweka gari Lina alikuja tukapanda mpaka kwenye chumba changu. “Sijui kwa nini naonekana kukupenda, maana tangu jana mle Princess Hoteli, baada ya kutoka na kukuacha humo, usiku mzima sikulala ila kukufikiria wewe tu.” Alisema Lina hali akijilaza.

“Oh Joe, mpenzi nakupenda sana ingawaje unaweza kuniona kuwa miye malaya kwa kukufuata baada ya kuonana siku moja tu. Lakini lazima ujue kuwa mtu unaweza kuwa hujapenda, lakini akaja mtu mgeni ukampenda kufa. Hapa Nairobi nimeishawahi kufanya mapenzi na mtu mmoja tu, ambaye anaitwa Benny Makunda. Lakini hata siku moja sikuweza kukosa usingizi juu yake, kama nilivyokosa juu yako jana. Ningejua unakaa hapa basi tu ningekufuata.”

“Waaa, unasema kweli ama tu kunidhihaki? Hata mimi nimekupenda Lina. Tangu jana tabia yako ya utulivu na kiburiburi niliipenda sana. Maana mimi napenda watu kama hao hasa wakiwa wasichana”

Loo! Hapa niliona mambo yanakorogana sana Benny aliwahi kuwa mpenzi wa Lina. Na Benny ndiye tuliyekuwa tunamashaka naye. Huyu kijana anaonekana ni 'Champion' kwa wanawake, kwani sasa anatembea na Lulu. “Huyu msichana Lina ananitania ama vipi.” ndiyo sasa yalikuwa mawazo yangu. “Lakini yote hayo nitafahamu muda si mrefu kwani naweza kumusoma msichana kama Lina Vizuri sana.”

“Kumbe unamfahamu Benny, hata amewahi kuwa mpenzi wako?” Nilimuuliza.

“Ndiyo,” alijibu.

“Mmeachana tangu lini?”

“Kuna huyu msichana wanayemwita Lulu. Msichana huyu anatoka Uganda na huwa yuko huku mara nyingi sana. Sura yake kama ulivyomuona inavutia wavulana wengi sana. Alipokuja huku mwezi wa jana Benny alimuona, na wakaanza mapenzi. Mwishowe Benny hakunijali tena. Nami kwa tabia yangu nikaona siwezi kupenda mtu ambaye hapendeki.

“Kwanza nilimuonya Benny asitembee na Lulu kwani Lulu ingawaje ni mzuri kiasi cha kutisha namna ile, lakini ni hatari sana kwa mambo ya ukahaba. Lakini baada ya muda mfupi Lulu alirejea Uganda. Benny akarudi sasa. Lakini miye sikumtaka tena.

“Benny ana fedha na ana fedha nyingi. anazitoa wapi sijui, lakini ana fedha. Kazi yake ni dereva wa taksi tu. Anaendesha taksi yake moja 'Mercedes Benz'. Nilipokataa Benny alinibembeleza sana lakini nikakataa tu bado. Alinihidi kuwa angelinunulia gari moja aina ya 'Citron' mwezi huu, maana atakuwa 'Giriki' mwezi huu. Miye nilizidi kukataa tu. Na nilikuwa nimeapa hata siku moja sitafanya mapenzi na mvulana tena. Nilikuwa nafikiria kwenda kuwa mtawa. Bahati nzuri au mbaya ndipo akaja huyu kijana ambaye amenifanya hata sikuweza kulala. Oh, kweli mama aliniambia usimpende mgeni, lakini mimi hata, nitakupenda tu.” alimalizia Lina.

Bado mimi sikumwamini hata punje.

“Benny alikwambia hiyo pesa angetoa wapi?” Nilimuuliza.

Alisema ati ana rafiki zake huko ng'ambo ambao wangemletea fedha hiyo. Benny anafahamiana na wazungu wengi sana,” alisema kwa mashaka kidogo.

Ubaya wa huyu msichana ni kuwa huwezi kumwelewa hata kidogo kwani anaposema, husema kwa utulivu mno hivyo kwamba huwezi kumtambua yupo upande upi.

“Unaweza kuwatambua wazungu hawa ukiwaona?”

“La, wengi wao wamerudi kwao. Ndiyo sababu nakueleza kuwa, watamtumia pesa kutoka ng'ambo waliko,” alijibu.

“Unafikiria ni Wazungu kutoka upande gani?”

“Sijui maana mimi nilikuwa sihusiani nao sana.”

“Ni wanaume au wanawake?” Nilimwuliza huku nikijifanya siyajali sana mazungumzo yake haya.

“Wuuuuu. Willy, Willy Gamba, umesema ndiye wewe! Loo! Siamini masikio yangu ni wewe kweli, kweli! Nimesikia jina lako mara nyingi. Nimesikia sifa zako. Nilikuwa nikidhani ni hadithi tu kama tunazosoma katika vitabu. Sikufikiria ama kuota kama nitakuona. Nimesoma habari zako katika magazeti, lakini nilikuwa sijaota ya kuwa siku moja nitalala kitandani na Willy Gamba.” alisema Lina huku akitetemeka na kunibusu, “Nini kimekuleta sasa hapa, Willy?” aliuliza.

Nilifikiria sana kama naweza kumwambia. Mwishowe nikakata shauri nimwambie kwani siye nyakati zingine huwa tunaropoka kusudi tuone nini kitatokea. Mara nyingi huwa tunajitega wenyewe halafu tunatafuta njia ya kujinasua tena. Hivyo nilimweleza mambo yote tangu mwanzo mpaka mwisho. Pia nilimweleza jinsi tunavyomfikiria Benny. Na jinsi ambavyo tumenusurikanusurika usiku wa jana.

“Jana usiku nilipokuwa nikitoka nilimuona Benny hapo nje ya Princess katika gari moja ya Kimarekani 'Pontiac' yeye hakuniona” aliniambia Lina.

Kama Lina anasema kweli basi Benny ndiye alipanga mauaji ya John na kama nilivyokwambia ahadi chuki na uchungu viliniingia juu ya Benny.

“Je unamjua rafiki yake yeyote wa Kireno au wa Afrika ya Kusini?”

“Hapana lakini naweza kukusaidia ukitaka,” alijibu.

“Kukuambia ukweli Benny si mchezo. Anatembea na bastola tatu, na kila nilipokuwa nikimuuliza ni za nini aliniambia kuwa ni za kujikinga kutokana na maharamia. Maana akiwa na taksi, wanaweza kuikodisha halafu kufika njiani wakakunyang'anya, hasa mtu mwenye 'Benzi' kama yeye. Tena akipiga risasi zake

hazikosi. Maana siku moja tulikwenda msituni kuwinda katika bonde la ufa, ndipo nilimtambua.

“Tulikuwa na mdogo wake ambaye alibeba chupa za fanta ndogo. Basi alikuwa anaweka hizo chupa kwenye kichwa cha mdogo wake na kuanza kupima shabaha kwa bastola. Ajabu ni kwamba hakuweza kumjeruhi mdogo wake hata kidogo. Na aliniambia kuwa huwa anafanya haya mazoezi mara mbili kwa juma. Hivyo nakusihi Willy usimuendee ovyo.

“Asante sana kwa kunionya Lina maana kama ningalikurupuka huenda hata mimi ningeyala marisasi kama rafiki yangu John.”

Mara simu ililia.

“Huyu ni Peter nazungumza, ni Joe huyo?”

“Ndiyo Peter unataka nikupe hadithi gani?”

“Sikiliza Joe, na habari. Nimepata habari kamili juu ya maisha ya Benny, Benny anakaa Westland 'plot No. 3' karibu na Sclatirs Hostel. Yeye ni dereva wa taksi. Anaendesha taksi moja aina ya 'Mercedes benzi 280 SE'. Nambari KKZ 601. Rangi ya kijani. Benny anafahamika kuwa kijana tajiri sana, maana hilo gari lake linapendwa na watu wengi hasa watalii. Hivyo anafahamiana na watalii wengi sana. Amesoma mpaka darasa la kumi na nne. Kisha akaenda nchi za ulaya, ambako inasemekana hakufanya vizuri katika mtihamu wake ikapasa arejee. Amewahi kukaa ureno kwa muda fulani fulani huko. Ni kijana fundi sana katika kutumia bastola. Ana shabaha za ajabu. Walimuomba aende jeshini akakataa. Polisi huwa wana mashaka naye kuwa uenda akawa naye ndiye mmoja wa magaidi wa hapa Nairobi wanaonyang'anya mali katika maduka makubwa makubwa na benki. Lakini hawajawahi kumshika ila wanamfikiria tu. hajapelekwa kontini hata siku moja. Tabia yake ni ya utulivu sana, lakini ni shupavu sana na mvumilivu wakati wa shida. Wasichana wengi sana wanakufa kwake kwa sababu ana sura nzuri. Kama onavyomuona. kwa kifupi ndivyo mambo yalivyo.”

“Asante Peter, endelea kufanya uchunguzi uwao wote ambao unaweza kutusaidia.”

“Miye nitajaribu kila njia ya kuwasaidia. Na kama una shida nyingine yeyote unaweza kunieleza tu. Kwa kheri mpaka wakati mwingine.”

Nadhani hata kama huwa unatumia makamasi badala ya ubongo, unaweza kuona mambo yanavyokuja yenyewe. Benny anafahamu kutumia bastola vizuri sana. Kwa hiyo Benny analo kundi la watu ambao amewafundisha namna ya kutumia

bastola nao wamekuwa stadi kama yeye. Benny amekaa ureno kwa muda, na alipokuwa huko alifanya urafiki na watu wa huko na hata akaweza kutumia bastola vizuri sana. Ni wazi kuwa hao wareno wamejua habari za hizo karatasi za siri. Wakakata shauri waziibe.

Wamejaribu wao wenyewe na kushindwa. Waliposhindwa na kuona wao hawawezi kuziiba wakatafuta majambazi wa hapa hapa Afrika ya Mashariki. Kwa sababu wanamjua Benny na amewahi kuwa rafiki yao wakamwendea.

Walipomwendea Benny akaona hawezi maana hana fedha ya kutosha. Lakini Benny anajua kundi fulani la majambazi, kwa hiyo akaenda kumwambia 'bosi' wa hayo majambazi juu ya wizi wa karatasi hizo. Na, pia kuahidiwa kupata fedha nyingi sana. Huyu 'bosi' akakubali.

“Kisha akamfanya Benny mkubwa wa genge hilo akapewa pesa, gari na kila kitu. Sasa shida ikawa watazipataje, kwa hivyo wakatafuta mtu mwenye kujua habari nyingi juu ya hizo karatasi na kuwapa mambo yote.

“Umeona basi mambo yalivyo? Kufika hapa sasa naanza kuona mwanga. Ila kuna maswali ya kujiuliza. Je huyu boshi ni nani? Je nani aliye na karatasi sasa? Tutawashikaje maana wameisha tufahamu. Huyu aliyetoa habari ni nani? Na wakati gani hivi vitabadilishwa? Na nani aliyekuja kuzichukua hizo karatasi toka Ureno?.

Ukinijibu maswali haya, nadhani tutakuwa tumemaliza kazi yetu. Lakini rafiki yangu, inaonekana kabla hatujajibu maswali haya tunaweza kuwa wote tumeisha kufa, maana kuyajibu, kuna maana ya ua au uuawe. Ureno, hii ni kazi ya Ureno. Kwa hiyo lazima mwenye kuzichukua kuzipeleka Ureno ni mwenye asili ya Kirenoreno. Na kama kubashiri kwangu ni sawa naona tunaweza kufanya kitu , lakini kama ndiyo nimekosea, basi tumekwisha kazi kabisa.”

“Lina,” nilimwita hatimaye, “tafadhali jaribu kuchunguza lini Benny alianza kuwa dereva wa tekisi. Pili lini amenza kukaa huko Westlands, maana najua ni watu wenye fedha sana tu wanaoweza kukaa huko. Tatu, kama unaweza, jaribu kupata habari za Wazungu anaotembea nao Benny siku hizi. Ukiwa kama msichana wake wa zamani, ukijifanya bado unampenda, kwa hiyo unajaribu mrudiane, nadhani unaweza kupata majibu ya maswali yangu. Pia jaribu kuchunguza ni Wazungu wa kutoka wapi hao rafiki zake.”

Niliagana na Lina akaenda zake. Nilijilazimisha kumwamini. Na kama nilikuwa nacheza na moto, Mungu ndiye anayejua. Kwani Chifu alisema, “Mara hii usiamini mwanamke yeyote.”

SURA YA TANO

MNAMEO saa nane Sammy alikuja chumbani kwangu. Akanieleza, “Unajua Willy, huyu msichana Lulu pia ni hatari. Maana kila alipokuwa akitoka kuonyesha mavazi anafanya maringo kiasi cha ajabu hata watu wote kushangilia. Na wakati wanaposhangilia ndipo watu wanauawa.

Kwa hiyo inaonekana kuwa kila Lulu akitoka hawa watu huwa wameona hatari kwa upande wao hivyo hupeana ishara. Lulu anatoka, watu wanashangilia, wao wanaua!”

“Sasa wewe unafikiria tutaendelea vipi?” Nilimuuliza baada ya kumweleza yote niliyokuwa nimeambiwa na Lina pamoja na Peter.

“Mimi naona kuwa twende kwenye maonyesho ya saa kumi. Na twende tukitahadhali sana. Kitu tutakachotafuta ni mtu anayeruhusu hao wanawake kutoka. Tukimfahamu huyo basi tunaweza kujua mengi. Na pia lazima tumpate Lulu tuweze kujua anajua kiasi gani cha habari hii”.

Nilikubaliana na mawazo ya Sammy, kwa hiyo tulimpigia Robin Simu kumweleza jinsi tulivyokwishaakata shauri la kwenda maonyesho ya saa kumi. Naye alituambia kuwa angekuja kutupitia hapo chumbani kwangu. Mpaka sasa tulikuwa tumejua kuwa wameishatufahamu, la sivyo wasingelinifuata wakati nilipokuwa nikija nyumbani na Lina.

Robin akaja saa tisa na nusu, tukaanza safari kwenda zetu 'City Hall'. Kila mtu alikuwa amechukua bastola kwapani kama ingekuwa lazima itumike.

Tulienda tukakaa kwenye viti vyetu vil evile vya asubuhi. Peter naye alikuja akakaa karibu yetu tena. Lina hakuonekana mchana huo, watu wengi walikuwa wamekuja huo mchana na ukumbi wote ulijaa.

Kama kawaida ya Benny na Lulu walikuja wamechelewa kidogo. Kila mtu alipiga makofi walipokuwa wakipita. Lulu alivaa 'mini' moja inayoonyesha mapaja yake kwa uwazi mno kabla hajaenda kwenye chumba cha maonyesho, Lulu alimvuta Benny wakaja moja kwa moja mpaka tulipokuwa tumekaa mimi, Sammy na Peter. Benny hakuwa na furaha alipotuona. alionyesha kicheko, lakini kicheko chake kilikuwa cha chukichuki.

“Nadhani hamtajali kama nitawafahamisha kwa rafiki yangu huyu,” alisema Lulu.

“Hatutajali,” alijibu Sammy.

“Huyu anaitwa Benny Makunda, dereva wa Teksi na ni rafiki yangu.” Kisha aligeuka kwa Benny akasema, “Na huyu ni Joe Masanja, yule ni Athumani Hassani, wote waswahili kutoka Mwanza wamekuja kwenye maonyesho ya mavazi hapa petu, maana wao ni waandishi wa habari.”

“Nimefurahi kuonana nanyi. Bila shaka mnaipenda hali ya hapa petu Nairobi,” alisema Benny, huku tukishikana mikono.

“Nasi pia tumefurahi sana kukutana nawe. Na hali ya hapa inaonekana kuwa baridi, lakini tunaipenda, “nilijibu kwa niaba ya wenzangu.

“Mtakaa hapa muda gani?” aliuliza Benny akinikazia macho.

“Mpaka mwishoni mwa wiki,” nilimjibu.

“Na mkitoka hapa mtarudi Mwanza, ama mtaenda mahali pengine?” aliuliza Lulu.

“Tutaenda Kampala,” nilimjibu huku nikitabasamu kidogo.

Nakwambia tabasamu la Lulu, ni hatari, maana alipotabasamu nikasisimkwa na damu vibaya sana. Lulu na Benny walitupiana macho kisha wakatuaga, wakaenda zao.

Maonyesho yaliendelea kama kawaida. Nilitoka hapo nilipokuwa nimekaa nikaenda pande za ukutani, ukutani ambako ningeweza kuona vizuri Benny anafanya nini.

Nilimuona Benny akizungumza na Lulu katika chumba kimoja cha kubadilishia mavazi, maana mlango ulikuwa umefunguliwa. Kisha alimwendea kijana mmoja ambaye alikuwa amevaa vizuri sana huku akivuta mtemba. Huyo kijana, kule kumwona tu, utafikiri kuwa ni mwunguna sana.

Walizungumza kwa muda mfupi kidogo, lakini huyo kijana alionekana hapendelei hayo mazungumzo kwani alikuwa na wasiwasi sana. Baadaye nilikuja kutambua kuwa ndiye mruhusiji wa wanawake kutoka katika chumba cha kubadilishia mavazi kwenda kwenye jukwaa. Wanawake walikuwa mara kwa mara wakitoka na kuingia.

Mwishowe nilimwona Benny akiirekebisha tai yake kwa kuivuta vuta, baada ya kijana furani kupita karibu naye na kumpa kijitabu. wakati huo wote huyo kijana alikuwa akiendesha mpango wa jukwaani alikuwa akimwangelia Benny kila baada

ya nusu dakika. Hatimaye kijana huyo alikimbia moja kwa moja hadi kwenye chumba cha kubadilishia mavazi na kuzungumza na Lulu. Ilionekana ilikuwa zamu ya msichana mwingine kutoka lakini huyo kijana alibadilisha mpango na kumfanya Lulu atoke muda huo.

Moyoni nilijua kuna jambo, kutokana na tulivyoelewa asubuhi. Nilijiweka tayari, maana ilionekana huenda mimi ndiye nimetiliwa mashaka. Kwani wanaweza kuwa wameniona nikichunguza mienendo ya Benny, alipokuwa akizungumza na kijana wa kwenye jukwaa pamoja na Lulu.

Lulu alipotoka alikuwa amealia Mufti. Mara hii alikuwa ameonyesha mtindo mwingine unaoitwa 'love at night' yaani 'mapenzi wakati wa usiku'. Kweli ulitisha kwani mwili wa ndani wa Lulu ulikuwa ukionekana kabisa. Kitambaa cha vazi hilo kilikuwa kama kioo. Ungeweza kuona ndani bila taabu hata kidogo. Umati mzima ulipiga kelele, na watu hawakuweza kuinua macho yao, maana kama unataka kujipatia taabu wewe mwangalie huyo mtoto kwenye jukwaa.

Kwa sababu mimi nilikuwa na mashaka sikuwa kipofu. Niliangaza huko na huko. Ghafla nikasikia mtu anaanguka nyuma yangu huku ameshikilia bastola karibu kufyatua. Watu hawakutambua maana kila mtu macho yake yalikuwa kwenye jukwaa. Nilipoangalia nyuma niliona mtu huyo amekufa kwa kupigwa risasi. Kabla sijakimbia toka hapo, na bado Lulu anavutia watu kwenye jukwaa. Sammy alipita na kuniangukia kijikaratasi. Niliangaza nione Benny alipo sikumwona. Kwa hiyo niliharakisha kutoka kwenye maiti hiyo na kukimbia hadi nilipoketi awali kabla ya mtu yeyote kunitambua.

Lulu alichukua muda mrefu kwenye jukwaa, hivyo alinipa muda wa kuweza kurudi na kukaa bila mtu kutambua. Kwani wakati huo Lulu bado anawapa watu wote moto kiasi cha kutojitambua.

Nilikaa na kusoma kikaratasi hicho. Utashangaa nikikueleza. Mtu huyo aliyepigwa risasi nyuma yangu nilidhani ni mmoja wa vijana wa Robin kumbe hapana. Huyo mtu alikuwa anakuja kuniua mimi. Maana walikuwa tayari wametambua kwamba nitakuwa nikichunguza mienendo ya Benny. Kwa hivyo walimkonyeza Benny. Naye Benny akapanga namna ya kuweza kunitupilia mbali. Mtindo wao waliotumia ni ule ule. Benny anampa ishara yule kijana wa kwenye jukwaa alafu kijana huyo anamtoa Lulu nje. Kisha Lulu anapofika kwenye jukwaa, anatia watu wote moto kiasi cha kutojitambua. Ndipo watu wa Benny wanapopata muda wa kuua mtu wao wanayemtaka bila kutambuliwa wakitumia bastola iliyo na kiwambo cha kuzima mlilo.

Mpango huo huo ndiyo uliotumika kwa kutaka kuniua. Lakini bahati nzuri Sammy alishikwa na mashaka. Wakati Lulu alipotokeza aliniona mimi nimekaa mahali wanapoweza kunidhulu vizuri sana. Kwa hiyo yeye aliweka macho yake yote kwangu. Kumbe alikuwa sawa. Jamaa mmoja alitokea kwenye mlango mmoja unaotokea chooni ili aje animalizie mbali. Basi alikuja taratibu. Alipofika karibu alitoa bastola ili kufyatua. Kumbe Sammy naye alikuwa ameishamtilia mashaka akamuwahi kabla ajafyatua. Alikufa papo hapo bila mtu yeyote kutambua na Sammy akapita mahala pangu na kunitupia hicho kikaratasi bila kutambulikana. Kisha tukaenda mahali petu bila kutambuliwa.

Benny aliingia kutoka nje wakati Lulu alipokuwa akitoka kwenye jukwaa akirudi kwenye chumba cha kubadilishia mavazi. Benny aliponiona alishtuka sana. Rangi yake ikambadilika. Nywele zikasimama na jasho likamtoka. Akaenda moja kwa moja upande wa chooni. Nilimwangalia kwa usili sana alipoiona hiyo maiti ya mtu wake, akajiuma vidole na kwenda zake kwenye kundi, ndipo watu wakaigundua maiti hiyo.

Polisi waliitwa mara moja kila mtu akaanza kuulizwa ulizwa. Mapolisi walianza kukagua waone iwapo alikuwapo mtu mwenye bastola. Siye tulifahamu kuwa jambo linaweza kutokea hivyo bastola zetu tulikuwa tumeshampa mmoja wa vijana wa Robin na alikuwa ametoroka nazo tayari.

Huyo kijana wa kwenye jukwaa alipoulizwa na polisi kama alimuona mtu upande huo, mara moja alinitaja mimi. Polisi walinijia kuniuliza.

“Wewe ni nani?”

“Mimi ni Joe Masanja, mwandishi wa habari za maonyesho ya mavazi toka Mwanza,” nilijibu.

“Kwa nini ulikuwa umesimama upande ule wakati maonyesho ya mavazi yakiendelea, na hali watu wengine wote walikuwa upande huu?”

“Mimi kama mwandishi wa habari, niko huru kusimama mahali popote ninapoona ni pazuri kuwezesha kutazama mambo yote na kuandika kwa ufasaha.”
Nilimwambia huku nikionyesha hasira kidogo.

“Je ulimuona mtu yeyote akipigwa risasi karibu na wewe?”

“Hapana.”

“Je, maiti hiyo ilikuwepo wakati ulipoenda kusimama pale?”

“Hapana.”

Walianza kunikagua na wakanikuta bila ya silaha yoyote. Yule kijana wa kwenye jukwaa alikuja akaulizwa kama aliniona nikiwa na mtu yeyote hapo pembeni, akasema hakuona.

“Je, ulirudi wakati gani mahali pako, yaani hapa ulipo sasa?” waliendelea kuuliza.

“Nilirudi baada ya kuandika mambo yangu ambayo nilikuwa nahitaji.”

“Kama dakika ngapi hivi zilizopita?”

“Sikutazama saa lakini ni wakati huyo msichana aliyeonyesha mtindo 'Love at night' alipokuwa akiingia tu kwenye jukwaa.”

Waliniacha wakaendelea na kuhoji watu wengine. Sammy alikuwa ameniponyesha tena, la sivyo ningalienda kumsalimia babu yangu huko ndani ya udongo.

Maonyesho yalifungwa mpaka kesho yake saa kumi. Hii niliona itatupa muda wa kufanya kazi kama wakichaa. Na niliapa lazima nimpate Benny na vikalagosi vyake kabla hajafaulu kunitupilia mbali. Maana mara mbili sasa ninaponea chupuchupu.

Watu walipokuwa wakitoka mimi nilikuwa nikimvizia huyo kijana wa kwenye jukwaa. Alipotoka tu nikamfuata. Huku nikimuacha Sammy na Robin waendeleo na uchunguzi mwingine. Huyo kijana aliingia kwenye gari na kuanza kuondoka. Alikuwa peke yake humo garini. Mimi nilichukua gari moja niliyokuwa nimefanya mipango na idara ya uchunguzi waniletee. Nilipotoka tu nikakuta kijana mmoja tayari ameileta hiyo gari. Gari hiyo ilikuwa ya aina ya 'Zephyr 6' ambayo hukimbia sana. Niliweka gari moto nikamfuata huyo kijana. Nilihakikisha kuwa sifuatwi, ila tu Peter ndiye alipita karibu yangu nikampungia mkono.

Huyo kijana aliendesha gari yake kuelekea pande za Pangani, kwa hiyo nami nilielekeza gari langu huko huko. Niliacha magari matatu hivi mbele yangu kusudi asije akawa na mashaka akiona gari linamfuata katika kila kona aliyokuwa amepita. Lakini nilihakikisha kuwa sitampoteza.

Tulipofika kwenye nyumba za ghorofa za Pangani, huyo kijana alikwenda mpaka kwenye nyumba moja ya ghorofa na kusimamisha gari lake na kutoka nje. Mimi nilihisi kwamba hapo ndipo alipokuwa akikaa. Saa hizo giza lilikuwa limeishaingia hivyo nami nikasimamisha gari langu katika sehemu moja, halafu nikaenda kumvizia huyo kijana. Alipanda mpaka ghorofa ya tatu. Akafungua mlango wa

chumba kimoja na kuingia ndani. Wakati huo mimi nilikuwa nimesimama hapo chini nikimwalia. Kisha na mimi nikapanda mpaka ghorofa ya tatu.

Ghorofa hiyo ilikuwa na vyumba vitatu, yaani jamii tatu zilikuwa zikiishi kwa kila mmoja. Nilipochunguza, niliona kuwa watu katika vyumba vingine hawakuwemo. Watakuja wakati gani, hiyo haikuwa shida yangu wakati huo. Nilichungulia kwenye chumba cha huyo kijana nikamuona akiwa amekaa kwenye sofa hali akivuta sigara. Alionekana bayana kwamba hakuwa na furaha hata kidogo.

Nilibisha kwenye mlango, na nilipokuwa nikifanya hivyo, nilikuwa nikimchungulia kwa dirishani. Kabla hajaja mlangoni akaonekana kubabaika sana hata sigara kumdondoka toka mdomoni. Alijiachia huku na huku kisha akafungua kabati lake la nguo. Akapapasa katika mfuko wa koti moja na kutoa bastola! Ndipo akaja mlangoni kunifungulia huku ameshika bastola hiyo mkononi. Naona hata yeye alikuwa akihisi kuwa lazima lilikuwepo jambo.

Alipofungua mlango tu nikaupiga teke mkono wake uliokuwa umeshikilia bastola. Bastola hiyo ikaanguka kama hatua tatu hivi upande mwingine wa chumba. Nilikuwa nimeishotoa bastola yangu na kuiweka tayari mkononi. Alitaka kupiga kelele, lakini nikamuonyesha bastola, kwa hiyo akafunga akanyamaza.

“Funga hilo domo lako, la sivyo ukilipanua tu, risasi zote zitamalizikia ndani yako.”

“Jina lako nani?” Wakati huo nikimuuliza tumeishaingia ndani na huku nimefunga mlango. Nilipomuuliza hakujibu. Kufumba na kufumbua wakati nikigeuza kidogo macho yangu upande mwingine akaipiga teke bastola yangu. Nayo ikaanguka mahala pengine. Hapo hapo akanitia ngumi moja mpaka nikaanguka chini.

Nilipokuwa nikiribu kusimama, akanitia nyingine, mpaka chini. Kweli huyu kijana, anajua kuzipiga, maana ngumi zake zinatoka mfululizo kama nini. Alipogeuka kuchukua bastola nilijikunja na kumpiga 'Farasi teke' mgongoni mpaka akaanguka chini. Nilisimama upesi upesi, na kabla yeye hajasimama nilimtia teke moja la usoni mpaka akaona nyota na kuzirai.

Nilimwendea hapo chini na kumsukumasukuma. Kisha nikaiendea bastola yangu na kumsogelea. Alipoanza kupata fahamu nilianza kumuuliza tena.

“Jina lako ni nani?”

“Naitwa James, na wapenzi wangu huniita Jim, lakini wewe sitaki uniite Jim maana ni adui yangu. Tangu nizaliwe sijapigwa na mtu namna ulivyonipiga wewe kwa hivyo niite James, koroboi we.”

“Unamfahamu Benny?”

“Ndiyo”

“Tangu lini”

“Kwa muda wa mwezi hivi.”

“Kwani umekaa hapa Nairobi kwa muda gani?”

“Yapata miaka kumi sasa.”

“Na kama Benny pia anakaa humu humu mjini mbona mlikuwa muda wote hamjafahamiana?”

“Kwani wewe unajua watu wote wa Mwanza?” alinijibu kwa jeuri sana.

“Nani amekuambia natoka Mwanza?”

“Lulu na Benny”

“Kwa nini ulimbadilisha Lulu kutoka kwenye jukwaa kabla ya zamu yake?”

“Hiyo ni kazi yangu si yako. Unataka nini?” alisema kwa wasiwasi hali akitazama dirishani.”

“Nilipotupa macho nyuma kuangalia mlango ulifunguliwa na kijana mwingine akaingia ndani huku ameshikilia bastola mkononi. Nilijipindua mara moja na kumweka James juu yangu. Kisha nikasimama naye huku nimemfanya ngao yangu.

“Eh, kumbe una akili za kutosha.” alisema huku sauti yake ikigundagunda.

“Jaribu, na kabla ujaniua mimi utakuwa umemuua James kwanza. Si ajabu hiyo?”

“James hana thamani sana akifa zaidi ya kifo chako. Kilivyo na thamani!” alijibu huku uso wake umekunjamana.

Ghafla nilimsukuma James na kumwangukia mwenzake na hapo wote wakaanguka chini. Kabla hawajasimama nilipiga teke mkono ulioshikilia bastola. Kisha nikaanza kuwapa kazi. Kijana huyo aliposimama nilimpiga kichwa mpaka chini. James akatupa ngumi lakini nikaepa. Nilimtia kichwa mpaka akatabawali. Maana

alikuwa bado na maumivu ya magigano ya kwanza. Huyu kijana akabeba kiti na kunitupia lakini nikawahi kukidaka. Nilimtwanga kwa kiti hicho kichwani na kumfanya apepeseke mpaka ukutani. James alikuwa hawezi kusimama sasa ila kubaki akikoroma tu. Kijana huyo mwingine akaniwahi kwa ngumi moja kwenye shavu. Loo! mikono yake ni kama chuma, jino langu moja likanitoka. Hasira zilivyonipanda Mungu ndiye ajuaye. Maana sijawahi kupingwa ngumi mpaka jino likatoka. Kutokana na hiyo hasira nikamtia ngumi tatu mfululizo. naye akawa kama James.

Kwa bahati nikaiona kamba hapo ndani. Kabla hawajapata fahamu, niliwafunga pamoja kwa ustadi sana kisha nikafuata maji ya barafu na kuwamwagia. Walipopata fahamu nilivuta kiti nikakaa huku nimeshikilia bastola yangu mkononi.

Tuue basi unangoja nini?” alisema huyo kijana mwingine.

“Nitauaje watu waliokwisha kufa wenyewe?” nilijibu.

“Maana ya kutufunga hivi kama magunia ya kauzu ni nini?” aliuliza James.

“Maana nimeona nyinyi ni watu hatari sana.”

“Sasa nadhani utajibu maswali yangu James maana utani sasa umekwisha. Jina langu ni Willy, Willy Gamba, wa Idara ya upelelezi ya Tanzania lakini ambayo inafanya kazi bega kwa bega na Idara za namna hii katika Afrika nzima.” niliposema jina langu, kila mtu alitoa macho ya woga.

“Kama ni Willy Gamba, nitajibu maswali yako yote, sina njia nyingine. Lo! Kunaonekana kuna makubwa hapa mjini mpaka wakakuleta wewe. Maana nimeishasoma habari nyingi juu yako na vituko vyako vyote. Sina njia, uliza tu. Niko chini ya miguu yako,” alijibu James.

“Mimi sikujua kama ni Willy na kama ningalijua nisingethubutu kukufuata.” alisema huyo kijana mwingine.

“Nani alikutuma kunifuata?” nilimuuliza.

“Benny, ndiye alinituma.”

“Kwa nini alikutuma kunivizia?”

“Alisema kuwa wewe unaonekana mwenye kuingilia mipango yake na hivyo lazima uuwawe mapema, kusudi mipange iweze kufanyika kesho usiku.”

“Mipango gani hiyo?”

“Sijui, na hakunieleza zaidi.”

“Wewe ni nani wake mpaka akutume kuniua.?”

“Mimi nimeanza kumfanyia kazi tangu juma lililopita, sababu najua kutumia bastola. Nimewahi kuwa jeshini kwa muda.”

“Alikwambia kwa nini anataka mtu kama wewe?”

“Ati kwa sababu yeye ana pesa nyingi.”

“Unamfhamu Lulu?”

“Ndiyo.”

“Ni nani?”

“Ni mpenzi wa Benny.”

“Tangu lini?”

“Sijui”

“Benny alipokuwa akikutuma Lulu alikuwepo?”

“Ndiyo”

“Lulu alisema nini juu yangu?”

“Naye alisema kama Benny tu, ila aliongezea kuwa lazima nikuendee vizuri maana unaonekana kuwa mtu mbaya sana.”

Kisha nilimgeukia James, “Jim mpenzi, jibu swali langu ambalo nilikuuliza kabla kikaragosi cha Benny akijatuingilia.”

“Hebu uliza tena”

“Kwa nini ulibadilisha wakati wa Lulu kuja kwenye jukwaa?”

“Kwa sababu niliona ishara toka kwa Benny.”

“Ishara gani uliona?”

“Alishika na kurekebisha tai yake.”

“Ulijuaje kuwa hiyo ni ishara ya kukuambia ubadilishe wakati wa Lulu kutoka?”

“Benny alikuwa ameniambia kuwa kuna watu wanaomtafuta, na yeye ni lazima awafutilie mbali kabla wao hawajafanya hivyo, na tena alisema kwamba

anashughuli zake ambazo anataka ziishe kabla ya kesho kutwa asubuhi. Hivyo akanipa pesa ili nimfanyie kama alivyokuwa akitaka. Ati kwa sababu Lulu alikuwa akichukua mawazo ya watu, aliona kuwa akitaka wauwawe wangeweza kuuawa bila watu kujua nani amewaua.”

“Kwa nini hukukataa?”

“Kwa sababu angeweza kuniua hata mimi, ndiyo alinitisha.”

“Ulimuona mtu aliyemuua yule mtu aliyekufa pale ukumbini.”

“Hapana sikumuona, lakini nilifikiria wewe unajua.”

“Kwa nini ulichukua bastola nilipogonga mlangoni.”

“Kwa sababu nilikuwa na wasiwasi juu ya mambo niliyokuwa nimeambiwa na Benny.”

“Huwa unakaa na bastola hapa kwako, ama umepewa leo tu kuitumia.?”

“Nilipewa na Benny niitumie iwapo nitaifuatwa na mtu yeyote.”

“Kuna mtu mwingine yeyote anayeshirikiana na Benny?”

“Sijui hajaniambia lakini nafikilia huenda yupo, maana baada ya Lulu kuingia kwenye jukwaa leo, Benny alienda kupiga simu.”

“Kuna watu wangapi waliotumia hiyo simu leo tulipokuwa kwenye maonyesho?”

“Ni Benny tu niliyemuona”

“Nambari ya simu aliyotumia Benny ni ngapi?”

“Una maana alikokuwa akipiga ama ile aliyokuwa anatumia?”

“Nina maana zote.”

“Alikokuwa akipiga sijui, lakini ya mle mwenye 'hall' ni 21899.”

Niliwambia wafunge midomo yao, mpaka baada ya siku mbili hivi. Nilionelea niwaache hivyo ningemwambia Robin aje awachukue awaweke ndani kwa siku mbili hivi.”

“Haya wajomba, kama mnataka usalama fanyeni kama nilivyowaambia, na ujanja wowote, mnaweza kujikuta mko ndani zaidi. Na ndipo mtalia na kusaga meno.” Niliondoka nikawapigia Sammy na Robin simu. Nilimweleza Robin juu ya hawa watu na jinsi ya kuwafanya. Akasema angefanya kama nilivyomwambia. Na pia

akanieleza anahisi kupata fununu ya jambo fulani kwa hiyo lazima nimwone asubuhi hotelini kwake mnamo saa tatu hivi. Pia nilimweleza kuwa sasa naenda kumwona Lulu na nikamwambia Sammy apige huko hotelini kwa Lulu simu itimiapo saa nne hivi. Na kwamba ikifika saa nne na nusu bila ya kuniona aje huko hotelini kwa Lulu, huenda nitakuwa nimo msambweni.

Nilipiga simu kwenye Idara ya Uchunguzi nikawaeleza wanitafutie nambari za simu ambako simu ilipigwa kutoka kwenye simu nambari 21899 mnamo saa kumi na mbili na nusu. Na wakasema hiyo ni kazi rahisi. Pia niliwaambia wanipe jina la mtu mwenye simu hiyo, wakasema pia kuwa hilo lisinitie shida ni kazi ndogo.

SURA YA SITA

HATIMAYE niliondoka kwenda Intercontinental Hotel. Nilipokuwa naingia nilimkuta Peter na Wazungu fulani fulani pamoja na wapigania uhuru wengine wakinywa kahawa katika chumba cha kahawa. Aliponipungia mkono nikaenda kuwasalimu. Nilikuta Wazungu wote hao walikuwa Marekani na walikuwa wanatoka katika Baraza la Umoja wa Mataifa, kwenye sehemu inayoshughulika na Afrika Kusini. Ilionekana walikuwa wamekuja kwa mazungumzo na wapigania uhuru.

Walininunulia kahawa, baadaye Peter na hao wageni wake iliwabidi waondoke wakalale maana walikuwa wamechoka. Nilimwuliza Peter kama amemwona Lulu, akasema alimwona akiingia ndani, lakini hajatoka nje. Pia nilimwuliza kama kuna mtu mwingine yeyote aliyekuwa ameingia na Lulu, akasema hakumwona yeyote. Basi tuliagana wao wakaenda zao miye Willy, nikakaza roho kupanda chumbani kwa Lulu.

Vijana wa Robin walikuwa wameishapata hata nambari za chumba cha Lulu. Nilienda moja kwa moja mpaka kwenye kile chumba. Lakini kwanza nilihakikisha hakuna mtu aliyeniona huko juu.

Hoteli Intercontinental ni nzuri sana na ghali. Na kama wee ni 'giriki' nusunusu huwezi, na msichana Lulu anatisha maana mtu wa kukaa katika hoteli hiyo lazima awe 'giriki'hasa. Hiyo ninaweza kusema kwamba Lulu ni 'giriki' hasa, ila sivyo asingeweza. Maana wanawake wengine wote wa kwenye maonyesho hata waliotoka ng'ambo ni yeye tu anayekaa hapa. Na kama kuna mtu aliyempangishia, lazima huyo mtu awe na pesa si mchezo. Na hii nadhani ndiyo ilikuwa kweli hasa, maana Lulu alikuwa msichana mrembo hasa. Mtu yeyote mwenye fedha angemfanyia lolote analotaka. Ninaamini kwamba, Lulu akikuambia wende ukamwibie fedha ili awe wako, Wallah utakubali ufungwe ikiwa utashikwa, lakini ukaibe.

Nilitelemka taratibu kabisa mpaka chini. Hapo chini sikumkuta mtu yeyote, licha ya Sammy niliyetegemea kumuona. Niliingia katika gari yangu mpaka hotelini kwa Sammy. Nilimkuta Sammy akisoma gazeti liitwalo. 'The Detective' nilimweleza mambo yote niliyoyapata kutoka kwa Lulu

Sasa tulianza kuelewa mambo yote yalivyo, “Inaonekana Lulu ameingizwa katika mpango huu kusudi amsaidie Benny katika mambo fulani fulani. Mojawapo likiwa kama yale aliyokuwa akiyafanya maonyeshoni. Laiti isingekuwa sababu kama hiyo basi Benny asingefanya mapenzi na kupoteza fedha nyingi kwa Lulu. Pia tulianza kutambua kuwa Benny siye 'Bosi' ila 'Bosi' mwenyewe yupo', na Benny ndiye msaidizi wake.

Hivyo zile karatasi anazo 'Boss'. Na anayemjua huyo 'bosi' ni Benny peke yake wengine wanadhani 'Bosi' ni Benny.

Kwa hiyo kazi kubwa sasa ni kutafuta kwa kila njia tumjue huyo 'bosi' ni nani. Na kwa kufuatana na habari nilizozipata kwa James, hizo karatasi zitabadilishwa kesho usiku.

Jambo jingine ambalo lazima tuchunguze ni mahali ambapo mabadilishano ya karatasi hizo yangefanyika. Kwa kuwa wamekwishajua kuwa tunafanya kazi juu ya jambo hili, wanaweza wakaharakisha mambo zaidi na wakazibadilisha hizo karatasi haraka iwezekanavyo. Kwa hiyo nasi inatubidi tufanye kazi haraka kusudi tuweze kuzipata hizo karatasi kabla ya wao kuwapa hao watu, na kabla hawajalipwa.

Haya ndiyo mawzo yangu niliyokuwa nayo. Sammy pia alionekana kuwa na mawazo kama hayo. Tulimpigia Robin simu, tulimweleza juu ya mambo yote tuliyokuwa tunafikiri. Robin alisema, “Ninaona mawazo yenu ni sawa. Walakini inafaa mnipe wasaa maana mimi na vijana wangu tunaanza kupata fununu ya jambo fulani.”

Sammy alitoa wazo kuwa yeye ataenda kuchunguza katika ile nyumba ya Benny kama anaweza kupata habari yeyote, kusudi mimi anipe nafasi nilale. Lakini mimi sikukubaliana naye niliona miye ndiye niende, na yeye akiona sirudi, anaweza kuja kunitazama huko. Maana kila siku tunapokuwa tukifanya kazi na Sammy, miye huenda kwanza tukijua ni mahala penye hatari na yeye huja nyuma. Na mara nyingi hii imefanya kuokoa maisha yetu.

Sammy alisisitiza kuwa, kwenda kule peke yangu kunaweza kuwa na maana ya kifo, kwa hiyo ni afadhali twende sote pamoja. Lakini bado niliona hili si sahihi. Mwishowe alikubaliana nami kuwa mimi niende kwanza halafu yeye aje baadaye, baada ya muda kama wa saa moja hivi.

Nilirudi hotelini kwangu nikabadilisha nguo. Mara hii nilichukua bastola mbili, moja ile yangu ya kawaida, '45 automatic' na ya pili ndogo kiasi cha kalamu ya wino. Hii ya pili niliisukuma kwenye mkunjo wa chupi niliyovaa.

Halafu nikanywa bilauli moja ya maji na whisky. Kisha nikaandika kijikaratasi cha kumwachia Lina, maana nilikuwa namtegemea usiku ule saa sita. Alikuwa amenipigia simu kuwa huenda angalikuwa na jambo kamili ambalo lingeliweza kunisaidia, wakati huo. Ghafla nikajiwa na wazo nimpigie Lina simu, nimweleze kuwa sintokuwepo ila nitaenda kufanya uchunguzi kwenye nyumba ya Benny.

Hii ingenisaidia mambo fulani fulani. Kwanza kama nikimpigia simu Lina, na kama Lina ananicheza yuko upande wa Benyy nitakuta Benny yuko tayari ananingojea maana Lina atamweleza hizi habari. Pili Lina amewahi kuwa mpenzi wa Benny kwa hiyo anafahamu kila kona ya kile chumba. Kwa hiyo anaweza kunipa muhtasari wa jinsi nyumba ilivyojengwa na jinsi vyumba vilivyokaa na hakuna uwezekano wa kufichwa vitu vya siri. Mwanamke..... japo siku moja tu ukikaa naye atakuwa amejua wapi hutaki aende na wapi unataka aende. Basi nilimpigia simu Lina.

“Hallo huyu ni Willy, habari Lina?”

“Salama tu Willy, mbona unanipigia simu na hali nimekwambia nitakuja? maana mpaka sasa nangojea simu toka mahali fulani ambayo inaweza kukusaidia sana.”

“Oh. unafanya kazi vizuri kabisa Lina. Sababu ya kukupigia simu ni kwamba ninatoka. Naenda kufanya uchunguzi kwenye nyumba ya Benny, kwa hivyo nilitaka unipe muhtasari wa nyumba ilivyokaa, na jinsi ninavyoweza kuingia ndani kwa usalama bila kuzuiliwa.”

“Lakini Willy, maahala hapo ni pa hatari sana. Mimi nilipopita karibu na mahali hapo niliona baada ya kuchunguza sana kuwa pamejaa walinzi. Na wote wako tayari kuua mtu yeyote atakayeenda hapo. Miye nilifanya uchunguzi huo nilikuwa huko 'Sclaters hosteli' na niliambiwa hivyo na msichana fulani ambaye ni shemeji ya Benny. Aliniambia kuwa Benny alikuwa amemwambia asiende pale leo maana pana hatari. Na kuwa ingekuwa salama kwake kama angebaki hostelini. Kwa hivyo mimi naona usiende, utahatarisha maisha yako bure tu, tafadhali.”

“Hapana Lina, lazima niende. Na wewe njoo kwenye chumba changu ifikapo saa sita hivi. Nadhani bado una ufunguo niliokupa. Wakati huo nina uhakika kuwa nitakuwa nimerudi. Na kama nitakuwa sijarudi jua basi kumetendeka jambo. Sasa nipe huo muhtasari basi.”

“Sikiliza Willy, nyumba yenyewe ina vyumba vitano sebule ya sita; choo, bafu na jiko. Vyumba vya kulala vine. Kile cha sita ni namna ya maktaba, maana huwa mna vitabu vingi sana na wageni hawaruhusiwi kuingia humo maana ndipo anatunzia bastola zake na hata za rafiki zake. Nyumba hiyo ina milango mitatu ya nje. Mmoja nyuma kutokea kwa 'Nakuru road'. Upande usio na mlango ni ule wa kulia, ambao unapakana na 'Scrates hosteli,' ila una dirisha moja kubwa la kutosha mtu kuingia kwa dirishani.

Unapoingia utaangukia ndani, utakuwa katika chumba kimoja cha kulala lakini hakina mtu sasa, maana yule shemeji yake ndiye alikuwa akilala humo. Vyumba vyote vya nyuma ni vya kulala. Benny analala kwenye chumba kinachofuata hicho chenye dirisha, mkono wa kushoto wa hicho. Chumba kinachotazamana na mlango wa mbele ukiwa sebuleni, ndicho hicho nilichokueleza, kinachotumiwa kama maktaba. Unataka nikueleze nini tena mpenzi!”

“Hayo yanatosha Lina, asante sana. Kama nikirudi salama ndipo nitaweza kutoa shukrani kwa udhati mbele yako. Hapana shaka tutaonana. Kwa heri mpaka hapo.” nilijitengeneza sawasawa, mara hii nilionekana kama mpelelezi haswa mwenye cheti cha kuua.

Nilitoka nje nikaingia ndani ya gari yangu, nikaelekea Westlands. Nilipokuwa ninaenda niliona gari kama mbili zinanifuata kila ninapopita. Nilipofika karibu na 'Klabu 1900' nilisimama. Hizo gari mbili zilikuja zikanipita. Nilipoangalia nikagundua kuwa katika gari la mbele mlikuwa na vijana wawili ambao niliwaacha chumbani kwa Lulu na Benny. Katika gari la nyuma mlikuwa na yule kijana niliyemrudisha wakati akitufuata nilipokuwa na Lina katika gari lake. Nao walienda wakasimama mbele yangu.

Niliwasha gari langu moto nikaenda kulisimamisha na magari mengine hapo klabu 1900. Halafu nikangoja, wale jamaa nao wakaja wakasimamisha magari yao hapo nje kisha wote wakatoka na kuingia klabu 1900. Walidhani mimi nimetoka na kuingia humo, maana nilipokuwa nikizimisha gari langu kijana mmoja naye ndiyo kwanza anawasili hapo, alitoka katika gari lake na kuingia ndani. Alikuwa amevaa koti kama langu, na ni mrefu kama mimi, kwa hiyo walidhani ni mimi. Kisha nilitoka katika gari langu, nikaenda kwenye magari yao, nikapiga risasi magurudumu yote manne ya kila gari, yakawa hayana kazi alafu nikaenda katika hiyo klabu ambamo niliwakuta wote watatu wamekaa huku wakiangaza macho huku na huku. Nilienda nikakaa kwenye meza moja nao alafu nikawaambia,”Tafadhalini wazee, mimi sitaki kufuatwa fuatwa, na kama mkizidi

mtaona cha mtema kuni. Mimi nilikuwa nikija hapa kunywa na nyie mnanifuata tu. Sasa nitawaacha hapa, na ninarudi kunywa mjini, na yeyote atakayenifuata nitamwadhiri vibaya sana.” kabla hawajajibu niliondoka na kurudi kwenye gari langu. Nililitia moto na kuondoka halafu nikaenda kusimama hatua chache nione kama watatoka.

Kitambo walitoka, na kuingia katika gari zao. Walipowasha wakakuta magurudumu hayana upepo yote. Walitoka na kuanza kuzungumza. Miye Willy nikaweka gari langu moto, kuendelea na safari yangu.

Niliondoka hapo kwa mwendo mkali mno. Nilipofika kwenye ile nyumba nikapunguza mwendo. Nikasimamisha gari mbele ya Sclaters hosteli karibu na miti. Hlafu nilianza kurudi kwa miguu, taratibu. Nilikuwa nimeacha koti langu katika gari, halafu nikavaa kijambakoti, ambacho kinanifanya mwepesi zaidi.

Nilienda nikavuka Sclaters hosteli kisha nikaangaza macho yangu mbele ya nyumba hiyo nikaona watu wawili wakizungukazunguka hapo mbele. nikaenda kuchungulia upande wa nyuma pia nikaona kuna walinzi, kama Lina alivyosema. Nyumba yote ilikuwa giza maana hamkuwa na mwangaza hata sebleni. Basi nilikata shauri nifanye kama Lina alivyosema Hapo nikaanza kumsifia Lina kwamba yu mwenye akili hasa. Na kwamba angefaa sana kufanywa mpelelezi.

Nilienda nikaruka seng'enge, nikawa nimeisha anguka ndani ya seng'enge. Lakini mmoja wao alisikia namna ya kishindo kwa hiyo akaja upande ule wangu. Nilijibanza kwenye ukuta. Aliposogea karibu nikamtupia kisu shingoni. Hatimaye mtu huyo alikufa bila mtu kujua.

Nilipanda mara moja kwenye ukuta, nikakwea taratibu bila kufanya kelele yeyote, mpaka nikashika kwenye dirisha. Hlafu nikatoa tochi yangu na kumulika ndani ya chumba. Nikaona kulikuwa kumelala mtu kwenye kitanda huku ameshikilia bastola mkononi alikuwa amesinzia. Alionekana kana kwamba anataka kuamka lakini kabla ajaamka nilimtia kisu shingoni pia. Akawa hoi bila kutoa sauti. nikaanguka kwenye kitanda bila sauti kutoka kwenye dirisha.

Mlango wa hicho chumba ulikuwa umefunguliwa, kwa hiyo nilitoka nje ya chumba hicho bila kufanya kelele hata kidogo. Nilijaribu mlango wa pili yake ambao Lina alisema ndimo Benny alikuwa akilala, nikakuta umefungwa. Nilichukua funguo yangu malaya nikafungua, nilipopiga tochi mle ndani nikakuta hakuwemo mtu. nilienda kwenye kimeza cha karibu na kitanda, nikaanza kutafutatafuta vijikaratasi vyovyote vya maana lakini sikuona. Ila nilipata karatasi

moja ya simu imeandikwa kwa kimombo. 'TELL THE BOSS TO MAKE SURE IT WON'T BE LATER THAN TUESDAY AT 10:00 P.M BECAUSE WE ARE EXPECTING THEM TO LEAVE THAT NIGHT AND BE HERE THE NEXT MORNING.' Fasili yake kwa kiswahili 'umwambie 'Bosi' kuhakikisha kuwa Haitazidi Jumanne saa nne usiku, maana tunawategemea kuondoka usiku huo na wawe hapa asubuhi ifuatayo”

Nilitoka kwenye hicho chumba na kufungua mlango nyuma yangu kisha nikaharakisha kwenda sebleni, kutafuta mlango wa maktaba. Maana nilikuwa nafikiRi kama Lina alikuwa anasema kweli, basi huenda humo ndimo mngepatikana mengi.

Niliingia sebuleni, bahati mbaya nikajigonga kwenye kiti: Yule kijana aliyekuwa mbele ya nyumba alishtuka. Niliweza kumuona sababu mlango ulikuwa wa vioo. Alikaa kidogo huku anaangaza macho ndani, nadhani kwamba alifikiri alikuwa yule mwenzake aliyekuwa amelala mle chumbani, lakini mwishowe alikata shauri ahakikishe, kwa hiyo alifungua mlango.

Mimi nilijibanza kwenye ukuta, alipoingia na kutaka kuwasha taa, nilimmulika na tochi machoni na hapo hapo nikatupa kisu, kikapambana naye kifuani. Kumbe na yeye alikuwa amefyatua bastola yake, na wakati alipoanguka tu, bastola yake ikafyatuka na kutoa sauti.

Wale walinzi wawili wa nyuma, walikimbia kwenye mlango wa mbele. Miye nilikuwa tayari nimekwishajibanza na bastola yangu nikiwangoja. Nilisimama kwenye 'swichi' ya taa kusudi wasije wakawahi kuwasha taa. Walipoangalia nje bila kuona lolote, walifungua mlango na kuingia ndani. Mmoja aliyekuwa mbele alitaka kuwasha taa hapo hapo nikaziachia risasi. Bastola yangu ilikuwa na kiwambo kwa hiyo haikutoa sauti. Yule wa nyuma akiwa bado anashangaa pia alizipata risasi.

Mara hii sikuwa na mchezo, madhihaka yote yalikuwa yamekwisha. Nilikuwa nimeishawachukia hawa watu kama kufa, hasa kwa sababu ya mauaji ya John. Kwa hiyo hata mimi sikuwa na huruma hata kidogo. Inaonekana kulikuwa na walinzi kama watano hivi na wote nilikuwa nimewafyeka kabisa.

Nilipiga tochi yangu sebleni, alafu nikakimbia kwenye mlango wa maktaba nikafungua na funguo zangu malaya. Nikaingia ndani halafu nikajifungua na kuanza kupekuapekua. Mlikuwa na vitabu vingi sana. Mlikuwa na masanduku ya vyuma yote yakiwa yamejaa vitabu. Nilifungua kabati moja la chuma, nikaona

mlikuwa na bastola kadhaa pamoja na risasi. Pia niliona bahasha moja ambayo ndani yake mlikuwa na barua. Juu yake ilikuwa imeandikwa Dr. Dickisoni Njoroge.

Nikiwa bado naendelea na upekuzi wangu bila kufanikiwa kupata chochote nilichokuwa nikikitaka, nilisikia mlango wa maktana unafunguliwa. Zilikuwa zimepita dakika kumi. Na nilikuwa nimeweka dakika kumi na tano tu kuwa kwenye nyumba hiyo, kwa hivi zilikuwa zimebaki dakika tano. Na Benny alikuwa ameisha niwahi kabla sijaondoka.

Nilijificha nyuma ya kabati hilo la chuma. Alipofungua aliwasha taa, hakuwa Benny ila kijana mwingine. Aliangaza huku na huko bila kuniona. Lakini mwishowe niliona akija upande wangu. Nilitoa kisu changu, kabla hajageuka, nikampata mgongoni, akaanguka bila hata yowe! Nilikimbia mlangoni. Nikaangaza sebuleni ambamo sasa taa zilikuwa. Sikuona mtu, nikakimbia mpaka kwenye mlango wa mbele, kabla sijatoka nje, nilipigwa kichwani mpaka chini.

Nilipozinduka nilijikuta nimefungwa kitini! Karibu yangu alikuwa Sammy pia amefungiwa kitini huku bado amezimia! Benny na Lulu walikuwa wamesimama karibu nami huku wakionekana na furaha sana.

“Naamini muda huu huna ujanja Willy, ninakuhurumia sana, maana kifo chako pamoja na rafiki yako kitakuwa kibaya na cha maumivu sana. Nami nitahakikisha kuwa mmekufa kwa taabu maana nyie mnaonekana watu wa ajabu sana, kumbe mambo yote waliyoandika juu yako ni kweli”.

“Wewe umeniingiza hasara sana ya watu wangu, maana umeua sita, na huyu rafiki yako ameua watano wakati akijaribu kuja kukuokoa lakini na yeye ameangukia kwenye mkasa huo huo.” Alisema kwa kujivuna sana.

“Sasa unadhani utafaulu kwenye mipango yako eti?”

“Kwanini nisifaulu, mpaka sasa yote yamekwisha kamilika, ila wewe tu na huyu rafiki yako ndiyo mlikuwa mnanipa taabu, lakini sasa hamtanipa taabu tena. Na sasa watu wangu wote watafanya sikukuu wakisikia wewe, John, na huyu anayelitwa Sammy amekufa”.

“Umefahamje kuwa huyu ni Sammy?”

“Lo! Wewe ndiye umechelewa kweli, nimekwambia saa zile kuwa kikundi chetu hata polisi wenyewe wamo. Nitashindwaje kujua basi. Nyie kila siku mnadhani ndiye wenye kujua habari nyingi, lakini mimi nina habari nyingi zaidi yenu, na

ninatumia akili zangu zaidi yenu nyie. Na pia nahakikisha kuwa sifanyi kosa hata moja”.

“Hii mipango mmeianza lini, na nani aliwasaidia katika jambo hili maana nyinyi msingelijua wapi pa uhakika ziliwekwa hizo karatasi?”

“Bosi' aliniambia kwamba nisiwaeleze jambo lolote mpaka amri itakapotoka kwake, lakini kwa sababu miye sitaki kuwaona mnaishi tena, nimeleta madebe mawili ya 'Petrol' na vijana wangu watawamwagia na kuwawasha moto mpaka mtakapokuwa mmeungua na kubaki majivu.”

“Unafurahi, kuchoma watu eh Benny, lakini kabla sijamalizika kabisa wakati nikiungua na wewe utakuwa umekufa.” Nilijibu kwa dhihaka.

“Uh, unadhani natania, Amani. Lete hayo madebe ya 'Petrol' pamoja na kiberiti,” aliita kwa hasira.

Wakati huo Sammy alikuwa ameisha zinduka akasema, “Wewe shetani mwanamke, siku moja nitakata kipande cha nyama katika mwili wako na kukifanyia sikukuu.”

“Nyamaza mwehu we, utaikataja nyama yangu na hali utakuwa umeisha kufa?” Alisema huku akitabasamu.

“Naona hapa tutakufa kama wanawake Willy, lakini hata hivyo huyu mwehu atashikwa na kutiwa ndani, nitafurahi sana kumpokea huko chini, na lazima nitahakikisha kuwa atapata taabu mpaka kupata makao,” alisema Sammy huku akionekana hajali lolote. Benny alitoa kicheko. Halafu akamwambia Aman atumwagie petrol.

Kabla hajamwaga Lulu alitoa oni, “Nadhani 'Bosi' atapenda kuwaona hawa washenzi wakiungua, kwa hiyo afadhali tumfuate aje ajionee hawa watu mashuhuri wa Serikali wakifa kitoto, na kifo cha aibu. Unaonaje Benny?”

“Lakini lazima tuache ulinzi wa kutosha hasa. Mlango wa nyuma weka walinzi watatu. Huu wa mbele watatu. Na wengine kuzunguka nyumba, halafu kwenye mlango wa chumba hiki watatu pia. Naamini hata kama angekuwa malaika hawezi kutoroka kwenye ulinzi wa namna hii.”

Wazo wako ni zuri sana Lulu. Nadhani 'Bosi' atafurahi ajabu na atatufanyia sikukuu. Lakini nyie wote angalieni kuwa hamfanyi kosa hata kidogo. Kosa lolote mshahara wake ni kifo cha namna hii hii.

Nilimuuliza mlinzi mmoja aliyekuwa akifunga mlango wa chumba tulichokuwa, “Itatachukua muda gani kwenda kwa 'Bosi' na kurudi?”

“Kama dakika kumi hivi”. alijibu na kisha akatufungia ndani. Halafu wakasimama pale mlangoni hali walinzi watatu wakiwa tayari na silaha zao.

Tulikuwa tumefungwa sana, hivyo kwamba hatukuweza hata kujitingisha. Walikuwa wametuvua nguo zetu zote isipokuwa chupi tu ajabu ni kwamba niliweza kusikia bado bastola yangu ndogo imo kwenye mikunjo ya chupi yangu. Jinsi ya kuitumia ilikuwa haifahamiki hata kidogo. Kuwa nayo na kutokuwa nayo yote yalikuwa mambo. Na pia tulijua tungefanya upuuzi wowote kabla Benbny, Lulu na 'Bosi' hawajarudi tungeliteswa na hawa walinzi.

“Mara hii hatuna ujanja kweli Sammy.”

“Hata mimi naona, maana sidhani kwamba kunaweza kuja mtu wa kutuokoa, na kama pia atakuja atakufa kabla hajafika humu ndani!”

“Mie nilikuwa siku zote natabiri kufa kwa risasi, maana pia nimeisha ua wengi kwa risasi”.

“Hakuna njia Willy, ila huenda mizimu ya mama Sammy ifanye kazi yake. Unakumbuka tulivyoona safari ile kule Lusaka?”

“Ndiyo, nakumbuka, lakini ulinzi pale haukuwa mkali kama huu wa hapa”.

Mawazo yangu yalirudi Dar es Salaam. Nilimfikiria mpenzi Della, moyo ukaniuma namna ya ajabu. Nilijua Della angeweza kujiua kama angesikia nimekufa. Nilimpenda naye alinipenda. Alikuwa msichana wa pekee yake aliyechukua moyo wangu na ambaye nilichukua moyo wake. Kisha nikamfikiria mama Willy. Lo! Mimi nilikuwa mtoto wake wa pekee. Hakuwa na mtoto mwingine hata mmoja. Mama Willy nilijua atakapoambiwa tu, ataanguka chini na kufa. Nilijua jinsi mama alivyokuwa akinipenda.

Nilionekana kama mawazo yangu si sawa. Nilikuwa katibu nipate kichaa kwa kufikiri mambo kama haya. Kisha nilimsikia Sammy akisema, “Nimesikia kitu kama mlilo wa bastola yenye kiwambo!”

“Unaota nini Sammy”.

“Hapana, kweli nimesikia.” Kisha nami nilisikia kishindo kwenye mlango kana kwamba watu wanaanguka.

Mwishowe nilimwambia Sammy kuwa huenda ni 'Bosi' anafika kwa hiyo watu wanamtotea njia.

Tulisikia mlango wa chumba ukifunguliwa. Moyo wangu uliruka kwani nilijua sasa mwisho wetu umefika. Maana “Bosi” amafika. Nilipomtaza Sammy niliona nywele zake zikisimama na rangi ilibadilika. “Wameisharudi! Alisema.

Mlango ulipofunguliwa tulishtuka kuona ni Lina ndiye anafungua mlango. Alikuwa ameshika bastola mbili mkononi. Akazitupa chini akaja kunifungua.

“Harakisheni tutoke hapa mapema kabla hawajarudi, maana nasikia watarudi mnamo dakika mbili au moja unusu hivi.”

SURA YA SABA

MIYE NA MSALITI

Tulirudi mpaka mjini tukiwa katika hilo gari la polisi. Tulipofika karibu na Pan Afrikani Hoteli, tulimwona daktari Njoroge akiwa ndiyo kwanza anarejea. Siye tuliendelea mpaka mjini. Yule kijana wa polisi alinishusha New Evenue Hoteli. Hapo nikaingia katika gari langu nililokuwa nimeliacha hapo nje ya hoteli. Nilitia moto gari langu na kuendesha mpaka Embassy hoteli.

Nilienda nikamuona Lina, maana nilikuwa nimemwambia asitoke mle ndani ya nyumba. Nilipogonga mlango kwenye chumba sikusikia sauti. Kwa wasiwasi nilifungua mlango taratibu. Nilikutana na tishio jingine, mara hii niliona lingeweza kuniua. Lina alikuwa ameanguka chini huku ametiwa visu, kimoja tumboni, na kingine ubavuni. Sura ya hapa mahala haikupendeza hata kidogo, miye Willy. Nililia kama mama anayemlilia mtoto wake wa pekee anapokufa. Lakini kulia kwangu si kwa kawaida, maana mimi ninapodiriki kulia wewe utakuwa umezimia. sili hovyoy.

Niliuangukia mwili wa Lina. Moyo ulikuwa bado unapiga, ingawaje yeye alionekana kama amekufa. Nilivitoa vile visu, damu ikaanza kububujika vibaya sana. Nilitoa vitambaa vyangu, nikaviweka kwenye matundu ya visu. Nilimwagia Lina maji kama anaweza, kabla hajafa kabisa anieleze neno lolote na kilichotokea. Sikuweza kufanikiwa, Lina alionekana hawezi kuziduka hata kidogo.

Nilipiga simu kwa Daktari aje mapema iwezekanavyo, ili akiweza amuokoe Lina ambaye moyo wake ulikuwa bado katika mapigo. Pia nilimpigia Sammy simu aje hapa mahala, lakini hakuweko. Niliacha ujumbe kuwa wakati wowote arejeapo aje huku chumbani kwangu.

Nilimbusu Lina ingawaje alionekana kama maiti. Yeyote aliyefanya jambo hili lazima awe mtu aliyejua kuwa Lina ndiye aliyetutorosha toka nyumbani kwa Benny. Kama unafikiri, unaweza kujionea mwenyewe mambo yanavyonyumbulika, maana tukio hili linaonekana la ajabu sana. Hapo hapo methali moja ya kiswahili ilinijia kichwani, “umudhaniaye siye, na usiyemdhania ndiye.” Sijui kama na wewe umeshaona na kukubaliana na tukio hili.

Daktari alikuja. Alipompima Lina, alisema kwamba bado ulikuwako uhai kidogo ndani yake, lakini hayakuwako matumaini makubwa. Hata hivyo alisema atamchukua Hospitalini kwake akajaribu kumsaidia. “Huyo huenda Mungu tu ndiye ataka aishi, la sivyo ameishakuwa marehemu, maana kisu cha ubavuni kimemchoma kwenye moyo.” alisema daktari.

Nilimuomba daktari amshtue kidogo kama anaweza, kusudi huenda naweza kupata kijijambo cha kunisaidia.

Alipomshtua Lina alitoa macho, kisha akafumba tena. Alijaribu kusema lakini akashindwa.

“Lina ebu niambie kimetokea nini?” nilimuuliza huku nikimtingisha, maana niliona anakufa tu, kwa hiyo afadhali nipate jambo linaloweza kunifanya nimpate muuaji wake.

“Alikuwa akanitishatisha, akaniuliza.....umekwenda wapi kisha akatoa visu akanichoma..... mimi nami niliwahi kumpiga risasi lakini hakuumia sana aha.....” Lina hakuweza kumaliza ila alizirai tena.

Daktari alimchukua kumpeleka hospitalini kwake na aliniambia angejaribu kila njia kuokoa maisha ya Lina. Na kama haitawezekana itakuwa sababu ya ahadi yake. Nilitoa shilingi mia tano nikampa daktari, na nilimuaidi kumpa nyingine elfu moja akiweza kuokoa maisha ya Lina.

Lina alikuwa amenipa pigo kubwa sana, moyo wangu ulipata kidonda ambacho Lina akifa hakitapona. Nilivyomuona Lina akiondoka na daktari! Basi tu. Mungu ndiye ajuaye, maana yeye na maiti yake hakukuwepo na tofauti.

Punde si punde Sammy alitokea. Nilimweleza mambo yaliyompata Lina, naye akasikitika sana. Ilionekana sasa tumebaki siye wawili tu kufanya kazi hii. Hii ilikuwa kwa sababu ya bahati tu, maana hata siye tumekuwa tukiponea chupuchupu. Hata hapa tulipokuwa tumekaa tukizungumza na Sammy tulikuwa na wasiwasi mwingi, maana wakati wowote tungeweza nasi kuwafuata rafiki zetu John na Robin na huenda dakika hii Lina.

“Sikiliza,” alisema Sammy “Tayari nimepata habari ndogo ndogo juu ya watu wanaohusika. Binafsi ninalishuku kundi lote lililotoka Ureno kuja kwenye maonyesho. Kwanza, wale wanawake wa Ureno waliokuwa wakionyesha mavazi walionekana kama kwamba si kazi yao ya kawaida. Pili, wamekuja vijana watatu pamoja na hao wanawake. Vijana hao tangu waje hawajaonekana hata kidogo ila tu

wameweza kuonekana hotelini kwao. Tatu, Robin alikuwa amepata habari kamili kuwa wao ndio ambao wamekuja kuchukua hizi karatasi kabla ya mauaji yake. Nne, kijana mmoja wa polisi ambaye tulimweka kumvia Benny, amesema kuwa Benny alienda mchana huo kama mara mbili hivi kukutana na hao waonyeshaji mavazi toka Ureno.

Hizi sababu za Sammy zipo katika usawa wa mia kwa mia. Kwa hivyo sasa lililopo ni kuhakikisha kuwa kwa njia nzuri ama mbaya siye ndiyo tunazichukua hizo karatasi badala yao.

“Je, yule kijana wa polisi aliyekuwa akimfuata Benny leo hii mchana, alisema lolote juu ya Benny kuja hapa Hotelini kwangu?” nilimuuliza Sammy.

“La, alisema Benny hakusogelea sehemu hizi maana alionekana mwenye shughuli nyingi sana.

Jibu hili lilinipa uhakika wa jambo fulani ambalo nitakapokwambia utastaajabu. Lililokuwepo sasa ni kuwatafuta Benny, Lulu na 'Bosi' kabla hawajafanya upuuzi mwingine wowowte, maana tusipowawahi sisi, wao watatuwahi.

Kabla hatujafanya jambo lingine lolote ilinibidi niandike ripoti kwa Chifu nikimweleza habari ya mambo yote yalivyo mpaka sasa. Maana sasa tumefikia karibu hatua ya mwisho na hii hatua ndiyo mbaya zaidi, maana kila kundi linapigania kushinda. Na hii ina maana ya vifo vingi sana. Nilimweleza Chifu mambo yote tangu mwanzo mpaka ambapo tumefikia, kisha nikaifunga na kuitia kwenye kisanduku changu cha barua za kutumwa.

Kisha nilivalia ili tuondoke. Tulijitayarisha kufa na kupona. Wote tulivalia furana ambazo risasi haziwezi kupita, 'bullet proof' kisha tukavalia juu kama kawaida. Hizi furana tulikuwa tumezipokea mchana huu toka kwa Chifu baada ya kumwomba wakati tunaona hatari zinazidi. Tulipokuwa tunataka kutoka simu ililia.

“Hallo, huyu ni Peter, wasemaje Willy.”

“Miye salama tu mheshimiwa, je una utenzi?”

“Ndiyo nina jambo la kukueleza, na ni la siri zaidi. Ni jambo la kuweza kukusaidia sana.”

“Niambie basi Peter mpenzi.”

“Hapana, kwenye simu mambo huwa si mazuri sana, kwa hiyo tafadhali njoo hapa.”

“Vema nakuja sasa hivi kama muda wa dakika kumi hivi.” Tulionelea tusiende wote kwa Peter ila Sammy aende kutalii kama Lulu yupo hapo Hotelini kwake. Na huko akamtishe ili aweze kutoa habari zozote. Kisha baada ya hapo Sammy angekuja hotelini kwa Peter, na hapo ndipo mahala ambapo tungekata jinsi ya kuendelea. Tuliagana tukatakiana bahati njema.

Nilienda zangu mpaka 'New Stanley Hoteli.' Nilipokuwa nikipita hapo chini, niliona jamaa wengi wakijiburudisha katika 'Thorn Tree. Lakini pia nilimuona kijana mmoja miongoni mwa hao watu ambaye aliponiona aliinama kidogo ili nisiweze kumfahamu. Lakini ilivyo macho yangu ni hatari, maana katika nusu nukta, nilikuwa nimeishaona kila mtu mwenye umati wa watu elfu moja. Huyu kijana nilimuona kule hotelini 'Intercontinental' wakati wamekuja na Benny huku wameshikilia bastola. Nilijifanya na mimi sikumuona nikaendelea zangu kumuona mheshimiwa Peter.

Nilipofika kwenye chumba cha Peter niligonga akanikaribisha ndani, “karibu Willy, asante sana kwa kufika!!” alisema akaenda kwenye kabati kuchukua vinywaji.

“Asante sana kwa kunikaribisha Peter, lakini miye sitaki vinywaji vyako maana nina kazi nyingi sana,” alikuwa bado akimimina pombe akidhani huenda natania kusema kuwa sitaki, “kwanza lazima nihakikishe kuwa nimewatia nguvuni waalifu wote na wengine kuwaua. Wewe ukiwa wa kwanza wa hao waalifu!” Peter ghafla alianguka chini chupa ya pombe akageuka kunitazama. Alipogeuka alikuta tayari nimeshatoa bastola mbili kumwanguka. Huenda nikadhaniwa mimi ni mkichaa, lakini la, kila siku nikisema neno au nikishuku neno jua niko sawa.

“Unamaanisha nini Willy, wewe unajua vema kuwa mimi ni mpigania uhuru halisi, na hasa nimepewa cheo kwa ajili ya uhaminifu wangu!” alisema huku akitetemeka kwa hofu.

“Ulidhani wewe ni mjanja sana Peter, yakwamba ungeweza kuuza wenzako bila kutambuliwa. Na kweli kidogo ungefaulu katika mambo yako, kama usingefanya makosa fulani fulani, na pia kwa sababu walimweka Willy katika kazi hii ambaye anashuku kila mtu. Hata pia nakusifu kwa akili zako nyingi, lakini nasikitika kwa kushindwa kwako.”

“Ulijuaje ya kuwa mimi nilikuwepo kwenye mpango huu?”

“Tangu siku ya kwanza niliyoondoka Dar es Salaam nilijua lazima kuwe na mtu ambaye kwanza ana cheo kikubwa sana kwenye Ofisi ya wapigania uhuru ambaye anashiriki katika tukio hilo.

“Kabla sijatoka Dar es Salaam nilienda nikakagua ile ofisi yenu iliyobomolewa, na ilionekana kuwa mle ndani vitu vingine vyote havikuguswa ila kabati lile lenye karatasi tu. Hii ilionyesha waziwazi kuwa lazima hawa watu wamepata habari kamili ya mahala karatasi hizo zilimo laasivyo tungekuta vitu vyote humo ndani vimevurugwa vurugwa kutafuta mahali zilipo hizo karatasi. Pia ilinipa wazo kuwa lazima awe afisa mwenye cheo kikubwa sana kujua hata mahala karatasi za siri kama hizo zilipotunzwa, maana afisa wa vivi hivi tu asingeweza kujua.

“Na kama unakumbuka siku ile usiku nilipokuwa nikienda kwa Chifu ulikuwa ukinifuata. Ulijifunga shuka na huku umevaa miwani myeusi. Gari lako halikuwa na nambari. Nilijua tu kuwa huyu mtu lazima ananifahamu ndiyo sababu anajibadili hivi.

“Wewe mwenyewe ulikuwa umekuja na hili kundi la akina Benny. Na baada ya kufanikiwa kuziiba hizo karatasi wao waliondoka wewe ukabaki Dar es Salaam. Ulibaki kwa sababu ulikuwa na wasiwasi ya kwamba wangeweza kuniweka mimi kwenye kazi hii. Hivyo ulivizia uone na ulikuwa sawa.

“Kisha ulinifuata Nairobi baada ya mimi tu kufika. Maana nilikuwa nimeweka mtu wa kuchunguza mpigania uhuru yeyote mwenye cheo ambaye angeingia Nairobi siku ile. Na wewe ulionekana ukitoka Dar es Salaam.” Wakati huo huo wote bado nilikuwa nimeshikilia bastola zangu tayari tayari, na Peter alionyesha mshangao wa ajabu machoni mwake.

“Ulipofika hapa.” Niliendelea, “Ulimuona John na kwa sababu mlikuwa mkifahamiana. John alikwambia kuwa alikuwa amekuja kwa tukio hilo. Hakusita kukueleza sababu kwamba anajua wewe ni afisa mkubwa sana katika ofisi ya wapigania uhuru. Uliripoti mambo hayo yote kwa Benny na Njoroge, na wao wakakuamuru umuue John. Ulifanya mpango ukamuua John.”

“Umejuaje kuwa Daktari Njoroge ndiye 'bosi'“ aliuliza.

“Hiyo ni rahisi. ngoja niendeleo kukueleza jinsi ambavyo wahalifu hawana akili, hali wakifikiri wana akili sana. Kisha ukamweleza Benny na Njoroge juu yangu - kuwa mimi pia ni hatari zaidi. Kwa hiyo jambo la kufanya ilikuwa wewe ukimbie upesi upesi kujifanya kuwa unatusaidia wakati unatuwinda.

“Wakati ninaenda kwa Lulu jana usiku nilikukuta 'Hotelini Intercontinental' na wageni fulani fulani, na ni wewe tu ulijua miye nimeenda humo. Ukaenda ukampigia Benny simu kuwa niko huko, akanifuata. Lakini mimi nilikuwa nimejua kitambo kuwa wewe utafanya jambo kama hili kwa hivi nikamwahi.

“Ulipomweleza Benny juu ya Lina akakuambia umtafute mpaka umempata uweze kumuua. Yeye hakutaka kufanya jambo kama hili maana kwanza alijua waziwazi kuwa Lina si mchezo, huwezi kumuendea hovy hovy. Pili alifikiri Lina anaweza kuwa yupo chumbani kwangu na kama kwa bahati mbaya angetukuta wote chumbani angejua maafa ambayo yangewapata.

“Lina naye aliwahi kukufyatulia risasi mkononi. Kuona hivyo ukakimbia kabla ya kuhakikisha sawasawa kama Lina amekufa ama vipi.” nilimwendea nikamvua shati lake, nikakuta kweli wamemfungafunga kwa vitambaa. Kisha nilijiegemeza kwenye ukuta huku nimeshikilia bastola zangu kama kawaida. “Halafu uliponipigia simu nje nikuone ndicho kilikuwa kifo changu na mimi, maana kuna watu ambao unajua watakuja humu wakati wowote. Wewe hukujua kama mimi najua, hivyo uliwaambia wakae kwa muda kidogo ili uweze kunipa pombe, na nisifikirie habari yoyote kusudi iwe rahisi kwenu kupambana nami. Lakini hapo ndipo ulipopiga chini hasa, maana Willy, alikuwa anajua kila kitu. Kwa hiyo nimekuja kwenye kifo chako si changu. Na nadhani taarifa nitakayoitoa kwa mkurugenzi wa wapigania uhuru itamfanya atoe machozi. Kwani kweli siye waafrika tunakulana kama samaki. Wahenga walisema kikulacho kimo nguoni mwako.” Na ni kweli kabisa.”

“Mh, kumbe unajidanganya sana Willy unadhani utatoka humu salama? wala usidhani kwamba wahalifu wanapofanya jambo kubwa kama hili huwa wanalifanya kwa pupa. Kwanza wanaambiana njia zote ambazo wanaweza kupita, na jinsi ya kuzuia pasiwepe na uwezekano wowote wa kuingiliwa.” Alisema Peter huku sasa amekaa kitini.”

“Wewe walikuahidi kukulipa kiasi gani Peter.”

“Lazima waliniaidi fedha nyingi laasivyo nisingelikubali kuhalibu jina langu na kuuza watu wangu.”

“Lakini kiasi gani hebu nipe jumla laasivyo naweza kugeuka mbogo sasa hivi, nikakutia marisasi maana unanijua waziwazi nilivyo.”

“Wangenilipan shilingi milioni kumi.”

“Na malipo yote ya hizo karatasi ni kiasi gani?”

“Ni shilingi milioni mia moja.”

‘Zimeishafika hapa toka Ureno?’

“Sijui kama zimefika,” alijibu huku akiwa na wasiwasi. niliachia risasi moja na kukipiga kiganja chake.

“Sema kweli, maana wewe, Benny na Daktari Njoroge ndiyo mnaojua ukamili wa habari hii.”

“Ndiyo imeishafika, ilifika jana usiku, lakini bado walioileta hawajatupa, watatupa leo usiku.”

“Watawapea wapi?”

“Kusema kweli hapo sijui,” alijibu kwa hofu tena. Nilimtia risasi nyingine ya mkono karibu na pale Lina alipokuwa amempiga.

“Wapi, niambie laasivyo utakufa.”

“Sijui kwa kweli, lakini nadhani itakuwa wakati wa maonyesho huko 'City hall'.”

“Hizo karatasi zimewekwa wapi?”

“Kule kwa” kabla hajamaliza usemi vijana wawili waliingia kupitia dirishani. Nilipogeuka kuwatazama, wengine wanne waliingia mlangoni. Peter alisimama na kukimbia kabatini alikotoa bastola na kuishikilia. Kisha wakaja vijana wengine wanne, wakawa kumi. wawili wengine wakaja lakini wakabaki

mlangoni mimi nilikuwa bado nimebaki nimesimama hivyo hivyo na huku bado nimeshikilia bastola zangu wote walikuwa wamejipanga upande mwingine wa ukuta wote wakiwa wameshikilia bastola zao.

“Tupa chini hizo bastola zako Willy, maana naona kifo chako kimefika,” alisema Peter kwa sauti ya ujuvi.

“Vipi, huwezi ukajihuzunikia mwenyewe, kabla mimi sijafa wewe mwenyewe utakuwa tayari umeishakufa. Ha ha ha ha, mbona nyie wapelelezi hamkubali kushindwa! Watu kumi na watatu na wewe mmoja bado unapanua domo lako. kuzungumza upuuzi mtupu. Wewe utakufa, miye nitapata fedha na hakuna atakayetambua kuwa miye Peter nilihusika na mambo haya.”

“Unajidanganya sana. Ukiniua mimi lazima Sammy atakupata tu.”

“Ohooo! Umechelewa sana rafiki yangu, Sammy ameishakamatwa huko chumbani kwa Lulu. Benny amemchukua huenda sasa ameishakuwa majivu,” alijibu mmojawapo wa wale watu.

Niliona kuwa huyu kijana hakuwa anatania. Nilikata shauri mara moja nipambane nao. Ikiwa nitakufa basi, lakini ikiwa nitapona nitahakikisha kuwa nimemponyesha Sammy nikimkuta bado hai.

“Fyatueni bastola zenu sasa mbona mnaogopa? mnaonekana mkitetemeka. Mkichelewa basi nitawamaliza miye kabla hamjanimaliza. Yaonyesha kwamba mnao uwoga wa kike,” nilisema hivi kusudi niwatie hasira, maana mtu akipatwa na hasira hawezi kuona sawasawa. Maneno yangu yalifanikiwa maana niliona wanapandwa na hasira hovy hovy.

Peter alitoa ishara huku akisema,

“Kwaheri Willy, nitahakikisha kuwa nimerithi mali yako yote hata Bella. Fika salama huko akhera.”

Walipotaka kuanza kunifyatulia risasi haraka nikawafyatulia mfululizo. Sita tayari chini. Niliipiga risasi mikono ya Peter akaanguka chini bila ya kuwa nayo bastola. Kisha nikawamaliza wale wanne waliobaki. Nilimsikia Peter akitoa sauti ya kuwaita wale wawili wa mlangoni. Walipokuja wakanikuta miye tayari nawangojea. Nikawafyatulia kisha nikawavutia ndani na kufunga mlango kisha nikamfuata Peter.

“Eh, umejua kuwa mimi ni Willy, eh Peter? Uhalifu haulipi. Na mshahara wa dhambi wa mauti bali karama ya Mungu ni uzima wa milele.”

“Oh Willy nisamehe, nilivutiwa na pesa. Oh nimetubu nimetubu.”

“Pesa, pesa Peter! Unakubali kuuza Afrika nzima kwa ajili ya pesa, ona sasa umepata nini ndani yake!

Peter alianza kulia.

“Zile karatasi ziko wapi?”

“Kule kwa Daktari Njoroge katika stoo yake. Zimewekwa katika sefu ya chuma humo stoo. Na watazibadilisha leo saa mbili na dakika kumi, lakini sielewi wapi.”

“Sasa Peter, kwaheri ya kuonana. Nitakupa risasi sita kwa sababu ndivyo nilivyoaidi nilipokuta John ameuawa. Nitakutia visu viwili kama kisasi kwa ajili ya msichana Lina kama nisingelikuwa nimeapa ningekurudisha Dar es Salaam wakakuweke kitanzi. Kwa heri kwa mara ya pili.”

“Ohoo nisamehe Willy.....”

Niliondoka mpaka kwenye mlango kisha nilimuendea na kumtia visu viwili hatimaye nikaachia risasi sita kama yeye alivyoziachia kwa John na kama alivyomchoma Lina.

Loh fulana yangu “buletproof” ilikuwa imeniokoa vizuri sana.

Niliondoka mle ndani haraka mpaka chini. Mawazo yangu sasa yalikuwa kwa Sammy, kwamba nitamkuta mzima ama vipi. Wameelekea upande gani sijui. Niliona nianzie kule kwa Lulu alikokwenda. Nilienda na gari langu mpaka hoteni kwa Lulu. Nilipanda mpaka kule chumbani kwa Lulu. MLango ulikuwa umefungwa. Nilipoingia ndani niliona kazi ya Sammy. Niliona Maiti nne zote zimekula visu.

Nilikaa kwenye kitanda nikifikiri wapi wamempeleka lakini sikuwa na mwangaza wowote. Nilizunguka huko na huko chumbani. Hofu, wasiwasi, uchungu, fikra, huzuni, vyote hivyo viliusukasuka moyo wangu, chuki na maudhi niliyokuwa nayo yangeweza kunifanya nizimie. Niliona karatasi kwenye kitanda. Nilipoiendea mwandiko haukuwa wa Sammy ila mtu mwingine. UPESI, NAIROBI SOUTH, WILISON AIRPORT, KABLA YA SAA MBILI KWENYE NYUMBA MOJA NAMBARI B 141. RANGI BLUE TAFADHALI UFANYE HARAKA LA SIVYO UTAJUTA KUCHELEWA KWAKO.”

'Lililo na mwanzo lina mwisho “Bosi”

Niliwaza harakaharaka kama huu ni mtego ama vipi. Lakini hata kama ni mtego niliona huenda unaweza kunisaidia. Sammy hakuwemo humo chumbani hivyo nikawaza kwamba pengine wanaye huko waliko au ameisha uawa na kutupwa mahala pengine. Zaidi niliona lazima wameenda naye huko waliko. Basi mwishowe nilikata shauri nifanye kama vile ilivyoelekezwa katika kile kikaratasi. Ilikuwa yapata saa moja kasorobo sasa.

Nilionelea katika hizo dakika kumi na tano nikimbie kule hotelini kwangu, nikaoge upesi upesi kisha nibadilishe mavazi maana shati langu lilikuwa limetobolewa tobolewa kwa risasi. Nilienda nikakoga haraka haraka, nikabadilisha shati na kuondoka zangu kuelekea Nairobi South.

Nilifika “Wilson Airporot” kama saa moja hivi. Kulikuwa na ndege moja tu hapo kiwanjani. Nilisimamisha gari langu, halafu nikatoka na kuanza kutafuta ile nyumba ilikokuwa. Mahala pote palikuwa kimya, baridi ilikuwa kali sana, na moyo ulikuwa unanipiga mno. Nilitafuta kwa muda mrefu kisha ndipo nikaiona. Wakati huo palikuwa pameisha kuwa giza mahala pote.

Moyo wangu ulizidi kupiga na nilinuia usiku huu huu ikiwa nikiwa mzima lazima nihakikishe 'Operesheni N-R-S-U' imefanikiwa. Nilienda ile nyumba pole pole huku nikichunguza huku na huko. Mawazo yangu yote yalikuwa juu ya Sammy kama ni mzima ama ameuawa.

Nilikuwa nimeisha kata shauri kuua kitu chochote kitakachokuja njiani pangum kabla sijaweza kufahamu nini kimempata Sammy.

SURA YA NANE

NILIJUA kama ile karatasi ilikuwa mtego basi watakuwa wananingoja lakini kama hapana basi watakuwa wanadhani kuwa miye nitaenda kumtafuta Sammy kwa Daktari Njoroge huko 'Lavington Green', au kwa Benny huko "Westlands". Nilipozungukazunguka nikakosa kumuona mtu yoyote hivyo nikadhani huenda hawakuwa wakinitegemea. Nilijibanza kwenye ukuta, halafu nikachungulia kwenye dirisha moja; taa zilikuwa zikiwaa humo ndani ya chumba. Nilipochungulia zaidi humo ndani nilimuona Sammy amelazwa kwenye kitanda na amefungwa kwa kamba. Pia alionekana akiwa bado amezimia. Moyo wangu ulifurahi sana na ukanipa nguvu zaidi kuona Sammy alikuwa bado anaishi, ingawaje chini ya hali ya mateso ya ajabu.

Niliwaza jinsi ya kuweza kuingia humo ndani lakini nilishindwa. Dirisha lilikuwa na vyuma ambavyo nisingeweza kuvifanyia jambo lolote! mwishowe nilijitolea nipitie mlango wa mbele, nilikuwa tayari na bastola zangu. Kijana mmoj alikuja kufungua mlango. Nilimpiga ngumi ya shingoni akazirahi papo hapo hata hakuweza kutoa sauti.

Niliingia ndani nikafika kwenye mlango wa sebuleni. Huu mlango ulikuwa wa mbao lakini juu ulikuwa na kioo, Nilipoangalia ndani nikawaona Benny, Lulu na watu wengine kama kumi hivi wote wakinywa kwa furaha sana. Nilifikiria niingie lakini sikuona jambo la maana, maana 'bosi' hakuwemo na bosi ndiye mwenye vitu ninavyovitaka. Hawa watu humu ndani walionekana wameridhika sana na mambo, ila Lulu mara kwa mara alikuwa akiangaza macho huku na huko.

Kisha wazo likanijia, nikarudi nje taratibu ili nikawe tena kwenye lile dirisha la chumba alimo kuwa amefungiwa Sammy. Kabla sijaenda, nilimbeba yule mlinzi wa mlangoni nikamsukumia kwenye mfereji wa maji halafu nikahakikisha kuwa haamuki mpaka baada ya siku tatu hivi.

Nilipofika pale dirishani, nilikata unyasi mmoja mrefu sana hivi ambao nilijua utamfikia Sammy hapo alipolala kitandani. Kweli ulifika. Niliusukumasukuma sikioni mwake mpaka akazinduka. Alipozinduka alitazama akaniona. Alitaka kusema jambo nikamfanyia ishara anyamaze, maana alionekana akili zake bado hazikuwa zinaweza kuunganisha mambo. Kwa sababu mimi ni namwelewa Sana Sammy, nilijua haitamchukua dakika nyingi kabla ajaweza kuelewa nini ni nini.

Baada ya muda kidogo niliona anaanza kutambua mambo, alinitazama akanitingishia kichwa kuonyesha kuwa sasa anaanza kuelewa mambo. Ilionekana kama akina Benny walikuwa wamemponda vibaya sana Sammy hata kuzirai muda wote ule. Na pia ilionekana akina Benny walijua itamchukua muda mrefu sana Sammy kuzinduka ndiyo sababu hawakuwa na wasiwasi.

Nilishawambieni kuwa Sammy ni maarufu kwa visu. Kwa hiyo alinifanyia ishara nimtupie visu ili aweze kukata zile kamba na kujifungua. Ungeweza kustaajabu angezikataje zile kamba maana hapo mwanzoni nilikuwa nimekwambia kuwa walikuwa wamemfunga vizuri sana. Lakini usitie shaka nitakuelelza sasa hivi.

Kichwa cha Sammy hakikuwa kimefungwa yaani kuanzia shingoni. Basi nilimtupia kisu toka dirishani nacho kikaanguka karibu sana na mahali alipokuwa. akajikurupusha huku na huko hadi akafanikiwa kukiuma kwa midomo. Sammy akakata zile kamba kwa kutumia mdomo. Kile kisu ni kikali sana fahamu, hata niseme zaidi ya wembe. Kisha nilimtupia visu vingine kama sita hivi nilivyokuwa navyo. Tulifanyiana ishara ambazo ni sisi wenyewe tu tunazozifahamu.

Miye nilirudi mpaka kwenye mlango wa mbele nione kama ninaweza kufanya lolote. Ilivyokuwa inaonekana mpaka sasa, ni kuwa mahala pa kukutania kati ya Benny, Bosi na wale waliotumwa kuja kuzichukua hizi karatasi ni hapo. Na pia ilivyoonekana hawa watu wataondoka na ndege ndogo kuelekea kwao, ndiyo sababu wakachagua nyumba ya kukutania karibu na kiwanja hiki.

Bado nafikiria la kufanya nikasikia sauti nyuma yangu, na nikasikia mdomo wa bastola unanigusa, “Haya tembea mheshimiwa, kama unadhani kuviziavizia nyumba za watu kunasaidia.”

Sikuwa na la kufanya ilinibidi nifanye kama nilivyo ambiwa. Mlango ule unaoendea sebuleni ulikuwa umefunguliwa nikaingizwa ndani.

“Karibu Willy, nafurahi sana kukuona tena baada ya kunitoroka jana kwa namna ya ajabu. Nimefurahi kuwa nyie watu hamnipi shida ya kuwatafuta ila mnajileta wenyewe. Kaa chini hapo tuweze kuzungumza kidogo kabla ujashuhudia kwa macho yako jinsi tutakavyofulu.” alisema Benny kwa maringo na taratibu sana.

“Asante sana kwa kunikaribisha Benny, lakini nasikitika sana kuwa hutafaulu katika mipango yako, aidha sitakaa nishuhudie ukifanya unyama mimi nikitazama tu.” nilimjibu kwa utaratibu mwingi pia.

Nilikuwa nikiwapa maelezo mengi hayo kusudi waweze kumsahau Sammy kwa muda na hii ingempatia muda wa kuweza kujifungua na kujinyooshanyoosha aweze kuwa tayari kwa vitendo.

Ilipofika kama saa mbili kasoro dakika ishirini hivi. Daktari Njoroge akiwa na walinzi kama wanne hivi aliingia.

Huyu Daktari Njoroge ni mtu mwenye umri wa makamo kama miaka arobaini na mitano hivi. Jinsi mwili wake ulivyokaa unaonyesha utajiri mtupu. Nilipata habari kuwa amesoma sana, na amehitimu kama Daktari huko Uingereza. Uso wake uonyesha furaha kila wakati. Pia uonekana kuwa anatoka katika ukoo ulioendelea vizuri sana.

“Karibu 'bosi' nadhani utafurahi sana nikikutambulisha kwa kiumbe ambaye kwa wakati wote huu amekuwa akitutia wasiwasi sana, lakini sasa tena amejileta na yuko chini ya mikono yetu,” alisema Benny kwa furaha kubwa.

“Endelea Benny, tuweze kufahamiana kabla hajazikwa,” alijibu 'bosi'

“Huyu ni mpelelezi maarufu katika Afrika nzima, bwana Willy Gamba, ambaye anafanya kazi na Idara ya Uchunguzi ya Tanzania, lakini mara nyingi; anafanya kazi bega kwa bega na Idara za aina hii hii za hapa Afrika ya Mashariki.”

“Aisii, mimi naitwa Dr. Dickison Njoroge, tajiri sana katika Afrika Mashariki nzima. Na nimekuwa tajiri hivi kwa ajili ya shughuli za namna hii bwana Willy, kwa hiyo kuniingilia kwako kulikuwa kunapoteza muda na fedha yangu. Lakini hata hivyo napenda sana mioyo yenu ilivyo migumu ya kwamba hata naona wivu. Ubaya ni kwamba, ushujaa wako mwisho wake ni hapa. Na kabla sijaona unakufa, nataka kukuonyesha jinsi miye nilivyo na akili nyingi, na jinsi kundi langu lilivyoundwa kwa uimara kabisa.” alisema Dr. Dickison Njoroge hali akinitazama kwa furaha.

“Siye tuna chama chetu, nacho ni kikubwa sana, kinao wanachama katika Afrika Mashariki nzima. Pia kina uhusiano na vyama vya namna hii hii katika Afrika na hata nchi nyingine za Ulaya. Hapa Afrika ya Magharibi, mimi ndiye rais wa chama hiki na kesho nategemea kuita mkutano ambao nataka tumchague Benny kama Katibu Mtendaji wa chama badala ya Job ambaye mlimuua katika msukosuko huu. Na pia nataka nikueleze waziwazi kuwa chama hiki kina wanachama pia kutoka hata Serikalini. Watu wenye vyeo vya juu kabisa wana hisa katika chama hiki. Kwa hivi ndiyo sababu kila siku siye hatuwezi kushindwa maana “Zimwi likujualo halikuli likakwisha” walisema waswahili.

Katika wizi wa karatasi hizi, mtindo wetu ni ule ule umetumika. Maafisa wetu wa Tanzania na Uganda wote tulishirikiana bega kwa bega mpaka tukafaulu. Na leo baada ya saa mbili na dakika kumi, chama chetu kitakuwa tajiri kuzidi vyama vingine vyote. Siye tunafanya kazi sawa sawa na jinsi nyie kwenye idara ya upelelezi mnavyofanya. Na pia tuna watu mashuhuri kama wewe na wengine kutoka katika idara yenu.

“Miye najua mpaka sasa mnajua tulivyozipata hizi karatasi, lakini najua hamjui jinsi ambavyo zitapelekwa na wapi zitapelekwa.”

“Tunajua Daktari Njoroge usijivunge kuwa akina siye hatujui, hata ambavyo unajidanganya utafanya usiku huu pia tunajua,” nilimjibu huku sauti yangu ikionyesha dharau kubwa.

“Kama unajua basi sijali hata chembe, maana wewe sasa ni sawa na maiti, na kama maiti inajua jambo nani huyo atakayejali?”

“Ulipokuja kwangu na kuharibu mashine yangu, nilipopata habari nilichukia kiasi kikubwa sana ya kwamba miye mwenyewe nataka kushuhudia kifo chako, na pia kwa sababu wewe ndiye mtu wa kwanza kuweza kunigundua mimi nikiwa kama kiongozi wa kundi la wahalifu. Kwa kifupi Bwana Gamba ni kwamba, muda wa dakika ishirini hivi siye tutakuwa watu tajiri kabisa.

“Hizi karatasi zinanunuliwa na watu wa Ureno kwa kiasi cha shilingi milioni mia moja na siye tumezipata kwa kuuza maisha ya watu wetu wengi. Na Serikali imezitafula kwa gharama iliyo kubwa kiasi cha kutisha. Kadhalika imepoteza watu wake mashuhuri kwa ajili ya hizi karatasi na bado wasizipate.

“Mnamo saa mbili kamili, wapelelezi fulani toka Ureno tunaonana nao hapa hapa ndani, na naona zimebaki dakika kumi kufika muda huo, na wakati huo nitahakikisha kuwa nyie mtakuwa mmeishakufa. Hao vijana wakitupatia fedha na siye tutawapatia hizi karatasi. Nao wataondoka na ndege yao moja ambayo itawachukua hapa hapa kiwanjani wakiwa kama watu waliokuja katika maonyesho ya mavazi na ambao kwa sasa wanamaliza maonyesho yao na wanarudi nyumbani. Kwa hivyo hakuna binadamu yeyote ambaye atawatilia tuhuma.

“Wakati wakifika Ureno miye na wenzangu tutakuwa tumegawana fedha, tunakula raha tu. Halafu wapigania uhuru watakapoanza kupigwa naweza kutoa kiasi cha shilingi milioni moja kuwasaidia. Na nakwambia nitatangazwa dunia nzima kama mtu mwenye moyo wa pekee na mwafrika safi. Siku moja utakapofufuka ukiwaambia kwamba mimi ndiye niliyewasaliti kwa kuziiba hizi karatasi na

kuwapa wareno nao wakupigwa vibaya sana, watakushitaki kwa kusema uongo maana tayari watakuwa wananiabudu kama MUNGU wao mdogo kwa kuwasaidia kiasi hicho. Unaonaje si hekima nzuri sana hiyo?”

“Kwa kweli ni hekima nzuri kama ungefanikiwa, Lakini kwa Sababu hutafanikiwa, hata mimi nakuonea huruma ya ajabu. Ni afadhali usingezaliwa bwana Njoroge maana yatakayokukuta hata watoto wako watajichukia kwa nini walizaliwa na baba kama wewe,” nilijibu kwa kiburi sana ingawa sikuwa na bastola hata moja. Bastola zangu walikuwa wameishaninyang'anya.

Nilikuwa na uhakika kuwa, wakati huu lazima Sammy ameishakuwa tayari, alikuwa tu anangoja kuwagutusha. Lulu alikuwa akinitazama kwa macho ambayo yalikuwa yananiambia hadithi za sungura nilizosisoma darasa la tatu. Alikuwa naye ameshikilia bastola mikononi mwake. Benny na vijana wengine walikuwa na furaha ya ajabu maana 'bosi' alikuwa akiwatukuza namna ya jabu.

Kamfungulieni huyo mbwa mwingine humo ndani, nadhani atakuwa bado amezimia, nataka kuwaona wanakula marisasi mbele yangu mwenyewe. Maana naona huyu Gamba ni mshenzi kiasi cha kwamba hanitambui sawa sawa. Kuwa rais wa chama kama hiki, lazima atambue kuwa mimi ni mtu wa pekee, na pia mwenye busara za pekee,” alisema 'bosi' huku akimtazama Benny.

Benny alimueleza kijana fulani hapo akafungue mlango - Lulu tu ndiye alionekana hana furaha, huku rangi yake ikizidi kubadilika. Nilidhani huenda anachukia kuona bado naishi. Nilimtazama huku nikitabasamu kisha nikamwambia, “Wewe malaya unachelewa kwenye maonyesho, watu wanakungoja ukawaonyeshe mwili wako huo usio na bei. Mana ni mtu fisadi tu ambaye hathamini mwili wake kiasi cha kuonyesha kwa kila mtu.” Lulu hakujibu neno ila tu alitazama chini.

Benny aliniangalia kwa hasira nyingi akasema, “wewe rafiki yangu, huwezi kumwadhiri mke wangu kiasi hicho hali mimi nipo hapa. Hiyo dharau kubwa sana mshenzi wewe.”

“Yeeeeeeeya, wewe kweli uko nyuma, unadhani huyu fisadi anaweza kukaa na wewe! humjui nini, mbona hukuniuliza zamani nikueleze, maana mimi nina historia yake toka A mpaka Z.” nilisema huku nikicheka sana.

Benny alitaka kusema neno lakini kabla hajasema, yule kijana aliyeenda kufungua mlango wa chumba ambamo alifungiwa Sammy alianguka chini na kisu kifuni. Wote walisimama na kuanza kutoa risasi upande ule wa chumba miye niliruka nikaanguka chini ya sofa.

Mle ndani mlikuwa na watu kama kumi na watano hivi wa upande wao. Na miye nilijua Sammy ana visu sita kwa hiyo nilijua watu sita watakuwa wameishakufa kabla hawajatuandama. Lulu alisimama kama anataka kukimbia halafu kwa bahati mbaya akaangusha bastola yake kwenye kichwa changu. Basi niliona sasa tumeishaokoka, maana kama Sammy ataua sita miye wale wengine nitawafanya kazi kabla hizi risasi hazijaisha. Risasi sasa zilikuwa zinapigwa upande wangu na kule mlangoni kwa Sammy. Sammy alifanya mlango kama ngao yake.

Mimi nilianza kazi. Niliposimama niliona watu watano wameishaanguka. Basi miye niliwalisha waliokuwa karibu yangu. Nilipoona mwingine anakula visu nilijua sasa Sammy ameishiwa visu kwa hiyo ilikuwa sasa ni kazi yangu kumuokoa Sammy. Nilijaribu kumpata Benny lakini wapi. Wengi wao walikula risasi mpaka nikaona wamebaki wanne. Benny, Lulu, 'Bosi' na kijana mwingine. Walipoona mambo yamewazidia, walionelea wakimbie. Kweli walikimbia na kupotelea gizani.

Nilimfuata Sammy, nikampa heko kwa kazi yake nzuri aliyokuwa ameifanya kwa wakati huo. Aliniuliza nilipataje bastola nikamweleza iliangukwa na Lulu kwenye kichwa changu wakati nikijificha nyuma ya sofa kuzuia risasi.

“Miye sikubali kuwa aliangusha kwa bahati mbaya Willy, kila siku nakwambia wanawake wazuri ni sumu huenda ana jambo, maana tangu wanishike kule kwake tabia yake Lulu imenishinda. Jinsi anavyojiheshimu ni ajabu.”

“Hata mimi nimemuona hakuwa na furaha wakati wengine wote walipokuwa wanafurahia sana. Sasa tufanye nini Sammy, maana hatujui hawa watu wamekimbia wapi.”

“Mimi nadhani, tukusanye hizi maiti tuzifiche mahala fulani. Kwanza naona bado dakika nne wale wapelelezi wa Ureno wafike hapa. Mimi naona tuwangojee hao hapa maana hawatakuwa na habari kuwa siye ndio tumo humu. Wakija tutawafungulia tukijifanya kama sisi ni walinzi wa Njoroge na kundi lake. Watakapokuwa wameingia ndipo sisi tuwageukie mbogo na kuwaua wote. Lakini lazima tuwe macho maana jua hawa watu pia ni wa kazi kama yetu kwa hiyo lazima wanaweza wakang'amua jambo fulani wakatuwahi kabla hatujawawahi. Pia lazima tuwe tunajua kuwa Benny na kundi lake wanaweza kurudi upesi iwezekanavyo kusudi waje wawazuie hawa watu, au awje na kundi la kuweza kutumalizia mbali. Lakini hii itamchukua muda mrefu kidogo hivyo tutaweza kupata nafasi ya kuwacheza hawa watu.”

Mawaidha ya Sammy niliyaona kuwa muruwa kabisa. Tulikusanya zile maiti na kuzitia kwenye chumba fulani. Halafu tukakaa tayari kuwangoja hao binadamu. Nilichukua bastola tatu toka kwa maiti hizo za kundi la Benny, na Sammy pia. Tukajitayarisha vizuri kabisa, maana mara hii tutapambana na watu waliofundishwa kazi hii hii kama sisi.

Mlango uligongwa, miye nilienda kuufungua, Sammy alijificha kwenye chumba kimojawapo, “Come in, the boss is waiting for you,” yaani”karibu ndani 'bosi' anawangojea.”

Thanks a lot” yaani” Asante sana, “walijibu. Walikuwa wavulana wanne na wasichana wawili, nilingoja wote waingie halafu mimi niwatokee kwa nyuma. Yule wa mwisho alipoingia, alitoa bastola mara moja na kuniuliza mahali alipo 'bosi'. Lo, nikaona hapa mambo yatachaga.

Akaniambia nisitoe sauti, pia akaniuliza idadi ya walinzi wanaomlinda 'bosi'. Nikasema kumi na wanne. Akamweleza na mwenzake akamkubalia kuwa wanaweza kuwashinda tu, ila wakaambiana kuwa lazima wamgutushie 'bosi' na watu wake halafu wachukue hizo karatasi kwa nguvu kisha watoroke.

Unaona sasa mambo yalivyokuwa yanachaga. Miye yaliyokuwa yananitisha sasa. Maana kumbe hawa watu hawakuja na fedha, ila tu walikuwa wamemfanyia 'bosi' akili, waje humu ndani kisha wawanyang'anye hizo karatasi kwa nguvu, halafu wawaue ndipo watoroke na hizo karatasi kwenda zao bila kulipa fedha hata senti moja.

Alitaka kunipiga shingoni na kitako cha bastola, lakini kabla hajaniwahi miye nikakinga kwa mkono na ile bastola ikaruka. Hapo hapo nikatoa zangu vita ikaanza.

Hawa wote sita walionekana watu wanaijua kazi yao barabara. Sammy alitokeza kwa nyuma kwa hiyo tukawaweka mahala pema sana. Fahamu mpaka sasa miye fulana yangu nilikuwa bado ninayo, kwa hiyo ilizidi kunisaidia sana. Mapigano kati yetu na kundi hili yalikuwa makali kupita mengine yote yaliyokuwa yameishapita. Mwishowe tulishinda, wanne wao tulikuwa tumeisha waua na wawili wengine walikuwa wamejeruhiwa vibaya sana.

Tuliwaendea hawa waliojeruhiwa, wakatuuliza siye ni nani, tukawaeleza kila kitu. Nao wakatueleza kuwa kusema kweli nia yao haikuwa kulipa pesa zote hizo, maana serikali yao ni maskini sana kuweza kulipa pesa nyingi namna hiyo. Ila tu

walikuwa wamemdanganya Njoroge na chama chake kusudi waweze kuzichukua hizo karatasi bila malipo yoyote.

Sasa lililokuwa limebaki ni kupambana na Njoroge. Tuliona hii itakuwa kazi rahisi zaidi. “Miye Willy naona tungoje hapa maana Benny lazima atarudi, na mimi nataka nimwue Benny maana ndiye aliyemwua Robin, na mimi niliapa nitamwua mtu aliyemwua Robin asiponiua yeye,” Alisema Sammy.

“Vema, tutawangoja hapa.”

Kidogo tu, simu ililia.

“Hallo, ni nani?” Nilijibu huku nikiuliza.

“Sikiliza, njoni karibu na Railway Training School hapa Nairobi South, kuna nyumba moja mfano wa ghorofa chumba nambari saba. Hapa ndipo walipo kwa hiyo msikawie. Bado wanajaribu kukata shauri mahala pa kwenda. “Hii sauti ilikuwa kama ya mwanamke ingawaje ilibadilishwa na kusikika kama ya mwanaume. Tulikata shauri tufanye kama tulivyoambiwa.

Tulienda mpaka karibu na RTS, halafu tukaanza kuitafuta ile nyumba, hii ilituchelewesha sana hata tukadhani tutakuta wameisha toka humo ndani. Mwishoni tukaiona, na hapo tukaenda ndani. Tukaenda mpaka chumba nambari saba. Tulipofika tukapiga mlango kwa nguvu, mpaka ndani.

Nakwambia tulipoingia hatukuamini hata kidogo. Lulu alikuwa ameshikilia bastola mbili mkononi, Benny na 'bosi' wamekaa huku wameinua mikono juu.

“Fanyeni haraka, wamemtuma mtu kuleta kundi jingine la watu. Watafika sasa hivi,” alisema Lulu.

“Hii ina maana gani Lulu,” aliuliza Benny.

“Mimi ni mpelelezi kutoka Uganda, ila nilifanya kazi nanyi nikijua tungeweza kuwashika vizuri sana. Tulikuwa na John katika kazi hii. Na ni John tu aliyekuwa akijua kazi yangu. Ulikuwa mpumbavu sana Benny uliponipenda sana. Nami niliwala akili vizuri sana hata wote mkaangukia upande wangu,” alisema Lulu huku akimwemweseka.

“Unaona sasa mjomba mambo yalivyo zidi kunyumbulika. Kumbe Lulu alikuwa upande wetu. Kwanza siku ile Benny alipotaka kutuchoma na petroli, Lulu alisema wamwendee 'bosi', huku akaponya maisha yetu. Kadhalika na kule chumbani

'Wilson Airport' aliniangushia bastola. Halafu nikiwaambia wasichana ni sumu nyie mnanidhania mimi ni mpumbavu’’

“Wapi karatasi?” Nilimuuliza Daktari Njoroge.

“Zipo hapa,” alizitoa huku akitetemeka.

“Wale Wareno wote tumeisha waua, lakini kabla hujafa nitakueleza kuwa uhalifu haulipi hata kidogo. Wale watu nao walikuwa wamekuzunguka. Nia yao ilikuwa kukunyang'anya hizo karatasi kwa nguvu, halafu wakuue, unaona hiyo,” nilimweleza huku nikienda kuzichukua hizo karatasi. Niliziangalia nikahakikisha kuwa kweli zilikuwa zenyewe.

Hatukutaka kupoteza wakati kwani tulihofia kukutwa na hilo kundi jingine la wahalifu hawa. Hivyo haraka tukapiga simu polisi. Si baadaye motakaa ya polisi ilisimama nje ya jumba hili tulimokuwa, punde askari polisi kadhaa wakaingia tulipokuwa. Nyuso zao ziliainisha ghadhabu iliyokithiri kiwango. Haikosi kila mmoja wao alichukizwa sana na hila za wasaliti hawa ambao ati ni pamoja na wazalendo wa Afrika!

Moyo wangu ulirudi kwa Lina. Kama mwehu, nikawaacha wote na kutia gari moto kwenda kumwona Lina maana mpaka sasa moyo wangu ulikuwa bado ukiniuma kwa ajili yake.

Nilipofika kwa daktari nilingia kwa fujo sana maana nilikuwa na hamu ya kutaka kusikia nini kimempata Lina.

“Daktari, Lina vipi?”

“Naona ataishi, ila kwa sasa usiende kumwona maana unaweza kumsumbua,”

Hata, lazima nimwone, nisipomwona naweza kuzimia,”

“Hapana usiende kumwona tafadhali.”

“Nyamaza daktari.” Nilimvuta daktari mkono. Akaona hana la kufanya ila kufanya kama ninavyomwambia.

Nilipoingia Lina alikuwa amesinzia. Nilimwinamia na kuanza kumbusu ovyo. Daktari alicheka akasema. “Naona kweli mapenzi ni hatari-yaweza kuua.” Akafunga mlango akaenda zake. Lina alifungua macho yake.

“Oh Willy, nilikuwa nakuota sasa hivi umenikumbatia, kumbe ni kweli. Oh, sasa nimepona kabisa, nibusu Willy nikarejewe na uhai.”

“Lina, Lina mpenzi, mimi na wewe mpaka kwa mama Willy kifo ndicho kitakacho tutenganisha.”

MWISHO